

# MSHAMBA

*Flani Hivi!*

Bro Elihuruma Maruma

## **MSHAMBA FLANI © 2020 ELIHURUMA MARUMA**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhuswi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yejote ya kitabu hiki kwa njia, namna na mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.

**SIMU:** +255 752/ 715 307 008

**Facebook:** *Eliburuma Maruma*

**Instagram:** *@bro.elly247*

**Email:** *ellyrealspeaker@gmail.com*

**ISBN:**

Kimepigwa chapa na:

**CLIMAX SOLUTIONS - ARUSHA**

**+255 658 288 054 / +255 687 699 862**

*climaxsolutions8@gmail.com*

# YALIYOMO

WAKFU.....	vi
SHUKRANI.....	vii
1 .....	1
<b>MKALAMA, SINGIDA .....</b>	<b>1</b>
2 .....	4
<b>CHUO KIKUU MLIMANI.....</b>	<b>4</b>
3 .....	9
<b>MAPENZI SAFARI .....</b>	<b>9</b>
4 .....	16
<b>SAKINA, ARUSHA.....</b>	<b>16</b>
5 .....	23
<b>MTOTO WA NYOKA NI NYOKA!! .....</b>	<b>23</b>
6 .....	28
<b>ZALI NA SHIBE .....</b>	<b>28</b>
7 .....	33
<b>ONE DAY GAME .....</b>	<b>33</b>
8 .....	38
<b>TOM BOY!! .....</b>	<b>38</b>
9 .....	43
<b>SAKATA LA UTEUZI.....</b>	<b>43</b>
10 .....	47
<b>ZAMA UWEPONI .....</b>	<b>47</b>
11 .....	54
<b>MBWEMBWE DARASANI.....</b>	<b>54</b>
12 .....	59

<b>WAKAMATA WINGU.....</b>	<b>59</b>
13 .....	62
<b>KULA UJANA .....</b>	<b>62</b>
14 .....	67
<b>MATUNDA YA MWANA!!.....</b>	<b>67</b>
15 .....	70
<b>MAISHA YA HOSTELI.....</b>	<b>70</b>
16 .....	73
<b>WALOKOLE WAKUTANA.....</b>	<b>73</b>
17 .....	76
<b>BASH &amp; BONANZA .....</b>	<b>76</b>
18 .....	86
<b>SIKU KUU!!.....</b>	<b>86</b>
19 .....	91
<b>KASHI KASHI DARASANI .....</b>	<b>91</b>
20 .....	95
<b>006 MAFIAN GANG.....</b>	<b>95</b>
21 .....	103
<b>AKISI YA MSHAMBA.....</b>	<b>103</b>
22 .....	106
<b>UFUSKA KAZINI.....</b>	<b>106</b>
23 .....	112
<b>EXPERIENCING UTAMU .....</b>	<b>112</b>
24 .....	115
<b>VURUMAI ZA UCHAGUZI!.....</b>	<b>115</b>

25 .....	119
<b>MISS UNIVERSITY!</b> .....	<b>119</b>
26 .....	123
<b>JIMMY “The INVISIBLE”</b> .....	<b>123</b>
27 .....	138
<b>KIROBA KUNDUCHI!!</b> .....	<b>138</b>
28 .....	142
<b>MBUDYA ISLAND!!</b> .....	<b>142</b>
29 .....	148
<b>CHEERS!!</b> .....	<b>148</b>
30 .....	150
<b>SUPPLEMENTARY CASE</b> .....	<b>150</b>
31 .....	155
<b>QUEEN MAUTINI!</b> .....	<b>155</b>
32 .....	157
<b>NAMBALA, TENTERU</b> .....	<b>157</b>
33 .....	159
<b>PENZI PENZINI!!</b> .....	<b>159</b>
34 .....	161
<b>TOM BOY PENZINI!!</b> .....	<b>161</b>
35 .....	164
<b>BAHATI YA MTENDE!!</b> .....	<b>164</b>
36 .....	167
<b>MSHAMBA ULAYA!!</b> .....	<b>167</b>
KIPANDE MUHIMU.....	169

**WAKFU**



Riwaya hii ni Mahususi kwa Vijana wote!

# **SHUKRANI**



1. Mungu Mkuu YHWH aliyenipa Neema ya kipawa hiki.
2. Familia yangu kwa nafasi ya kutosha kutumika kwenye Ufalme.
3. Kaka Ambwene Nkwera kwa Uchapaji wa Kitabu, Esuvath Mollel kwa kukipitia, Elifuraha na Neema kwa picha za kava.

# 1

## MKALAMA, SINGIDA

**Z**ilisikika kwa mbali sauti nzuri za ndege pamoja na majogoo machache yakiwika japo kwa uchovu kwa sababu ya baridi na upepo mkali wa kiangazi. Giza nalo lilikuwa bado totoro na hapakuwa na mwanga wa aina yejote nje. Hivi ilikuwa ni mishale ya saa kumi usiku kuelekea saa kumi na moja. Katika hali hiyo ilisikika pia sauti ya mguno na mahangaiko ya mwanamke mmoja aliyezeka katika nyumba ndogo ya udongo yenyeye vyumba viwili iliyezekwa kwa nyasi.

Mwanamke huyu makamo mwenye umri wa miaka 44 aliyejulikana kwa jina la Wankembeta alikuwa mjamzito, na ukulele huu ulikuwa ni wa uchungu wa kujifungua. Mama huyu mjane alifiwa na mumewe miezi nane iliyopita alikuwa amejilaza kwenye kitanda chake cha Kamba pamoja na mdogo wake aliyeitwa Lumba. Kwa namna usingizi wa alfajiri unavyokuwaga mzito na mtamu ulimchukua Lumba takribani dakika kumi kugundua hiyo hali, kwa lile wenge la asubuhi akaanza kuita “Dada!! Dada!! kuna tatizo gani jamani?” Kisha ghafla bila hata ya kujibiwa akakumbuka dada yake ni mjamzito na siku zake za kujifungua zilikuwa zimekaribia sana, na hiki ndicho hasa kilimfanya aondoke nyumbani kwake na aje kuishi na dadake

hapo kwake. Hivyo kwa haraka haraka akajifunga kaniki lake vizuri, akafungua mlango na kutoka nje huku akikimbia moja kwa moja mpaka kwa Bibi Mkombo. Bibi Mkombo ni moja kati ya wakunga wa jadi maarufu pale kijijini kwao, na huwa anaaminika zaidi kwa namna ambavyo huwahudumia wamama wanaojifunga kwa mafanikio.

Kama baada ya dakika kumi na tano ilisikika sauti ya mtoto akilia ndani ya nyumba ya Mwankembeta. Hii ilikuwa sauti ya mtoto wa kiume aliyezaliwa na Mama huyu wa Kinyiramba, Mama ambaye kila mtu alikuwa amemkatia tamaa kwamba hato zaa tena kwa sababu ya umri wake. Cha ajabu alizaliwa mtoto wa kiume mwenye afya njema sana. Vilisikika vigelegele vya nguvu sana toka kwa Lumba na Bibi Mkombo wakishangilia ujio wa mtoto mwanaume kwenye familia hii kwa mara ya kwanza. Na sio mtoto mwanaume tu bali ni mtoto wa kwanza na wa pekee kwenye familia hii.

Wankembeta Makalla na Jonathan Mkumbo walioana kwa ndoa ya jadi miaka zaidi ya 25 iliyopita. Na katika Maisha yao yote hawakubahatika kupata mtoto. Asubuhi hii ya tarehe 24/07/1988 siku ya Jumapili Alfajiri na ndipo sasa kwa mara ya kwanza mtoto alizaliwa katika familia hii bila uwepo wa babake. Bi Wankembeta aliwaambia Lumba na Bibi Mkombo kwamba mtoto huyu ataitwa MASHAURI na ni kwa sababu waliingia mashauriano na mumewe marehemu Mzee Mkumbo ya kwamba wajaribu bahati yao tena kabla Mama huyu hajafikisha umri wa miaka 45, maana angekuwa ameingia umri ambao asingweza kuzaa tena kwa urahisi. Mambo yote haya yalikuwa yanatokea katika Kijiji cha Kinyambuli kilichopo kata ya Nkito, Wilaya ya

Iramba, Mkoani Singida. Wilaya hii ya Iramba kwa sasa imegawanyika na maeneo haya yapo kwenye Wilaya mpya ya Mkalama.

Kijiji cha Kinyambuli ni Kijiji ambacho idadi kubwa ya wakazi wake ni Wanyiramba, ijapokuwa kuna idadi ndogo ya watu wa kabilalau Wanyisanzu. Kijiji hiki kipo katikati ya vijiji vya Mazangili na Muli, lakini pia ni jirani na Kijiji cha Malaya. Wenyeji wa vijiji ni maarufu kwa ufugaji wa Ng'ombe, Kuku, Mbuzi na Kondoo pamoja na Punda, lakini pia wanajishughulisha na kilimo cha Dengi, Alizeti, Mtama, Mahindi na Karanga kwa sehemu.

Kabila la Wanyiramba ni kabila lililojaliwa watu wa kazi, namaanisha watu ambao wanajua kufanya kazi kwelikweli. Kama ni kulima wanalima kwelikweli. Mpe Mnyiramba wa asili kazi ya mikono kisha utaona uwezo wao katika utendaji kazi. Hawa ni maarufu pia kwa ulaji wa NYAMA kiasi kwamba huwa wana utani wao ambao huwa wanasema “NAMA ni NAMA” wakimaanisha NYAMA ni NYAMA yaani wanakula nyama ya mnyama yeyote maadam tu ni nyama. Lakini pia vyakula vyao maarufu ni Ugali wa mtama kwa Mlenda, pamoja na Makukuru. Na kinywaji chao kikuu ni TOGWA, kinywaji kinachotengenezwa kwa Mtama uliolowekwa ukaachwa kwa muda yaani “Kimera” kinywaji hiki hutumika zaidi katika msimu wa kilimo katika hamasa ya kazi. Lakini pia hutumika mara moja moja kama kifungua kinywa asubuhi.

Hivyo kijana Mashauri alizaliwa miezi nane baadae tangu kufariki kwa Baba yake mzazi Mzee Jonathan Mkumbo.

# 2

## **CHUO KIKUU MLIMANI**

**T**arehe 02 mwezi wa 10 mwaka 2008 ilionekana foleni ndefu sana kwenye ukumbi wa Nkurumah, moja ya kumbi maarufu zaidi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam maarufu kama Mlimani. Foleni hii ilikuwa ya wanafunzi wapya waliodahiliwa Chuo Kikuu Dar es Salaam kwa masomo ya Shahada kwa kozi mbalimbali. Katika foleni hii mwishoni alionekana mvulana mmoja mfupi mweusi mwenye mwili unao onyesha ukakamavu wa kutosha, kijana huyu alivalia shati la satini la kung'aa la rangi ya pinki lenye mikono mirefu ambalo hakulichomeka kwenye suruali, na chini alivalia suruali nyeusi pana na ndefu iliyofunika viatu kiasi kwamba ilikuwa ngumu kujua amevaa kiatu cha aina gani. Ungemuangalia kwa haraka haraka ni kwamba mtu aliyevaliwa na nguo badala ya kuvaan nguo. Ama ungeweza kusema pengine nguo sio za kwake na hivyo amezaima. Mkononi alikuwa ameshikilia rundo la vyeti mbalimbali tayari kwa ukaguzi, maana hiki ndicho ambacho kilikuwa kinafanyika kwa wanafunzi hawa ambao ndio walikuwa kwenye mchakato wa Usajili.

Kijana huyu hakuonekana kuongea na mtu zaidi ya kushangaa shangaa huku na kule, midomo yake ilikuwa mikavu

sana na kwa kuwa mchana ule kwa joto la Dar es Salaam hakuonekana kama amepata walau sahani ndogo ya chakula wala kikombe cha maji. Huyu alikuwa kijana Mashauri aliyekuwa amesimama mwishoni kabisa mwa foleni ile ndefu inayokatisha tamaa kwamba atafika saa ngapi ili asajiliwe. Wakati akiwa amesimama mwishoni mwa ile foleni akiwa amechoka sana, huku wanafunzi wenzake wakimshangaa na kumuangalia kichinichini huku wakijiuliza huyu MSHAMBA wa wapi? Ghafla ikatokea gari ndogo aina ya Toyota Mark II balloon nyeusi, ile gari ilionekana mpya kabisa kana kwamba ni kama mhusika alikuwa ndio kwanza ametoka nayo bandarini. Ile gari ilikuja na kusimama kwenye moja ya vile vibarara vyta karibia na ukumbi wa Nkurumah karibu kabisa na ilipoishia foleni ile ndefu ya wanafunzi na nukta chache kutoka alipo Mashauri ambaye ndiye alikuwa mwishoni mwa foleni. Wakati wanafunzi wengi walikuwa wanashangaa na kuonyeshana ile gari, kutoka kwenye ile gari, alionekana kushuka msichana mrembo sana aliyevalia blauzi nyeupe juu iliyombana na suruali nyeusi nyepesi iliyomkaa vizuri sana. Kwa namna alivyoumbika yule binti macho ya watu wote yalihamu kuangalia gari na yakaanza kumuangalia yule binti. Alikuwa binti mwenye urefu wa wastani, mweupe pee mwenye kasura kazuri cha kitoto huku mtaani wanaita “Baby Face” kichwani alikuwa amechana nywele zake vizuri zilizoonekana za asili zisizojua hata harufu ya dawa. Chini alikuwa na umbo pana la wastani huku hipsi na nyuma pakionekana vema bila kutumia nguvu kubwa. Huku juu kuanzia kiunoni alikuwa mwembamba na kifua kidogo, kwa namna alivyo juu na chini usingedhania kama ni mtu mmoja, kwani amejazia sehemu ya chini baada ya kiuno chembamba na juu baada ya kiuno ni mwembamba mwenye kifua

kidogo kinachovutia sana. Binti huyu alishuka akiwa na pochi yake pamoja na bahasha ya vyeti mkononi, na kaja moja kwa moja mwishoni mwa foleni aliposimama Mashauri.

Cha ajabu wakati haya yote yakiendelea, Mashauri aliye kuwa karibu na huyu Binti Mrembo hakuonekana kuelewa wala kushangaa hata kidogo juu ya kile kilichokuwa kinaendelea badala yake kila mda alikuwa anaangalia foleni kama inasogea au la huku akipiga miayo ya njaa na uchovu wa Safari ndefu ya kutoka Singida.

“Kaka, habari yako?” sauti nyororo naya upole ya Lulu ilisikika ikimsalimia Mashauri. “Nzuri” Mashauri alisikika akijibu kwa mkato sana.

“Samahani, eti hapa wanakagua vyeti gani?” Lulu alimuuliza tena Mashauri kwa upole. Mashauri kwa uchovu na sauti yake nzito yenye bass alijibu “cheti cha kuzaliwa, kidato cha nne, result slip ya six na barua ya kudahiliwa hapa” “Ahsante sana Kakangu,” Lulu alishukuru.

Wakati haya yakiendelea wavulana wengi walitamani sana waipate ile nafasi ya kuwa karibu na Lulu kwenye ile foleni, kiasi kwamba waliokuwa mbele walitamani kurudi nyuma ila wakaona ni kujichoresha.

Baada ya maelezo ya Mashauri, Lulu alitoa Vyeti husika kwenye ile bahasha yake na akakaa nyuma ya Mashauri kwenye ile foleni. Wakati Lulu amesimama nyuma ya Mashauri kwenye foleni, kwa macho ya kuibia ya kidada alianza kugundua mambo machache juu ya Mashauri. Kwa kuwa Lulu ni mrefu na Mashauri

ni mfupi sana, Lulu aliweza kuona kwa urahisi cheti cha kidato cha nne cha Mashauri kilichoonyesha ufaulu wa Daraja la 1.7 na Result Slip yake iliyoonyesha Ufaulu wa Daraja la 1.4 kwa masomo ya PCM yaani Physics, Chemistry na Mathematics na kwamba amesoma Mzumbe Boys High School. Wakati huo Mashauri hakuwa anaelewa kinachoendelea, yeye alikuwa anaendelea kuangalia foleni inayosogea walau kwa haraka haraka sasa kuliko kabla, na hii ikampa sana moyo. Japo bado kila baada ya dakika chache alikuwa anapiga sana miayo na kujinyoosha. Lulu alivyoona Mashauri anapiga sana miayo na namna midomo yake ilivyokauka, aligundua kwamba huyu kijana amechoka sana maskini, lakini pia ana kiu na hajala chochote.

Mara akakumbuka ana chupa ya maji ndogo ya Kilimanjaro na Biskuti za Chokilate ambazo alikuwa hajazitumia bado. Taratibu aliingiza mkono wake kwenye pochi yake akatoa yale maji na ile biskuti, alianza kusita kumpa hasa alipokumbuka huyu kijana alivyokuwa anajibu kifupi na bila hata kumuangalia usoni. Wakati anataka kusita kumpa, akakumbuka Mama yake mzazi aliwahi kumwambia “Mwanangu wajibu wako ni kutenda wema, aidha ukikataliwa au usipoambiwa ahsante hiyo siyo juu yako”. Hii ikampa nguvu, kwa mkono wake laini akamgusa Mashauri bega na kumwambia “Kakangu samahani, inaonekana umechoka sana, lakini pia una kiu na njaa. Tafadhali naomba upokee haya maji na hii biskuti, kisha nipe vyeti vyako nikushikie foleni walau uende pale nyuma ukapunguxe njaa na kiu”. Kwanza Mashauri kwa ile pupa tu na njaa kali kidogo apige magoti kushukuru kwa ule muujiza, ila Lulu akamzuia. Waliokuwepo

kwenye foleni na ambao kila wakati wakimuangalia yule msichana hawakuamini kinachotokea.

# 3

## MAPENZI SAFARI

**U**siku huu Hamidu hakulala kabisa, maana kama kuna kitu hakipendi basi ni kusafiri na magari yanayoondoka alfajiri na mapema. Alilala na kushtuka kila wakati, na kila aliposhtuka aliangalia saa yake na kuona bado bado kidogo. Ilaa awamu ya mwisho aliposhtuka saa kumi kasoro za usiku, aliona hana sababu ya kuendelea kulala tena. Alielekea bafuni kuoga, kisha akavaa na akawa tayari kuelekea stendi ya mabasi Mijini Bukoba.

Mzee Mhina almaarufu kama Mbaba wa Mji ni Baba yake mzazi wa kijana Hamidu Mhina. Mzee huyu ni mwanajeshi mstaafu, mara baada ya kustaafu jeshini akiwa kambi ya Lugalo ambapo ndio kambi yake ya mwisho na ambapo alidumu hapo kwa miaka zaidi ya mitano. Mzee Mhina alistaafu na cheo cha Luten Kanali akiwa na miaka takribani 60. Mzee huyu ni mcheshi sana na mpenda haki mno, mara baada ya kustaafu aliamua kurudi kwao Bukoba ili aendelee kuwekeza nguvu zaidi kwenye biashara zake za maduka na nyumba za kulala wageni. Isingekuwa rahisi ukatishe mitaa ya Bukoba Mjini miwili mitatu bila kukutana na aidha Mhina Shop au Mhina Executive Lorge ama Mhina Gest House. Pamoja na kuwa na maduka Zaidi ya 10 makubwa na

Guest Houses Zaidi ya 5 Bukoba Mijini, bado alikuwa na maduka mengine makubwa matatu Muleba Mjini. Kwa asili Mzee Mhina yeye ni Mhaya wa Mleba. Mzee Mhina watu wengi walipenda kumuuta Mbabe wa Mji kwa sababu ya tabia yake ya kutotaka mtu aonewe, popote akigundua kuna mtu anaonewa basi lazima ataingilia ugomvi na kumtetea anayeonewa kwa kumshughulikia anayeonea. Pamoja na kuwa na umri wa miaka Zaidi ya 65 sasa lakini bado alikuwa na nguvu za kijana wa miaka 40, na kwa namna alivyokuwa mrefu wa kimo na mwili wake umejengeka vizuri ilikuwa rahisi sana kumshughulikia mtu yejote. Vijana wote wahuni wa mjini walikuwa wakimuona anapita walipokaa aidha walitawanyika ama waliacha wanachofanya na kumsalimia kwa adabu.

Mzee huyu alijaliwa watoto wanne na wote ni wa kiume, na pamoja na dini na uwezo wake kumruhusu mke zaidi ya mmoja, Mzee Mhina alibaki kuwa na mke wa ujana wake Bi Husna. Katika watoto wake wanne wa kiume, watatu wote walikuwa wanajeshi tayari na wa mwisho alikuwa Hamidu ambaye ndo kwanza alikuwa amemaliza kidato cha sita. Moyoni mwake Mzee Mhina alidhamiria kwamba Hamidu achague kuwa mtu mwingine yoyote ila sio kuwa mwanajeshi. Siku zote mzee Mhina alimsisitiza sana Hamidu kwamba “Mwanangu kaka zako wote ni Wanajeshi tayari. Tafadhali wewe chagua kitu kingine cha kufanya sitakuingilia ila sio jeshi”.

Hamidu alimuelewa sana baba yake, na alidhania kuchagua njia tofauti. Pamoja na kusoma kidato cha kwanza mpaka cha sita kwenye shule ya jeshi, bado Hamidu aliamua kuwa mwanasheria. Hamidu aliyefanana sana na Baba yake Mzee

Mhina kuanzia sura mpaka umbo, alisoma kidato cha kwanza mpaka cha nne Makongo Sekondari na hatimaye kidato cha tano na sita alisoma Jitegemee Sekondari.

Alfajiri hii na mapema Mzee Mhina na mwanae Hamidu walikuwa kwenye gari aina ya Land Rover Tdi wakitokea mtaa wa Kashai uliopo karibu na Uwanja wa Ndege wa Bukoba lakini pia karibu na Ziwa Victora. Mzee huyu kwa furaha alikuwa amempeleka mwanae stendi kuu ya mabasi Bukoba tayari kwa safari yake kuelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alidahiliwa kwa ajili ya kusomea Shahada ya Sheria. Usiku huu wa kuamkia leo Mzee Mhina aliamua kwenda nyumba yake ya Keshai ambapo kwa kawaida humo huishi watoto wake wanapokuwa likizo, lengo lake ilikuwa ni kumpa mausia Hamidu mtoto wake wa mwisho wanaefanana kila kitu isipokuwa tabia. Kikawaida Mzee Mhina huishi na mkewe Bi Husna kwenye jumba lao la kifahari lililopo Mtaa wa Rwanishenye ambao upo kilomita 2 kama unatoka stendi ya Bukoba kwenda Bukoba Mjini. Mzee Mhina aligundua kwamba Hamidu pamoja na kufanana nae sana kimuonekano kitabia Hamidu alikuwa mtu wa vurugu, visasi na asiyependa haki. Na swalii kubwa Mzee Mhina alimuuliza Hamidu ni “With these kind of characters, What kind of Lawyer are you going to be?” Akimaanisha kwa namna hii ya tabia ulizo nazoz, utakuwa Mwanasheria wa namna gani? Lakini kwa Hamidu iliingilia sikio hili na kutokea sikio lingine.

Hatimaye walifika Stendi kuu ya mabasi ya Bukoba, na Hamidi aliagana na Babake na kisha akaingia kwenye basi la Princess Muro linalofanya safari zake Bukoba – Dar. Kikawaida Hamidu anapokwenda kukata tiketi huulizia nafasi ambayo abiria

mwingine atapandia aidha Muleba au Biharamulo, lengo lake ni kutaka kuyatumia yale masaa ya awali kama mawili mpaka matatu kujiachia kwa kulala kwa raha zake. Kikawaida kutoka Bukoba mpaka Biharamulo ni kati ya masaa mawili na nusu mpaka matatu, muda ambao ungemtosha kabisa Hamidu kulala bila bugudha. Na ndivyo ilikuwa, asubuhi hii Hamidu alikaa siti iliyoandikwa C1 yaani dirishani na nafasi ya pili C2 ambayo ndio ilikuwa pamoja na C1, abiria wake alitakiwa kupandia Biharamulo. Baada ya kama dakika kumi tangu Hamidu kuingia kwenye gari, Princess Muro ilianza safari yake tayari kutoka Bukoba kuelekea Jijini Dar es Salaam.

Saa tatu kasoro robo asubuhi, Princess Muro ilionekana kuzunguka Round About kuu ya Mji wa Biharamulo tayari kwa kuingia stendi kuu ya mabasi ya Biharamulo. Kama baada ya dakika tatu hivi, tayari lilisimama stendi na kuanza kupakia abiria wake wa Biharamulo. Zaidi ya Abiria watano walipanda hapa Biharamulo, katika Abiria hawa alionekana Binti mmoja mfupi wa wastani, mwenye weusi wa kuteleza, mnene aliyejaliwa kila mahali kwa mpangilio, Wataalamu hupenda kuyaita maumbo namba nane. Alivalia kijigauni kifupi cha rangi ya chocolate, na ndani yake akavalia skini laini nyeusi iliyofunika mpaka miguuni. Kichwani alikuwa amenyoa nywele ndogo sana pemberi halafu hapa juu akawa amesukia rasta mchanganyiko wa rangi ya kahawa na nyeusi, kisha akavalia miwani ya macho iliyokuwa na fremu ya kahawia na lensi ya gharama sana. Usingetumia nguvu kubwa kwa haraka kugundua kwamba Binti huyu anatoka kwenye familia inayojiweza kiuchumi. Basi Binti huyu alipanda moja kwa moja huku macho yake yakiangalia juu kwenye ubavu wa STAFF

CARRIER akijaribu kuangalia kama ataona mahali seat yake ya kukaa ilipo. Wakati anaangalia huku akizidi kwenda nyuma zaidi, Wakala wa mabasi wa Bihamulo akamuita “Irine nafasi yako hii hapa C2, unakwenda wapi huko nyuma?” Basi Binti huyu aitwaye Irine alirudi nyuma kidogo na kisha akakaa kwenye seat yake C2, alilalama akionekana kushangaa “Mudi, mbona nafasi yangu si ya dirishani jamanii na nilikuombapo?”. Yule Wakala aliyejulikana kwa jina moja la Mudi akamjibu, “Irine, nilikuambia nafasi za mbele unazotaka hakuna ya dirishani, zote zimeuzwa Bukoba.” Halafu akacheka kiaina akamwambia tena “Ila wewe mrembo bhana na ninamuona kijana amejilaza hapo dirishani, naamini kwa ulivyo mbona hufiki Kahama utakuwa umekaa dirishani.” Irine huku akicheka akamwambia “Kwenda huko”.

Hamidu aliyejekuwa amekaa dirishani kwenye seat C1 hakuwa hata anaelewa kinachoendelea, maana bado alikuwa amelala fo fo fo. Kwa mbali wakati Basi la Princess Muro likiwa linaitafuta Lusahunga, Hamidi alianza kuhisi kwamba hayuko peke yake kwenye zile seat mwenyewe kama alivyokuwa awali. Hakutaka kuamka kwa gafla, hivyo akaanza kusoma ramani ya kutaka kujua amekaa na nani huku akijidai bado amelala. Kwa kuwa alikuwa amevaa Tsheti nzito iliyokaa kama sweta na yenye kofia, na bado kichwani alikuwa na kofia yake ya FUBU aliyovalia kwa nyuma. Taratibu akiwa kajinamisha kwenye seat yake akiwa ameegemea mbele ya seat yake akafungua macho na gafla akakutana na umbo la kuvutia la mwanamke ambaye bado hakujua ni mdada mkubwa ama binti wa rika lake. Akatazama namna kile kigauni kilivyokuwa kimemkaa huyu mwanamke, na kwa Irine alikuwa amekaa, kile kigauni chake kilipanda juu zaidi

na hivyo Hamidu aliweza kuona sehemu ya mapaja kwa urahisi japo yalikuwa yamefunikwa na ile skini ambayo Irine alikuwa ameivaa kwa ndani.

Kikawaida Hamidu ni Mgonjwa sana kwa wanawake wenyewe maumbo makubwa ya aina hii, hivyo alijiona mwenye bahati sana na kichinichini alijiapisha ya kwamba hata kama awe mdada mkubwa kwake kiasi gani bado angetumia mbinu zote kutupia ndoano yake. Akajambia moyoni Dar mbali, labda awe anashukia Kahama hapo haitakuwa bahati yangu. Moja ya tabia ambazo Mzee Mhina alikuwa anazichukia na kuzikemea sana kwa Hamidu ni tabia za kupenda Starehe, Pombe, Vurugu na zaidi Wanawake. Kwa kipindi hiki cha likizo yake ya kuhitimu kidato cha sita yaani kuanzia February mpaka September, Hamidu alishakutwa na Baba yake kwenye nyumba yao wanayoishi watoto ya Kashai mara tano tofauti na akiwa na wasichana watano tofauti. Mzee Mhina ameshamtoa Hamidu polisi mara mbili kwa kesi za kupigana na kuleta vurugu CLUBS akigombaniana wanawake. Huyu ndiye Hamidu ambaye sasa yupo kwenye gari anaelekea Jijini Dar es Salaam.

“Habari yako kaka?” Irine alimuliza Hamidu baada tu ya kuinuka huku akijinyoosha kwa uchovu. “Oooooh! Fresh, Mambo zako? Hamidu alijibu huku akijipindua na kumtazama binti huyu mwenye sura ya kuvutia, na rangi halisi ya kiafrika, shombeshombe wa Kichaga na Kihaya. Baada ya kukutana na sura ya binti mdogo wa rika lake, Hamidu alichangamka zaidi na maombi yake makubwa ilikuwa na huyu binti awe anaenda Dar es Salaam au akipungua sana walau Dodoma.

“Samahani Kaka, mwenzio huwa nina matatizo, tafadhali naomba nikae seat ya dirishani jamani kama hutojali?” Irine alisema kwa sauti nyororo na ya kubembeleza. “WHY NOT! Huku akisimama kumpisha Irine akae dirishani. Wakati huo gari lilikuwa linapita Nyakanazi ile njia panda ya kueleke Kigoma.

# 4

## SAKINA, ARUSHA

“Hellow My Princess, how are you honey?”, Alisema Dr Mollel huku anacheka kwa Furaha. “Am good Dady, Miss you already!” Alijibu Lulu kwa sauti ya kudeka kidogo. “Sorry Sweet, it was very busy day, I’ have been through a lot”, Alikazia Dr Stephen Mollel. “Pole sana Dady wangu!” Alijibu Lulu. “Was your Uncle around at the Airport?” Aliuliza tena Dr Mollel kwa kujali, “Yes Dady” Alijibu Lulu.

Dr Stephen Mollel, Daktari Mbobe (Bingwa) wa Wanawake na Watoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru Jijini Arusha, ambaye pia miezi miwili iliyopita aliteuliwa kuwa Daktari Mkuu wa Hospitali hii ya Mount Meru. Dr Mollel alifunga pingu za Maisha na Bi Suzan Loishiye mwaka 1986 mara baada ya kuwa ndio kwanza ametoka nchini Urusi ambapo ndipo hasa aliposomea shahada yake ya Udaktari wa Binadamu kwa miaka saba. Pamoja na kuboea katika fani hii, Dr Stephen Mollel ambaye yeye kwa asili ni mtu wa jamii ya Wamasai wanaoishi Oldonyosambu ambao wao kwa asili ni wafugaji. Baba yake Dr Mollel alikuwa ni Mchungaji wa KKKT, na kwa hivyo haikuwa ngumu kwa Dr Mollel kupata elimu yake kwa mafanikio. Hata na hivyo Dr Mollel alikuwa moja ya watoto waliokuwa na akili za

kuzaliwa. Na kwa sababu ya uwezo wake huu mkubwa wa akili, kufaulu kwake ilikuwa jambo la kawaida sana tena kwa ufaulu wa juu mno.

Yeye na mkewe Bi Suzan mara baada ya kuoana walidhamiria kwa pamoja kupata watoto watatu tu. Lakini pamoja na Ubobeju wake kama Daktari bingwa wa mambo ya Wanawake na Watoto, bado alijikuta akishangaa sana ni kwa nini tangu walipooana mwaka 1986 mpaka 1990 mke wake Bi Suzan ambaye hakuwa na dalili zozote za utasa hakuwahi kushika mimba. Baada ya miaka minne bila mtoto, Dr Stephen Mollel na mkewe waliamua kumuomba Mungu na kwa bahati nzuri mwaka wa 1990 majira ya mwezi Mei Bi Suzan alishika ujauzito na tarehe 12/01/1991 alizaliwa mtoto wa kike waliyempa jina la Lulu. Waliamua kumuita Lulu kwa sababu alitafutwa kwa bidii ya muda mrefu, lakini pia walisema thamani yake ni kama yale mawe ya thamani ya Lulu. Na kutokana na mahangaiko aliyoypata Bi Suzan akiwa mjamzito na wakati anajifungua kwa upasuaji Wataalamu wenzake na Dr Mollel walishauriana na Dr Mollel ya kwamba mama huyu kwa usalama wake asizae tena. Na hii ndio sababu Lulu ni mtoto wa kwanza na wa mwisho kwa wazazi wake ambaao ni Dr Stephen Mollel na mkewe Bi Suzan.

Lulu Stephen Mollel, ambaye Baba yake alikuwa akimuita Princess (Binti Mfalme) tangu akiwa mdogo, Ni mtoto aliyelelewa na kujaliwa na wazazi wake kama mboni ya jicho. Kwa hiyo katika Maisha yake yote hakuwahi kuijua shida wala kupungukiwa kwa namna yoyote ile.

Hapa unaona Dr Stephen Mollel anampigia simu binti yake kumjulia hali, maana alichofanya ni kumkatia tiketi ya ndege ya asubuhi sana ya Shirika la Ndege la PRECISION AIR siku ile ile aliyo takiwa kuripoti chuoni. Na akawa amemuomba mdogo wake Saruni Mollel anayeishi Dar es Salaam aje ampokee na amsaidie kumpeleka chuoni. Japo kuwa haikuwa mara ya kwanza kwa Lulu kufika Dar es Salaam ila Dr Mollel hakutaka Lulu apate shida hata kidogo. Na kwa kuwa mdogo wake Saruni Mollel ni mfanyabiashara mwenye Maduka makubwa ya vipuri vyatya magari kwenye maeneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam haikumsumbuu kutii agizo la kakake la kumpokea Lulu airport na kisha kumpeleka Chuoni. Saruni anamheshimu sana kakake maana ndiye alichangia kwa asilimia kubwa sana yeche kufika hao alipo, kwa kumpa mtaji na kumuunganisha na watu wakubwa ndani na nje ya nchi. Lakini na anajua kakake kwamba huwa akisema jambo lake hataki kupigwa. Dr Mollel alimsisitiza mdogo wake Saruni kwamba ahakikishe anamfuata yeche mwenyewe Lulu na kumpeleka Chuoni, na asijaribu kumtuma mtu mwengine ye yote. Hii yote ni kwa sababu Dr Mollel hakutaka kabisa Lulu awe na mazoea na mtu ye yote.

“Dady, Ba Mdogo alinipeleka mpaka Chuoni. Na guess what? Nimefanikiwa kusajiliwa na nimepata Hostel nzuri ya ndani ya Campus.” Lulu alisema kwa sauti ya madeko kwa Baba yake. “That’s Awesome, hapo sawa kabisa!” Alijibu Dr Mollel. “Unaishi na kina nani hapo? Na how many are you in your room?” Aliuliza Dr Mollel. “Dady, I was the last one for today registration, so unfortunate in this room am alone right now.” Lulu alimjibu Baba yake.

Basi waliendelea kuongea kwa muda mrefu, na badae Bi Suzan nae aliongea na mtoto wake wa pekee na kumuasa mambo mawili matatu ya kuzingatia. Ukweli ni kwamba mpaka wakati ule Lulu alikuwa peke yake kwenye chumba cha Hostel alichokuwa amepewa, na sababu ni kwamba kwa siku ile usajili ulikuwa umeisha na ungeendelea siku inayofuatia. Hivyo kwa kesho yake angejua viruri watu ambao wamepangwa chumba alichokuwa amepewa yeye. Na kwa kuwa vyumba vya Hostel aliyokuwepo Lulu hukaa watu wanne kwa chumba. “Princess, your uncle is outside your hostel room please go with him.” Dr Mollel alimuandikia Lulu sms ambayo hakuitegemea. Kwa namna Lulu anavyomfahamu Baba yake alimjibu tu kirahisi “Oky Dady” bila kumbishia. Alichofanya ni kujiandaa haraka haraka na kwenda mahali alipopaki gari Babake Mdogo Mr Saruni. Baada ya kama dakika ishirini walifika Mbezi Beach mahali ambako Saruni alikuwa amejijengea jumba kubwa la Kifahari ambapo alikuwa akiishi na mkewe na watoto wake wawili ambao bado walikuwa wanasoma Primary level kwenye shule ya FEZA hapo hapo Jijini Dar es Salaam.

Tangu Lulu alipokuwa mdogo ilikuwa ni ndoto za Babake mzazi Dr Mollel ya kwamba Lulu aje kuwa Daktari kama yeye. Na alijaribu kumtengenezea mazingira ya kuupenda Udaktari kwa kila hali tangu alipokuwa mdogo. Hata wakati Lulu alipoanza Elimu yake ya Kindegateni na Primary katika shule ya St Patrick Trust kule Sakina, Baba yake daima aliwasisisitiza walimu wahakikishe lulu anapenda masomo ya Sayansi na Hisabati maana alitaka mwanae awe Daktari. Na kweli Lulu alifaalu masomo yote kwa alama za juu. Lulu alianza kujielewa anachopenda zaidi mara

baada ya kuanza Elimu yake ya Sekondari katika shule ya Sekondari ya Masista inayofanya viruri sana inayojulikana kama PRECIOUS BLOOD, shule iliyopo Kijiji cha POLI kule Meru kituo kinachofuata mara baada ya Tengeru kama kilomita tatu barabara kuu ya lami. Lulu alikuwa anafaulu masomo yote vizuri sana, ila alijikuta anapenda zaidi masomo ya Sanaa, na alijiona angependa kuwa Mwanasheria zaidi kuliko kuwa Daktari. Alijua sana kwamba jambo hili lingemhudhi sana Babake mzazi ambaye kila wakati alimsisitiza anataka Lulu aje kuwa Daktari bingwa wa Wanawake na Watoto kama alivyo yeye. Pamoja na yote hayo alidhamiria sana kwamba ni lazima aje kuwa mwanasheria.

Sister Geusepina moja ya walimu mashuhuri wa somo la Hiistoria na Kiiingereza, kuna siku alimuuta Lulu ofisini kwake na akamuuliza “Lulu, you are such the best student in all subject, who are you wanna be in the future?” Sister Gausepina alimuhoji Lulu. “Sister, thank you! My Dady dream since early days of childhood was for me to be Medical Doctor like him. But you know what? Serious I wanna be a Lawyer. I wanna stand for Justice.” Lulu alizungumza japo kwa huzuni na kutokujiamini. “My daughter Lulu, follow your heart. At first Dady won’t understand, but later He will appreciate. Good day! Sister Gausepina alijibu pamoja na kumuaga. Kiukweli yalikuwa maongezi mafupi lakini ukweli ni kwamba yalimpa nguvu Lulu mara kumi zaidi. Hii ilikuwa ni kuelekea Novembra ambapo Lulu alikuwa anajiandaa na mitihani yake ya muhula wa mwisho wa kidato cha Tatu. Lulu alipenda sana kuwa mwanasheria, na kila wakati akimkumbuka Baba yake anakata tamaa, lakini akikumbuka maneno ya Sister Gausepina

“At first Dady won’t understand, but later He will appreciate” alipata nguvu na kuamua kusonga mbele.

Kikawaida Dr Mollel ni mtu wa misimamo mikali, na huwa akiamua jambo lake hulisimamia mpaka ahakikishe linakuwa. Mkewe Bi Suzan na bintiye Lulu walikuwa wakielewa vizuri, na mara zote wamekuwa wakimsikiliza na kumtii sana. Bi Suzan pamoja na kuwa na Masters Degree ya Mambo ya Diplomasia na Mahusiano ya Kimataifa, na kufanya kazi kwenye Shirika la Umoja wa Mataifa. Bado alibaki kuwa Mwanamke wa Kimasai mwenye Unyenyekevu, Utii na Heshima kwa Mumewe katika mambo yote. Na ndiyo ilimfanya Dr Mollel kumpenda sana mke wake na kuamua kutoka moyoni kwamba hatamsaliti mwanamke huyu, na hivyo akaridhika na mtoto wao mmoja wa kike na wa pekee.

Siku moja wakati wa likizo ya mwezi wa kumi na mbili, wakati ambako Lulu ndio alikuwa anajiandaa kuingia kidato cha Nne mwaka unaofuata, alasiri kama ya saa 10 jioni hivi Mama yake alimwambia Lulu ajiandae ili waende Supermarket ya SHOPRITE kwa ajili ya kununua mahitaji ya nyumbani. Wakati wanatoka nyumbani kwao maeneo ya RASKAZONE Sakina wakiambaa na barabara kuu ya Namanga-Arusha, kabla hawajafika maeneo ya SILENT INN Lulu alimuuta mama yake kwa sauti ya upole sana “Mom”, “Princess” Mama yake alimjibu huku akiwa ameshika usukani kwa umakini sana wa gari yake mpya aina ya Rava 4. “I see myself I disappoint Dad” Lulu alisema kwa huzuni. “What?!!” Mama yake aliuliza, wakati huu Mama alikuwa anakata kulia kuachana na barabara ya kuelekea Mianzini, huku akifuata barabara ya Arusha Technical huku

akinyoosha moja kwa moja mpaka KONA NAIROBI. “Mom, promice if you will be in my side!” Lulu aliendelea kusema kwa huzuni. Bi Suzan Mama yake na Lulu ni mtu mtulivu sana, na ndio maana mpaka leo amebaki kwenye orodha ya Wanadiplomasia mashuhuri kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. Hivyo alivyoona Mtoto wake anaonyesha dalili kama ana jambo zito aliamua kumpa muda tulivu, hivyo wakati amekata kushoto baada ya kufika KONA NAIROBI kuelekea kilombero ilipo Supermarket kubwa ya SHOPRITE watati huo, akamwambia mwanaae “Princess My Doughter, Hold on!!”, akitaka atulie kidogo ili wafike Supermarket wapate nafasi ya kuzungumza vizuri.

# 5

## MTOTO WA NYOKA NI NYOKA!!

„ Yaani yule mtoto amefanya maajabu eti! ”, Alisikika mama mmoja wa Kinyiramba. “ Nilisema tu, yaani huyu mtoto atakuja kumuokoa mama yake eti! ” Mwenzake mwingine aliongezea. “ Bora uwe na mtoto mmoja kama huyu kuliko kuwa na watoto wengi ambao ni hasara tupu! ” Mwenzao wa mwisho alizungumza kwa uchungu. Hawa walikuwa ni Wamama watatu wa Kijiji cha Kinyambuli, ambao walikuwa wanatoka ofisi za Kijiji kuangalia Matokeo ya Darasa la Saba mwaka 2001 ya Mtihani wa Taifa.

Mashauri Jonathan Mkumbo alikuwa ni mwanafunzi pekee aliyefaulu kuendelea na Elimu ya Sekondari katika Kata yote ya Ntiko. Mamia ya Wanafunzi toka vijiji vya Kinyambuli, Malaja, Mazangili na Muti walikuwa wamefeli mtihani ule. Na kwa mara ya kwanza ndani ya miaka minne hatimaye Kata ya Nkito inatoa mwanafunzi kwenda shule ya vipaji yaani Masengo Technical School iliyopo Dodoma. Katika jumla ya alama 150, Mashauri Jonathan Mkumbo alipata alama 140. Hii ndio ilimfanya kuchaguliwa kuendelea na Elimu ya Sekondari tena kwenye shule ya maana.

Bi Wankembeta, Mama yake na Mashauri ambaye ungemuangalia kwa haraka haraka kama humjui ungedhania ni Bibi yake. Na hii kwa sababu alimzaa Mashauri akiwa na umri wa miaka 44, na wakati ambaao Mashauri anamaliza darasa la Saba, tayari Mama huyu alikuwa na miaka 57. “Songela Nzuwa Wane Wituma”, alisikika Bi Wankembeta akimshukuru Mungu kwa lugha ya Kinyiramba. Lumba mdogo wake na Bi Wankembeta akasema kwa Furaha sana “Kweli KUCHELEWA SI KUKATALIWA”. Kwa kweli Matokeo haya ya Mashauri yaliwu ni habari kwenye Kata ya Nkita kwa wiki nzima tangu matokeo haya yatoke.

Mzee mmoja aliyeonekana umri umeenda sana huku akiwa ameleta chakari pombe za kienyeji, alipopita nje ya nyumba ya Bi Wankembeta na kumuona vile wanavyomshukuru Mungu kwa Furaha, ikabidi aulize kwa sauti ya kilevi “KULIKONIII” Baada ya Lumba kumuambia kilichotokea, Mzee akapiga makofii akasema “Sasa la kushangaza hapo ni lipiiiiii jamani??”, Akaendelea kusema “Nyie mbona washamba hivi jamani, nyie vipi alaaa. Hamjui kwamba “MTOTO WA NYOKA NI NYOKA!” Ahahaha hahaha hawa vipi hawa!!!!!!” Alimalizia kucheka kwa dharau kisha akaondoka zake. Wakati huyu Mzee akiongea nje, Mashauri alikuwa ndani na kwa hivyo alimsikiliza viruzi sana. Kilichomshangaza Mashauri licha ya kujua Mzee alikuwa akiongea yale maneno huku ameleta sana, Moja ni kwanini hakushangazwa juu ya kufaulu kwake, na Mbili ni ile kauli yake ya mwisho kwamba “MTOTO WA NYOKA NI NYOKA”. Baada ya yule Mzee kuondoka, Mahauri alitoka nje na kujaribu kumuuliza Mama yake Mzazi na Mamake mdogo

kwamba yule Mzee alikuwa akimaanisha nini? Wao wakamjibu kwa wepesi sana “Achana na Mzee Mataatu Mlevi huyo” Mamake mdogo alisema “Mwanangu Masha, uje mtu akizeeka sana anarudia utoto. Hapo haelewi hata anaongea nini”. Mama yake Mashauri alisisitiza kwa kawaida, Mashauri sio mtu anayependa ubishi sana, ila ni mtu wa kuchukua hatua. Hivyo aliamua kuwaelewa na akaacha kuendelea kuwaliza.

Siku iliyofuata asubuhi ya saa nne Mashauri akiwa na kibuyu alichikijaza Togwa alionekaza akienda nyumbani kwa Mzee Matata aliyekuwa akiishi na wajukuu zake watatu. Alipofika alimuulizia akaambiwa yupo ndani ila kachoka sana maana jana alilewa sana. “Nani huyo ananiulizia saa hizi??” Mzee Matata alibwatuka kutokea ndani. “Wewe Mzee kweli ni Matata si ulikuwa umelala wewe??” Mjukuu wake mmoja alitania. “Unatakiwa ulale kiume kiasi kwamba jina lako likitamkwa tu unaamka chaap!!” Mzee Matata alijibu kwa mkwara sana. Baada ya majibizano mawili matatu na mjukuu wake, Mzee Matata akamkaribisha Mashauri ndani. Alivyomuona tu kwamba Mgeni mwenyewe ni Mashauri akasema tu kwa sauti “Mtoto wa Nyoka ni Nyoka, Mimi nilijua tu utafaulu!”. Mashauri aligundua yupo eneo sahihi na maswali yake yatajibiwa yote tena kwa undani. Baada ya salamu, akachukua kibuyu akamwambia “Babu nimekuletea Togwa kidogo ya kunywa”. Mzee Matata ile kuipokea tu bila kusubiri akainywa kwa haraka haraka bila kuishusha mpaka nusu ya kibuyu. Kisha Mashauri akamwambia “Babu nina swalii? Kwanini unasema ulijua tu nitafaulu, na unasema Mtoto wa Nyoka ni Nyoka? Mzee Matata aliposikia lile swalii kwanza akashusha pumzzi na akaanza kumhadithia kijana.

“Jonathan Mkumbo ambaye ndiye Baba yako Mzazi alikuwa ni mtu mwenye akili sana kiasi cha kuogopwa na Wakoloni. Alipofanya mitihani ya Darasa la Nne wakati ule, alikuwa ni mionganoni mwa wanafunzi wachache Tanganyika yote waliofaulu na kutakiwa kuendelea na masomo. Ila kwa sababu za fitina za Wakoloni jina lake lilitatiliwa mbali. Hivyo ikabidi Jonathani arudi kijijini na kuendelea na kazi zake za kilimo na ufugaji. Laiti kama Baba yako Mzazi angelisoma, leo hii angekuwa mtu mkubwa sana na wala hata pengine asingekuwa amechukuliwa na umauti. Wazungu washenzi kabisa wale, walijua Jonathani angeendelea kusoma angewazidi uwezo na ndio maana walifanya hila asiendelee. Mimi pia nilikuwa sio mchezo japo Baba yako na wewe ni kama Baba yako kabisa, yaani nilivyosikia unaongoza wenzako tena kwa mbali sana tangu darasa la kwanza nilijua tu kwamba ni lazima ungefauku tena ungeenda mbali. Daah!! Jonathani!!! Jonathani!!! ulikuwa Rafiki yangu sana, pumnzika kwa Amani Mwamba”. Mzee Matata alitamka huku akitokwa na machozi. Na kisha akatema mate mkononi mwake, akampaka Mashauri kichwani kama ishara ya kumbariki. Na kisha akasema “Siku hiyo Babako alipitia hapa twende tukakate miti tayari kwa kazi yetu ya kuchoma mkaa, Mimi nilikuwa kama najisikia homa hivi nikamuomba tuhairishe kwa siku ile. Yeye akaniambia ‘Matata Wewe ni ndugu yangu, pumnzika ila mimi acha nikapambane’ Na hivyo, siku hiyo akaondoka akaenda mwenyewe porini kukata miti. Majira kama ya saa 10 alasiri hivi naletewa taarifa Jonathani amekutwa porini ameangukiwa na mti na amekufa. Kiukweli ilinuma sana hasa ukiangalia wakati huo ndio kwanza Mama yako alikuwa ni mjamzito wa mwezi mmoja tu. Na hivyo Baba yako alikuwa bila

kukuona mtoto wake wa pekee. Soma mwanangu umuokoe mama yako, utuokoe Kinyambuli na uiokoe Tanzania”. Alisisitiza Mzee Matata huku akinyanya tena Kibuyu na kumalizia ile nusu ya Togwa kwenye Kibuyu ambayo ungedhani ameisahau.

# 6

## ZALI NA SHIBE

**B**aada ya Mashauri kumaliza kula ile biskuti na maji aliyokuwa amepewa na yule binti yaani Lulu, alienda mahali na kulan a kunywa kwa haraka haraka. Alipomaliza alirudi na kumshukuru tena Lulu, na kisha akaendelea kutulia kwenye foleni. Kwa asili Lulu ni muongeaji sana halikadhalika na Mashauri pia, kwa hivyo pamoja na kuwa karibu kwa muda mrefu kwenye ile foleni walikaa kimya kwa muda mrefu sana. “Hongera Mashauri, unaonekana una akili Sana zisizo za kawaida!” Lulu alivunja ukimya, “Eeeh umejuaje jina langu?!!! Ahsante ila kwa nini!!” Mashauri alijibu kwa kuhamaki. “Jamani umesahau uliniachia vyeti vyako, macho hayana pazia japo samahani” Lulu alisema, wakati huo aliweka madeko kidogo kama kawaida yake. “Oooh!! Kwa hiyo uliangalia eti!! Usijali ni kweli naitwa Mashauri Jonathan Mkumbo.” Mashauri alisema. “Aisee, yaani Division 1.7 O level na Division 1.4 Advance halafu PCM mmmh nimesema nikupongeze tu jamani!” Lulu alikazia. “Ahsante Dadangu, utukufu kwa Mungu.” Mashauri alijibu.

Vijana wa mjini walikuwa wakiwafuatilia Lulu na Mashauri na kushangaa mbona kama wamezoeana kwa gafla vile. “Na mimi naitwa Lulu Stephen Mollel, natokea Arusha. Na

nimedahiliwa hapa kuchukua masomo ya Sheria.” Lulu alimalizia kujitambulisha. “Oooh, Umesema Lulu eeeh. Hongera pia mwanasheria!” Mashauri alijibu kisha kwa aibu akaongezea “Mimi nasomea Uhandisi wa Umeme hapa!” “Eeh jamani kumbe tunaingia wote na tutatoka wote what a lucky?!!” Lulu alioneckana kushangaa na kufurahia. “Kivipi?!!” Mashauri aliuliza kwa mkato na mshangao. “Mimi nafanya Shahada ya Sheria kwa miaka minne, na huwa najua Engineering yoyote huwa ni miaka minne, ndio maana nikasema kumbe tunaingia wote na kutoka wote” Lulu alitoa maelezo ya kutosha. “Aaah kwa Neema ya Mungu itakuwa hivyo, maana nasikia kuna kurudia mwaka ukifeli.” Mashauri alisema. “Hamna bhana, tutamaliza wote wa kurudia mwaka sio mimi wala wewe kwa akili hizo” Lulu alitia msisitizo. “Amina.” Mashauri alijibu.

Wakati huu foleni ilikuwa imesonga sana na ilibaki watu kama watano tu zoezi liishe kwa siku hii. Baada kama ya dakika 20 wote walikuwa wameshasajiliwa, na walikuwa wameenda eneo la mwisho ili kupangiwa mahali pa kulala yaani Hosteli. Kikawaida Wanafunzi wengi wanaoanza mwaka wa kwanza na wanaowahi hupangiwa kuishi ndani ya Chuo, wale waliochelewa wakakuta pamejaa pamoja pamoja na wale ambao sio mwaka wa kwanza ndio huishi MABIBO HOSTEL na Hosteli nyingine za nje. Kwa bahati nzuri Mashauri na Lulu wote walipangiwa Hosteli za ndani ya Chuo. Baada ya kumaliza eneo la mwisho la kupangiwa nyumba ilibidi watawanyike, lakini kabla hawajatawanyika Lulu alisema hiki “Mashauri, naomba kama hutojali tukutane baada ya nusu saa pale tuliposajiliwa twende tukale. Si unajua wewe ndio kampani yangu kaka!” Mashauri

kikawaida huwa hapendi na hajawahi kuwa na mazoea na wasichana, kwa hiyo alitaka akatae ila alipokumbuka kwamba hana hata mia mfukoni aliona hatapata muujiza mkuu kama huu kwa leo, hivyo kwa ustarabu wa hali ya juu akajibu “Sawa Dada Lulu!”

Saa 12 unusu jioni wakati mwanga wa mchana unazidi kufifia na kagiza kanaanza kuingia, kwenye moja kati ya Cafeteria za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walionekana vijana wawili wakike na wakiume wasioendana kabisa kimuonekano. Huyu wa kike alionekana wa Kishua sana na mrembo kupitiliza, na huyu wa kiume alionekama MSHAMBA kupitiliza kuanzia mavazi mpaka muonekano. Kwa namna walivyokaa inaonekana kama walifahamiana kwa muda mrefu sana, kila aliyeingia kwenye ile Cafeteria pamoja na walikaa mle ndani walikuwa wanawaangalia sana wale vijana. Moja, ni kwa sababu ya uzuri wa yule dada usioelezeka, na Mbili na muonekano wa kishamba wa yule kaka wa kushangaza. Lakini Tatu ambaao ni ajabu zaidi ni inawezekana wale watu wasioendana vile wakakaa pamoja. “Mashauri, kula chochote unachotaka Mhandisi, Dadako nitalipia!” Alisema Lulu kwa utani kidogo. “Sawa Mwanasheria” Mashauri alijibu. Unajua Lulu mwenyewe alishangaa ni kwa nini leo amekuwa na ujasiri na ukaribu na huyu mvulana kiasi hiki, kuna muda aliquwa anaongea mpaka anajishtukia. Mwisho wa siku akajiambia huyu kaka ni mtu mwema na anafaa kuwa Rafiki, lakini pia kwa namna alivyamuona aliamini Mashauri anahitaji msaada wake.

“Mashauri, hivi wewe unatokea wapi kwa asili?!!” Lulu aliuliza. “Mimi natokea Singida-Iramba kijijini huko!” Mashauri alijibu wakati akibugia pande la kuku na ugali. “Oooh!! Kwa hiyo

wewe ni Mnyiramba au Mnyaturu?!” Lulu aliliza. “Lulu hilo neno Iramba linaonyesha mimi ni Mnyiramba!” Mashauri alijibu. “Na je una kaka na dada wangapi?” Lulu alidadisi. “Sina kaka wala dada, wala Baba, Mie nimezaliwa kwetu mwenyewe!” Mashauri alijibu. “Eeh! Makubwa jamani, Masha mbona tunafanana vitu vingi hivyo!” Lulu alihamaki. “Kivipi?!” Mashauri aliuliza. “Hata mimi sina kaka wala dada, ni mtoto wa kipekee kwa mama yangu na baba yangu.” Lulu alikazia. Halafu akaongezea “Jamani, kweli hatujakutana kwa bahati mbaya!”. “Biblia inasema, kila jambo hutokea kwa kusudi chini ya juu!” Mashauri alionekana kushiba sasa alitamka kwa ujasiri. “Amina!” Lulu alijikuta kasema kwa sauti mpaka akajishtukia. “Dada, unaabudu wapi?” Mashaujri aliuliza huku akimtazama Lulu machoni na wakati huo akinyanya glasi ya juisi ya Rozella tayari kwa kunywa. “Mimi Mlutherani, Wewe je?! Halafu wewe lazima utakuwa mlokole tu kwa maandiko hayo!!” Lulu aliuliza na kujibu. “Aaahaha Mimi pia ni Mlutherani japo pia ni kweli kwamba nimeokoka tena tangu O level. Lulu, Ulokole sio dini wa dhehebu.” Mashauri alijibu na sasa sauti ilibadilika kama mtu anayetaka kuhubiri, si unajua wapendwa tena ukimleta kwenye uwanja wake. Lulu alipoangalia saa yake aliona muda umeenda sana, pamoja na lile joto kali la Dar hakuwa ameoga baada ya michosho mingi ya mchana Lulu aliamua kukatiza mada, akanyanyaaka akaenda kulipa kisha akamrudia Mashauri aliyekuwa amemaliza kula pia. Kisha wote kwa pamoja wakatoka nje, ki ukweli kila mtu alikuwa anawashangaa. “Mashauri, naomba niwe nakuita Masha au Mhandisi na muda mwagine Mtumishi ahahahahaha!” Lulu aliongea kwa utani huku akicheka. “Sawa tu, Dadangu Lulu!” Mashauri alionyesha kukubaliana. Unajua hata kule kwao Singida

nyumbani Mama yake daima humuita “Masha”. “Hivi una simu Masha!?” Lulu aliuliza. “Hapana Dadangu!” Mashauri alijibu. “Oooh! Usijali, Utapata tu!” Lulu alionyesha kusikitika huku akimtia moyo. “Sasa naomba tufanye hivi, chukua hii ikusaidie na nitakuandikia namba zangu halafu kesho utanitafuta ili tuendelee na maongezi, sawa Mtumishi!” Lulu aliongea huku akimpa shilingi elfu tano Mashauri, na baadae akatoa kalamu na karatasi na kumuandikia namba zake. Na baada ya hapo kila mmoja akatawanyika.

# 7

## ONE DAY GAME

“ Naitwa Hamidu!” Hamidu alijitambulisha, “Am Irine!” Irine alijibu. “Sorry, unaenda mpaka wapi mrembo!?” Hamidu aliuliza. “Narudi Dar es Salaam” Irine alijibu. “Oooh inamaana wewe unaishi Dar sio?! Maana umesema unarudi” Hamidu alisema. “Hapana kwetu ni Biharamulo, ila mimi nimesoma Dar es Salaam tangu form one mpaka form six, so muda mwingi nimekuwa Dar.” Irine alizungumza kwa sauti nyororo huku akijiweka vizuri kwenye siti yake. “Eeh kwa hiyo ulimaliza form six mwaka huu sio!?” Hamidu aliuliza. “Ndio, nimemaliza Jangwani na kwa sasa nakwenda chuoni Mlimani!” Irine alijibu. Ni kawaida kwa Wanawake kutoa details nyingi wanapouliwa jambo, na hivyo kwa muda mfupi Hamidi alijua mengi kumuhusu Irine. Jambo la kwanza alifurahia kwamba atasafiri na mtoto mzuri kama yule mpaka Dar es Salaam hivyo ana kampani ya kutosha tena ya maana itakayomfanya aone ile safari ni fupi sana, hapa wanaume watanielewa vizuri. Lakini mbili, Chuo anachoenda kusoma ye ye ndio ambacho huyu msichana pia anaenda kusoma. Kwake hii ilikuwa ni upenyo mrahisi mno wa kumpata huyu msichana na kumbuka Hamidu ni mtu wa wasichana na sio mmoja wala wawili.

“Can I surprise you Beauty??!” Hamidu aliongea ung’eng’e kwa bashasha sana, si unajua tena vijana waliokulia Kijijini. “Sure”, Irine alijibu kwa utulivu sana. “Mie pia nimemaliza form six Jitegemee High School, na hapa nipo njiani kuelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam!” Aliongea Hamidu huku akijisogeza zaidi kwa Irine. “Oooh! My God!!” Irine aliongea kwa mshangao, kisha akaongeza “Yani niliwaza leo nitakaa na nani kwenye gari na lisafari lilivyo lirefu hivi, unfortunate nimekutana na mtu wa maana sana jamani.”

Mara ikasikika sauti ya Kondakta wa gari kwenye spika za ndani ya gari, “Wapendwa Abiria wetu wa Princess Muro sasa tunaingia Kahama tafadhali wanaoshukia Kahama sofea mbele hatutaigia stendi. Na Abiria tunaoendelea na safari tutaingia Hotelini kuchimba dawa pamoja na chakula cha mchana kwa dakika kumi, zingatia muda!” Baada ya dakika tano gari lilikuwa limebaki hotelini, bila kupoteza muda Hamidi alipitisha mkono nyuma ya kiuno cha Irine na kumsaidia kufungua mkanda wake wa siti. Na kisha akajifungua na wake, “Thanks Dear, yaani sipendagi mikanda basi tu!” Irine alisema kwa sauti ya kudeka. “Karibu Mrembo!” Hamidu alijibu huku akiinuka tayari kwa kushuka.

Unajua Irine alikuwa hajamuona vizuri Hamidi tangu amepanda gari pale Biharamulo Stendi. Hapa sasa wakati anasimama ndio alimuona vizuri. Hamidu ni kijana mrefu wa wastani, amejazia vizuri sana kifua na mikono, lakini pia ana weupe kwa mbali aliouchukua kwa mama yake Bi Husna. Na ana uso mzuri wa kiume, halafu sasa anajua kuvalaa yaani ile haswa, Irine alijiona na bahati ilioje kukutana na kijana mtanashati kiasi

kile tena anayejali sana. Kumbuka alimuachia siti ya dirishani, na bado wakati wa kushuka amemfungulia mkanda. Baada ya Hamidi kusimama akawa kama amewazuia abiria wengine wa nyuma yao waliokuwa wameanza kushuka kisha akamwambia Irine “Lets Go!”. Irine aliyekuwa amesimama huku akirekebisha kigauni chake kifupi kilichokuwa kimepanda juu zaidi, akasogea akapita mbele ya Hamidi na kuanza kushuka. Unajua Hamidu alichanganyikiwa maradufu, akawa anameza mate mfululizo kwa namna binti alivyoumbika. Halafu Irine anajua kulitendea haki umbo lake namba nane wakati anatembea, Hamidu alijiapiza kwamba ile siku isingepita bila kumfaidi huyu mrembo. Walivyoshuka tu kila mmoja akawahi msalani, baada ya hapo wakakutana tena na hapa Hamidu akaamua kujionyesha kwamba ye ye ni kidume kwelikweli. “Irine Mum, take anything and everything I will pay!” Hamidu aliongea kwa kuji amini sana.

Kama ungekuwa haujaanza safari na hili basi tangu Bukoba au haujapandia Biharamulo ungeweza kudhania kwamba hawa vijana wametoka mahali pamoja na wanafahamiana kwa muda mrefu sana. Na usingetumia nguvu kubwa pia kujua kwamba niwapenzi, maana walionyesha ukaribu na ishara za wapenzi.

Ilipofika saa moja jioni gari la Princess Muro ndio lilikuwa linaingia Stendi kuu ya mabasi Singida mjini. Kwenye seat namba C1 na C2 walionekana vijana wawili wa umri wa miaka 20 na wakiwa wamelaliana na usingizi ulikuwa umewapitia kabisa. “Hoya hoyo wee Dada mafuta mafuta mazuri kabisa bei nafuu!” Aliongea mfanyakibashara kijana aliyekuwa anauza mafuta ya Alizeti huku akigongagonga kioo. Hiki ndicho kilimuamsha

Hamidu aliye kuwa amemzungushia mikono yake Irine aliye kuwa amelala fofofo, “Oyaa acha kusumbua, sitaki mafuta!” Alijibu kikorofi Hamidu kama kawa ida yake. “Broo sijakuita wewe lakini mbona unanizibia riziki??!” Alijibu muuza mafuta kwa sauti ya malalamiko na hasira. “Tokaa ndio nimekwamba sasa hataki mafuta”. Hamidu alijibu kwa hasira zaidi. Yule kijana wa mafuta akaondoka.

“Hamy, tumefika wapi?!” Irine aliuliza kwa sauti ya kike ile ya usingizini iliyoamsha mno hisia za Hamidu na ukichukulia kwamba alikuwa amelaliwa. “Lala Baby usijali, ndio kwanza Singida!” Hamidu alijibu huku akimshikashika taratibu sana Irine nywele zake kichwani. Irine alijiona yuko mikono salama kabisa. Saa tano za usiku Princess Muro ilikuwa inaingia stendi kuu ya Jamatini Dodoma. Kiukweli kila mtu ndani ya gari alikuwa amechoka sana maana gari lote lilikuwa kimya sana. “Wanaoshuka Dodoma sogea mbele tafadhali! Dodoma sogea mbele, dereva washa taa!” Alitangaza kondakta kwa kipaza sauti kilichokuwa ndani ya gari, safari kesho inaanza saa 11 asubuhi, ukichelewa unaachwa!!” hapa sasa gari lote lilikuwa macho na kila mtu alisikia tangazo.

“Irine!” Hamidu aliita, “Abee!” Irine aliitika kichovu. “Nisubiri hapa nashuka chaap nakuja!” Hamidu aliaga. “Aiyaa!” Irine alikubaliana. Hamidu alishuka chini na akaenda moja kwa moja kwa yule kondakta ambae wakati huo alikuwa anawashushia watu wanaoshukia Dodoma mizigo yao ya kwenye buti. “Niambie kijana wa Mzee Mbabe?!” Kondakta alimuongelesha Hamidu. “Umekula!?” Hamidu aliuliza kwa mkwara. “Hapana Tajiri yangu niambie!” Kondakta akajibu akitegemea jambo. Hamidu akaingia

mfukoni akatoa waleti, kisha akachomoa noti moja ya Elfu kumi akampa Kondakta. “Oya hii kale, si umeona kile kipisi niko nacho pale!?” Mimi naenda kulala Lodge kufurahia Maisha, Asubuhi nishtue mwanangu. Namba zangu hope unazo!” Aliongea Hamidu huku anarudi kwenye gari.

“Mrembo wangu, tukilala hapa tutachoka sana. Twende zetu Lodge tukajinyooshe vizuri aisee. Konda nimeshamalizana nae, atatuamsha asubuhi!” Hamidu aliongea kwa majidai na uhakika zaidi. “Sawa tu, maana nimechoka mno!” Alijibu Irine bila kujali sana, Hamidu alifurahia ushindi ule wa ajabu, hizi huwa anaziita ONE DAY GAME yaani unakutana na msichana siku moja na kulala nae siku hiyo hiyo. Alijiona mtu mwenye bahati sana. Ndani ya dakika 10 tax ilikuwa imepaki nje ya Lodge ya gorofa ya CANA LODGE, kisha Hamidu na Irine wakaingia. Hamidu akalipia Exessive Room ya Elfu 60 yenye kila kitu ndani mpaka fridge, baada ya hapo vijana wakaoga pamoja na kufurahia ujana wao. Japo ndio walikuwa wamekutana tu kila mmoja alijiona mwenye bahati kukutana na mwenzake.

# 8

## TOM BOY!!

**M**anka Sifueli Mrema, Binti wa Mwalimu Mrema ambaye wanafunzi wote waliosoma Shule ya Msingi Kiwalaa iliyopo Kata ya Mbokomu Moshi Vijijini, wanamfahamu vizuri sana Baba yake aliyekuwa mwalimu mkuu pale kuanzia mwaka 1987 hadi 2007. Kwa hiyo wakati Manka anazaliwa 1990 na anaanza kukua, kusoma chekechea mpaka anakaribia kumaliza kidato cha sita Babake bado alikuwa Mwalimu mkuu kwenye shule hii.

Manka tangu anakua, marafiki na watu wake wa karibu walikuwa wavulana. Hata na hivyo muonekano wake kila mtu kwa haraka angeweza kujua kuwa yeye ni mvulana. Tembea yake na namna anavyojojiweka weka kila wakati ilikuwa imekaa kivilana zaidi. Wakati amefika darasa la tano, alikuwa anajulikana kama Jike-Dume, japokuwa wengi walishindwa kumuuta hivyo moja kwa moja kwa sababu ya kuhofia kipigo cha Babake Mwalimu Mrema ambaye ni Mwalimu mkuu wa Shule hiyo. Mwalimu Mrema alimpenda sana binti yake maana tangu utoto wake sio mtu wa mambo mengi, na alikuwa ana akili sana za darasani.

Mwalimu Sifaeli Mrema pamoja na ukali wake aliokuwa nao, na fimbo zake ambazo wanafunzi walikuwa wanasema ni heri uchawe na mwalimu mwininge fimbo tano kuliko fimbo yake moja. Bado alipendwa sana na Wanafunzi wote kwa sababu ya uwezo wake wa kufanya somo la Hisabati kuwa rahisi kwa namna anavyofundisha. Lakini pia ni mwalimu aliyesimamia haki na maslahi ya wanafunzi. Historia inaonyesha ndiye mwalimu aliyeanzisha utaratibu wa wanafunzi kula chakula cha mchana shuleni, tena chakula kizuri. Na daima alichowaambia walimu wenzake na bodi ya shule ya kwamba kwake kipaumbele ni Wanafunzi na ufaulu na huwa alikuwa na msemo wake wa “HAWAWEZI KULIMA MAHINDI NA MAHARAGE, NA WASIYALE” hiyo kwake aliita dhambi.

Manka alipomaliza mitihani yake ya darasa la saba alifaulu na kupangiwa Shule ya Sekondari ya wasichana Ashira. Tofauti na wanafunzi wengine wanaofurahia kwenda shule za wasichana peke yake, Manka alihuzunika sana. Daima rafiki zake ni wavulana, na anajisikia faraja sana anaposoma na wavulana, na hao ndio washindani wake. Kwa kuwa Mwalimu Mrema alikuwa mjumbe wa bodi ya shule ya Kanisa iliyokuwa inafanya vizuri sana wakati ule yaani Natiro Sekondari, ilimbidi afanye maamuzi magumu ya kumpeleka Manka shule hiyo ya Private, na kuacha kwenda shule ya sekondari ya Wasichana Ashira alikopangiwaa baada ya kufaulu vizuri sana. Baada ya Baba yake kumjulisha kwamba ataenda Natiro Sekondari, Manka alishangilia sana mpaka Mama yake alimshangaa sana. Unajua kama haujui jiografia ya eneo hili unawenza usielewe kwa nini Mama alimshangaa, unajua kutoka Fukeni Kijiji wanachoishi ambacho

ni juu kidogo ya Kiwalaa, kutoka Fukeni kwenda Natiro ni mwendo wa nusu saa kwa mguu. Alichokifanya Baba yake ni kuhakikisha anampeleka kuishi Bweni ili pamoja na kupata kampani ya wavulana anayotaka, lakini pia apate pia mwingiliano na wasichana wenzake anapokuwa Bwenini maana hii asingeweza kuiepuka.

Godbless Mrema na Ben Phares hawa ndio walikuwa marafiki wakubwa wa Manka pale Natiro Sekondari, na wote kwa pamoja walikuwa wazuri sana darasani hasa kwa masomo ya sayansi. Walipomaliza kidato cha Nne, wote watatu walifaulu vizuri na hawa wawili yaani Ben na Godbless walipangiwa Same Sekondari, shule ya wavulana tu, na Manka alipangiwa Loleza shule ya wasichana tu. Na wakati marafiki zake walienda kusoma mchepuo wa PCB (Physics, Chemistry, Biology), Manka alienda kusoma PCM (Physics, Chemistry, Mathematics). Wakati huu Manka hakuona shida sana kwenda kusoma shule ya wasichana tu peke yao maana walau aliona wepesi baada ya mwingiliano alioupara na wasichana wenzake kwa miaka mnne.

Unajua Manka licha ya tabia nydingi za kiume alizonazo, alipopevuka alipata maumbile ya kike ya kuvutia, kwanza alikuwa na kifua kidogo kizuri, hakuwa mnene wala mwembamba na alikuwa na vihipsi vyta kichokozi na alijazia huku nyuma kimtindo. Kwa ufupi alikuwa Jike-Dume mwenye muonekano mzuri, sema kwa namna alivyokuwa anavaa na kutembea usingeweza kugundua kirahisi.

Alipofika Loleza ile shule ya Wasichana iliyopo Mbeya tayari kwa masomo yake ya PCM, alikutana na Gwantwa

msichana wa Kinyiramba kutoka kule Tukuyu. Walishibana sana kwa sababu licha ya uzuri aliokuwa nao Gwantwa hakuwa mtu wa mambo mengi, lakini pia walikuwa wanasoma wote PCM. Na Zaidi wote walikuwa wanasali kikundi kimoja cha dini cha UKWATA maana Manka kanisa lake ni KKKT na Gwantwa ni Moroviani. Hivyo walijiona wanabahati sana maana kila mahali walikuwa pamoja kama mapacha, mabinti hawa ambaeo walikuwa hawana mambo mengi, Moja ya vitu ambavyo Manka alikuwa amejaliwa na anapenda ni kuimba, mpaka leo ukienda Natiro utakutana na vikombe ambavyo Natiro Sekondari walishinda kwenye mashindano ya Uimbaji kwa sababu ya umahiri wa Manka na Gwantwa, moja ya alama ambayo Manka na Gwantwa waliacha Loleza mpaka leo kwa UKWATA na vikundi vyaya dini ni kuanzisha kwao kwa Matamasha ya Uimbaji ya Vikundi vyote vyaya dini yaliyokuwa yanaitwa LETS SING TOGETHER CONCERT. Na hii ndio ilikuwa njia pekee ya kuleta Wakristo pamoja pale shulenii kwa maana ya Ibada.

Walimu wengi waliwasapoti kwenye mambo yao maana kwa kweli walikuwa mabinti wa tofauti pale Loleza. Pamoja na kufanya vizuri sana darasani, walikuwa viongozi wa shule ambapo Gwantwa alikuwa Head Girl na Manka alikuwa General Secretary, na kwa UKWATA Gwanta alikuwa Mwenyekiti na Manka alikuwa Katibu wake. Unajua kwa asili Manka sio muongeaje sana, yeye ni mzuri kwenye kutenda na kusimamia. Gwantwa kwa asili ni muongeaji sana na ana nguvu kubwa ya kushawishi na kuhamasisha. Siku ya Mahafali ya kidato cha Sita ya kuagwa darasa la kina Gwantwa na Manka wanafunzi na

walimu walilia sana, kila mmoja alikiri kwamba hawatapata viongozi na wanafunzi kama hawa.

Matokeo ya Kidato cha Sita ya 2008 yalitoka, Manka alikuwa amepata Division 1.7 na ndiye aliyeongoza na Gwantwa alipata Division 2.10 kwa ujumla matokeo yao yalikuwa mazuri sana. Na hivyo kwa kuwa ndoto ya Manka toka udogo wake ni Umeme, na ndio maana alipomaliza darasa la saba alitamani sana aende Shule za Sekondari za ufundi kama Moshi Technical au Ifunda Technical japo haikuwa hivyo, badala yake walimpanga Ashira Girls ambapo aligoma kwenda kusoma. Hivyo baada ya kuhitimu Kidato cha Sita alijua ndio wakati muhafaka wa kuishi ndoto zake, hivyo bila kukosea alijaza Electrical Engineering, na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yaani UDSM a.k.a Mlimani.

Gwantwa alidahiliwa Chuo Kikuu cha St Joseph kilichopo Mbezi Luguruni Jijini Dar es Salaam ambako kinaendeshwa na Wahindi wa Kanisa Katoliki kwa Shahada ya Computer Science, huku Manka akidahiliwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa shahada ya Electrical Engineering. Na hatimaye marafiki walioshibana wanakutana tena Jijini Dar es Salaam kwa Elimu ya Chuo Kikuu.

# 9

## SAKATA LA UTEUZI

**B**REAKING NEWS! Macho ya watu kila mahali yapo kwenye Televisheni ya Taifa, ambayo inaonekana kwa mara ya kwanza Raisi wa Jamuhuri amejitokeza hadharani baada ya wiki mbili ili kuhutubia Wananchi wake mara baada ya skendo ya Ufisadi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini. Baada ya Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchunguzi, ilibainika mikataba ya hovyo ya kifisadi ambayo ilikuwa inalisababishia Taifa hasara karibu Bilioni 70 kila siku. Baada ya Kamati kuwasilisha ile Taarifa na kujadiliwa kwa kina Bungeni, Bunge liliazimia kwamba Waziri wa Wizara hiyo Mheshimiwa Paul Kengeja ajihuzulu, na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dr. Omary Mwala aondolewe haraka. Na ndivyo ilivyotokea, Waziri na Katibu Mkuu wake wa Wizara ya Nishati na Madini walijhuzulu.

Kila mtu ndani ya nchi nzima Bara na Visiwani walikuwa wanasubiri kwa hamu kubwa kwamba Raisi atakapotokea hadharani atasema nini lakini zaidi atafanya nini. Mheshimiwa Raisi wa Jamuhuri Isaya Mrisho Kikwenge, alikaa kimya kwa wiki mbili tangu viongozi hawa kujiuzulu, na leo amejitokeza hadharani na la kushangaza zaidi leo wanaonekana maafisa wa Jeshi wengi Ikulu isivyo kawaida. Baada ya itifaki mbili tatu,

namuona Mheshimiwa Raisi wa Jamuhuri anaelekea kwenye podiumu tayari kwa Hotuba yake. Watu wote wanasimama na kisha wimbo wa Taifa unapigwa na baada ya hapo watu wanaketi tayari kwa kusikiliza.

“Ndugu zangu Wananchi, sote tumesikia yale yaliyojitokeza. Nasikitika sana kwamba pamoja na Mie kusisitiza Uzalendo, Weledi na Uadilifu kila wakati kwa viongozi ninaowateua, bado kuna baadhi ya watu wamebaki na ubinafsi. Ninachoamini Mie Magugu yote yaliyojichnganya na Ngano yatang’olewa maana sasa yamekuwa, na hatimaye tutakuwa na watu waadilifu na Wazalendo na Nchi yetu itasonga mbele.

Nimeamua kufanya uteuzi kwa maamuzi magumu sana, maana najua Wizara hii kila wakati imekuwa ikituletea hasara kubwa badala ya faida, na najua bado kuna watendaji wengine ndani ya Wizara hii wanahitaji kuondolewa. Nimeamua kumteua Brigedia Jenerali John Sanga kuwa Mbunge na Waziri wa Nishati na Madini kuchukua nafasi ya Waziri aliyejiuzulu, na Luteni Dr. Hashimu Mnyange kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii kuchukua nafasi ya Katibu Mkuu aliyejiuzulu. Mungu Ibarki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika!”. Watu wote wakasimama na Mheshimiwa Raisi wa Jamuhuri akaondoka kwenye podiumu tayari kwa kumuapisha Waziri mteule.

Haya yote yalikuwa yakinoteka katika Ukumbi wa nje wa Ikulu Jijini Dar es Salaam. Nchi nzima ilitaharuki na kila mmoja alijiuliza ni kwanini Raisi ameamua kutumia wanajeshi wote kuanzia Waziri mpaka Katibu Mkuu. Sio kitu kilichozoleka kwa Maafisa wa Jeshi hasa wa Ngazi za juu kuteuliwa kwenye nafasi

nyeti za kisiasa kama hizi, na hasa ukizingatia wao sio wanasiasa. Na kwa ilivyozoeleka walau Maafisa wa Jeshi Wastafu ndio huteuliwa kuwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa.

Ni Dhahiri Brigedia Jenerali John Sanga na Katibu Mkuu wake Hashimu Mnyaruge walikuwa na kazi kubwa ya kuondoa uozo mkubwa uliopo hasa kwenye Shirika la Umeme pamoja na Sekta ya Madini. Wakati huu ndio shida ya kukatika kwa umeme ilikuwa kila mahali ndani ya nchi, yaani ilikuwa zaidi ya mgao wa umeme. Ukipita kila mahali penye miji na majiji makubwa ni kelele za majenereta tu. Na kwa upande wa madini, huko migodini wafanyakazi walikuwa wananyanyaswa na kuamriwa hovsky na wawekezaji na huku makampuni ya kigeni yakiiba madini kinyume na mikataba yao, na kuyasafirisha kimagendo. Kimsingi Wizara hii ilihitaji mtu mwenye ngozi ngumu ili kupambana na uozo huu, na kumaliza kabisa haya matatizo na changamoto za Wizara.

Calvin John Sanga, kitinda mimba wa Brigedia Jenerali John Sanga ambaye miezi kazaa alitolewa jeshini na kuwa Waziri wa Nishati na Madini. Calvin kijana mfupi mnene, mwenye rangi ya maji ya kunde, aliyejaa maneno mengi na siasa za kutosha mdomoni, mbishi asiyeshindwa kirahisi. Kila mahali aliposoma sio Makongo O level wala Jitegemee Advance alishika nyadhifa za juu katika uongozi wa Shule. Alipokuwa Makongo High School alikuwa kiranja wa Michezo na Burudani na kule Jitegemee High School alikuwa Katibu Mkuu wa Shule (GS). Ndoto zake kubwa ni kusomea Sheria na kuja kuwa kiongozi wa juu wa siasa, tangu alipokuwa Advance alishakuwa na kadi ya

Chama Tawala cha OCM, na kujiunga na jumuiya ya Vijana ya chama hicho.

Miezi miwili kabla ya ye ye kumaliza Advance pale Jitegemee ndipo Babake Brigadia Jeneral John Sanga aliteuliwa kuwa Mbunge na hatimaye Waziri wa Nishati na Madini jambo ambalo lilimpa Calvin nguvu zaidi za kutamani kuwa kiongozi wa juu zaidi wa Nchi hii. Hata na hivyo tatizo la Calvin lilikuwa ni majivuno, ujuaji mwangi usiokoselevu, starehe za pombe na wanawake na zaidi aina ya marafiki aliokuwa nao.

Calvin ni moja ya watu waliokuwepo kwenye foleni siku ile Lulu aliposhushwa na ile gari ya Mark II wakati alipomfata Mashauri na kuanza kuzungumza nae. Hata hivyo Calvin alidhamiria moyoni kumpata yule binti kwa gharama yoyote, siku zote aliamini watoto wazuri na warembo ni haki yake ya msingi.

Kilichompa Calvin kiburi kila wakati ni mama yake mzazi Dr. Lucia Shemdoe anayefanya kazi Wizara ya Fedha ambaye alikuwa akimpa Calvin chochote anachotaka. Aliamua kumlea hivyo maana wakubwa zake wote watatu ni wasichana na karibia wote walishaolewa wanaishi na familia zao. Hivyo Mama na Mtoto wake huyu wa kiume ulikuwa hauwaambii kitu kabisa. Pamoja na ukali wake wote wa Jeshi Brigedia Jeneral John Sanga alikuwa hawezи kumuadhibu Calvin kwa namna Mama yake alivyokuwa na mbinu za kumtetea. Kitu gani Calvin alitaka asipewe, kwake Maisha yalikuwa mepesi sana. Na maishani mwake hakuwahi kuamini atataka kitu halafu asikipate. Hata siku ile kuhusu Lulu alisema kwa watu wake wa karibu kwamba ni suala la muda tu Lulu ataingia kwenye himaya yake.

# 10

## ZAMA UWEAPONI

“Ninamjua Aliye Mwambaaa, Aliyeniokoa ni Bwana Yesu!!!!

**W**akati vyombo vikipigwa kwa ustadi sana kuanzia Kinanda, Gitaa la Bass, Solo na Drums, ilisikika sauti nzito ya kiume ikiimbisha wimbo huo, na watu walipokelea kwa sauti za Furaha.

“Ahsante Babaaaa, Ahsante Mwanaaaa, Ahsante nawe Roho Mtakatifu!”

Mara sauti ya kike laini na yenyе ustadi iliimbishia hiki kipengele, na watu walipokea kwa sauti za kuzama sana Rohoni.

Wakaati huo ndio kwanza Msichana Lulu alikuwa anapanda kile kilima cha kuelekea CCT- Chapel ya Chuo Kikuu ca Mlimani, hakuwa na mtu mwingine yejote. Kwa kadri alivyosogea ndivyo ambavyo aligundua kwamba watu walikuwa kwenye kuabudu na kuomba kwa namna ambayo kwake ni mpya sana. Alipofika nje ya Chapel mlangoni aliona bango limeandikwa “WELCOME 1<sup>st</sup> Year UKWATA-USCF” na chini yake ikaandikwa “Wanafunzi wa Madhehebu yote ya CCT tunaabudu hapa!”. Yeye alikuwa anafahamu kanisa analosali yaani KKKT lipo pia kati ya makanisa ya CCT, lakini kilichoshangaza ni huo mtindo wa kuabudu ambao hakuwahi kabisa kuuona kanisani kwao.

Ukweli ni kwamba Lulu hakuwa amekuja hapa kusali, kilichomfanya aje ni sms ambayo Mashauri alimtumia kwa simu ya mtu iliyosema “Dada Lulu, mimi Mashauri nimeomba simu kwa mtu, kama utapenda tuonane njoo CCT-Chapel kuanzia saa moja na nusu jioni!”. Wakati sms inaingia Lulu alikuwa amelala chumbani kwake Hosteli, alioshtuka kama saa moja na dakika 20 hivi na kuona hiyo sms alifurahi sana. Maana tangu jioni ile ya

siku walivyoona na Mashauri siku ya kwanza kwenye ile foleni ya usajili hakubahatika kumuona tena. Pamoja na kumuachia Mashauri namba za simu alizomuandikia kwenye kile kikaratasi zilipita siku tano bila kusikia chochote toka kwa Masha kama anavyopenda kumuita yeye.

Hivyo kitendo cha kuona ile sms hakujali sana amevaaje, na kwa kuwa hakufahamu CCT-Chapel aliona akianza kijiandaa anaweza kuchelewa na akakosa kumuona Mashauri na ukichukulia kwamba Mashauri hana simu. Akiwa amevalia suruali ya jeans iliyomkaa vizuri na kuonyesha umbo lake zuri, juu alivalia top moja ndefu, na kwa sababu ya kaupepo akaona walau avae kakoti chepesi juu. Hakuwa amefikiri kwamba Mashauri alimuita aje kanisani, yeye alidhani ni Meeting point tu. Lakini baada ya kuuliza watu wawili watatu mpaka akajua ilipo CCT-Chapel, kwa kadri alivyokuwa anaisogelea akaanza kugundua mbona ni kama watu wapo Ibadani. Ilibaki kidogo arudie njiani, ila kwa namna alivyokuwa na shauku ya kuonana tena na Mashauri ikabidi ajikaze na kufika mpaka mlangoni.

Alipofika mlangoni alishangaa alipokelewa na Wadada waliovalia sketi ndefu na magauni marefu mpaka akaona aibu, mmojawapo wa wale wadada akampa kanga afunge, Lulu hakuwa na ubishi hivyo akaichukua akafunga. Na kisha mwingine akamwambia karibu Dada nifate, Lulu huku akiwa na uoga na Mshangao akaamua kumfuata yule Dada. Wakati wanaingia ndani alishangaa namna watu walivyojaa, wote wamesimama wamefunga macho na wameinua mikono yao juu. Yule Dada akampeleka mpaka kitit cha tatu kutoka mbele, akamuonyesha ishara akae hapo. Lulu bado aliquwa haelewi sana

kinachoendelea, ila kwa kuwa alitamani kumuona tena Mashauri ilibidi akubaliane na hali. Na ye ye akasimama, akanyoosha mikono juu japo kichovu na kiaibuabu ila hakufunga macho. Hakuamini macho yake alipoangalia mbele na kuona kwamba kumbe ile sauti ya kiume aliyokuwa anaisikia ikiimbisha alipokuwa nje, ni sauti ya Mashauri.

**“Heri Heshimaaa na Enzi yakoo, na Enzi yako oo na Enzi yako ooo,**

**Heri Heshima na Enzi yakoo Sasa aa na Milele eeee!!”**

Wakati huu Mashauri alikuwa akiimbisha wimbo ulionekana kufanya Watu kuomba zaidi, wengine walisikika wakilia na kububujika. Wachache walipiga magoti, wengine walionekana kupiga makofi. Wakati anashangaa na kuwa na sitofahamu juu ya kinachoendelea, Akaona kuna binti mwenye umbo la wastani karibu na Mashauri akapokelea kwa sauti nyororo na stadi sana

**“Heri Mikuabudu kwa uzuri wako, kwa Uzuri wakooo, kwa uzuri wako oooooooo,**

**Heri Nikuabudu kwa Uzuri wako ooo sasa na Milele eeeh!”**

Hapa sasa alisikia ukumbini maeneo tofauti tofauti Watu wanasema “AHSANTE YESU, AHSANTE YESU!”

Kwa namna hali ilivyokuwa, alijikuta amefunga macho na walau na ye ye anasema sasa “AHSANTE YESU!” Baadae ndio alikuja kugundua ile ilikuwa ni Ibada maalumu ya Shukrani kwa Mungu pamoja na kuwakaribisha First Year. Na ndio maana wale

wote waliokuwa pale mbele ni First Year waliopewa nafasi ya kuongoza wengine katika kuabudu pamoja na maombi ya shukrani. Walihitimisha Ibada kwa Soda na Bites huku First Year wakijitambulisha majina yao, walipomaliza Advance, wanapotokea na Shahada wanazosomea. Yeye pale alitamani kafahamu watu wawili tu, yaani yule dada aliyekuwa akiimbisha na Mashauri na kaka mwingine Mashauri alimpa kipaza sauti na akaongoza maombi ya Shurkani.

“Naitwa Atupele Mwakalinga, nimemaliza Iyunga Technical High School-Mbeya, nyumbani ni Mbeya Iyunga, na nipo hapa kwa Shahada ya Computer Engineering kwa Neema ya Mungu” Alisema yule kaka aliyeongoza maombi ya Shukrani. “Mashauri Jonathan Mkumbo, nimemaliza Mzumbe High School, nyumbani ni Singida, Bachelor of Science In Electrical Engineering” Mashauri alisema kwa ujasiri ambao Lulu hakudhani anao. Lulu alikuwa anamsubiri yule Dada kwa shauku sana ambaye aliketi pembeni ya Mashauri, kama kitie kimoja kutokeaa alipo keti yeye, na kwa hiyo kivyovyyote baada ya Mashauri ni yeye. “Naitwa Manka Sifueli Mrema, nimemaliza Loleza Girls High School Mbeya (PCM), Mimi ni mwenyeji wa Moshi-Kilimanjaro na nipo hapa nachukua Shahada ya Electrical Engineering” alimaliza yule binti aliyekuwa na sauti nzito mno, kiasi kwamba usingeaminii kwamba ni yeye alikuwa akiimba vizuri vile. Lulu alitahamaki alipogundua licha ya kuimba pamoja na Mashauri, bado yule binti alikuwa anasoma darasa moja na Mashauri. Kiukweli hii ilimfanya ameze fundo kubwa la mate, kiasi kwamba alipofikiwa alisita kwanza kisha akajiweka sawa na kwa sauti yake Nyororo ya kisichana akasema “Miss Lulu Stephen

Mollel, from Arusha. Advance level St Joseph Girl High School, Pursuing Barchalor of Art in Law!” yaani kila mtu aliyekuwepo mle Chapel alishangazwa na uzuri wa yule binti, na zaidi namna alivyotamka matamshi ya maneno ya kingereza kama amezaliwa nacho. Na wengi hawakutumia nguvu kubwa kujua anatoka familia ya matawi ya juu. Unajua wakati wote huu Madhauri hakuwa anajua kuwa Lulu yuko mle Chapel mpaka aliposikia Miss Lulu ndio akajigeuza shingo na akaona ni yeye, na akagundua alikuwa amekaa kitit cha nyuma yao.

Walipotoka nje, wakati wapendwa wanasalimiana na kutambuana zaidi, Mashauri akiwa na Manka wakamfata Lulu, “Manka huyu anaitwa Lulu ni Dada yangu na Rafiki yangu!” Alisema Mashauri. “Manka”, Lulu alisema. “Eeh umejuaje?!” Manka aliuliza. “Nilipenda ulivyokuwa unaimba nikatamani kukufahamu, so I was just curious to know you, Are you Chagga?!” Lulu alisema huku akimaliza na Ung’eng’e kama kawaida yake. “Lulu ahsante sana kwa kuja Dadangu!” alisema Manka “Ahsante pia Masha, Ila jamani kwanini hukuniambia ni Ibada mpaka nakuja navalishwa kanga jamani” Lulu alisema kwa madeko na malalamiko kidogo. “Oooh nisamehe Dadangu, si unajua tena simu za kuazima!” Mashauri alijibu kwa unyenyekevu sana. “Usijali Masha, Manka have you eaten dinner guys?!” Aliwauliza Lulu. Na baada ya dakika tano walionekana wakishuka kilima cha Chapel na kuanza kuelekea Cafeteria ya karibu tayari kwa kupata dinner.

“Guys, nimependa mnnavyoimba kiukweli. Engineers Singers watu wa hasi na chanya!” Lulu alisema na kuwatania. “Ahsante Lulu!” Manka alijibu. “Utukufu kwa Mungu!”

Aliongezea Mashauri. “Yaani ujue mimi nimesoma shule za Seminari za Kikatoliki za Masister form one mpaka form six, na home huwa tunasali Lutherani tena English Service, so everything was very new to me today!” Alisema Lulu. “Usijali, utajifunza na kila kitu kitakuwa sawa!” Alimfariji Mashauri. “And another challenge, yaani Room kwangu nakaa na wadada siwaelewi kabisa!” Alilalamika Lulu, na akaongezea “Masha please, naomba sana usiniache unikumbushe walau niwe nahudhuria Kanisani, sawa Rafiki yangu?!” “Usijali Dada Lulu!” Masha alisema kwa ujasiri. “Promise Me! Mbele ya Manka!” Lulu alisema huku akinyoosha mkono kumuelekea Mashauri ili washikane mkono kwa ishara ya ahadi. Ikumbukwe hapa ilikuwa Cafeteria wakati wanakula chakula cha jioni. Kidogo Mashauri agome kutoa mkono kwa aibu na kulinda ushuhuda. Ila akili yake ikamwambia toa tu mkono, maana hata hivyo wapo na Manka, maana wangkuwa wao wawili tu ndio ingekuwa picha mbaya zaidi. Ila walau sasa kuna mtu mmoja wa kulinda Ushuhuda. Basi Mashauri akanyoosha mkono na kushikana na Lulu na akasema “I promise Dadangu” kwa namna mkono wa Lulu ulivyokuwa mzuri mweupe na mlainii, Mashauri hakuamini kama ni mkono wa mwanadamu wa kawaida. Alijikuta mapigo ya moyo wake yakienda mbio na akaingiwa na uoga maradufu. Kwa haraka akatoa mkono wake!

# 11

## MBWEMBWWE DARASANI

**K**itivo cha Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye moja ya Lecture Theatre zake kubwa, alionekana Wakili Msomi Maherufu na Mhadhiri Mbobevu wa Sheria Dr Ronald Kimaro akiwa anapandisha ngazi tayari kwa kuingia darasani. Dr Kimaro ni mmoja kati ya Wahadhiri (Lecture) wa siku nyingi sana Chuoni hapa, na sio rahisi usome Semister yoyote bila kufundishwa na yeye. Daima alifundisha vizuri kwa madaha na kwa kuchekesha mara nyingi wanafunzi walitamani kipindi chake kisiishe haraka. Licha ya kuwa na umri wa zaidi ya miaka 55 sasa, Dr Kimaro hakuwahi kuoa wala kuwa na historia ya familia. Kila wakati alijiweka kama kijana hivi kuanzia mavazi mpaka tembea yake.

Tangu akiwa na umri wa miaka 25 mara baada ya kuhitimu Shahada yake ya kwanza Chuoni hapo kwa ufaulu wa juu sana wa G.P.A ya 4.8. Chuo kilimbakisha Chuoni hapo kama Mwalimu Mwanafunzi kule chuoni wanamuita Tutorial Assistant, na tangu hapo licha ya kutoka kwenda kujiendeleza kielimu nchi mbalimbali, amekuwa akifundisha kitivo cha sheria kwa zaidi ya miaka 25. Dr Ronald Kimaro hakuwa mlevi hata kidogo, ila tatizo lake kubwa lilikuwa Wanawake. Siku hii ndio alikuwa anaingia darasani kwa mara ya kwanza na kama mwalimu wa kwanza kabisa kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza tangu wameengia chuoni. Chuo kilikuwa kimedahili Wanafunzi wengi wa Sheria kwa mwaka huu kuliko miaka mingine yote. LT5 ilionekana kujaa wanafunzi kila mahali tena kwa kubanana sana.

“Oooh Amazing, our country gonna have a lot of Lawyers!” Alisema Dr Kimaro huku akipandisha suruali yake juu kidogo. “How many are you guys?!” Dr Kimaro aliuliza kwa bashasha. “Fuor Hundred” Darasa lilijibu kwa pamoja. “Oooh, bado information is only 200 hundred will make up to final year” Aliwatisha Dr Kimaro wakati huu akiwa anaisogelea podiamu na akiiegemea kwa mkwara kidogo, kisha akashusha miwani yake kidogo ili aone vizuri halafu akasema “You have 4 tough years to make your dream time, but I tell you in these 4 tough years only the tough will get going”. Dr Kimaro huwa anatabia ya kuzungumza maneno mengi, ila wakati huo anakagua darasa mtu baada ya mtu. Na wakati akiwa anawapa hawa 1<sup>st</sup> year wa sheria Orientation nzuri macho yaligonga kwenye moja mistari ya katikati ambao walikuwa wamekaa wasichana watatu. Mmoja ni mwenye weusi wa kuteleza aliyeonekana kujazia ukimtazama hata

kwa juu, mwingine alikuwa mwenye weupe wa wastani na mwili wa kimiss, yaani mjini wanaita kipotable. Na watatu alikuwa mweupe pee, mwenye sura nzuri kama ya mtoto wanaita Baby face, na ni dhairi huyu alionekana ana kila alichotakiwa kuwa nacho msichana mzuri. Na baada ya hao wadada watatu walionekana vijana wawili wa kiume, ambao kwa haraka haraka tu unggendua wapo nao ama wanajuana vizuri. Kijana mmoja alikuwa amejazia sana kifuana mikono na alionekana ni mrefu sana, na huyu mwenzake alikuwa mfupi mnene mweupe aliyevalia kama tayari ni mwansheria serikalini. Akili na hisia za Dr Kimaro zilikuwa kwa yule binti aliyekuwa mweupe sanaa na mwenye sura kama ya mtoto. Kimsingi kama kawaida yake alijiambia moyoni “mwaka huu naanza na yule”. “My names are Advocate Dr Ronald Robart Kimaro your Lecturer, will be with you in all eight semisters, goodluck!”. Alimaliza Dr Kimaro na kutoka nje kwa bashasha sana.

Ile crew ya wale wasichana watatu na wavulana wawili, ilikuwa ni kundi la kina Irine, yule alikutana na Hamidu kwenye gari wakiwa wanatoka Bukoba kuja Dar. Wa pili ni Queen msichana wa mjini aliyesoma Jangwani kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, na Rafiki yake Irine maana walisoma wote kidato cha tano na sita Jangwani HGL. Msichana wa tatu ni Lulu Mollel yule binti mrembo kutoka Arusha.

Lulu alijikuta amepangwa chumba kimoja cha Hostel na Irine na Queen na baadae aligundua kwamba wanasomea Sheria. Na leo wakati wanakuja darasani ilibidi waongozane pamoja maana hakuwa na jinsi, na walipofika darasani waliketi sehemu moja. Na wale wavulana wawili, mmoja yule mrefu aliyejazia

kifua ni Hamidu mpenzi wake na Irine waliokutana kwenye Princess Muro wakiwa wanatokea Bukoba na walijikuta wanaingia kwenye penzi. Na wa mwisho yule kijana mfupi mnene mweupe mwenye suti ni Calvin John Sanga mtoto wa Brigedia Jemerali John Sanga ambaye ni Mbunge wa kuteuliwa na Rais, na Waziri wa Nishati na Madini.

Calvin na Hamidu ni marafiki wa muda mrefu maana walisoma wote O level Makongo tena darasa la Arts, na baadae wakaamua pamoja wakasomee Jitegemee Sekondari Advance baada ya kupangiwa na serikali shule za mikoani ambazo hawakuzipenda. Kwa hiyo Queen na Irine ni marafiki wa tangu Advance Jangwani Sekondari, na Hamidu na Calvin ni marafiki wa watoto wa Wanajeshi ambao wote wamesoma Makongo na Jitegemee. Na Queen, Irine na Lulu wanaishi room moja Hosteli. Na vijana wote hawa watano wanasomea Sheria, na wamekuwa wakwanza kuingia kwenye fikra na macho ya Mhadhiri Matata Dr Ronald Robart Kimaro.

Calvin John Sanga, mtoto wa Waziri alijiona mwenye bahati sana siku ile. Maana yule binti aliymchanya tangu alipomuona kwa mara ya kwanza kwenye foleni, hatimaye siku ya kwanza ya kuingia darasani anajikuta amekaa nae karibu, na haitoshi eti anaishi chumba kimoja na girlfriend wa rafiki yake Hamidu. Calvin kijana mwenye sifa na ujuaji mwingu hii siku alitulia tuli darasani kama mtu makini na mzee wa busara ili asije akajiharibia kwa merembo wa ndoto zake za chuoni.

Mara baaada ya Dr Kimaro kutoka darasani, Hamidu na Irine walionekana kukumbatiana darasani huku wakipeana

mabusu ya haja kwa muda mrefu kana kwamba ni wapenzi waliopoteana mda mrefu, kumbe jana yake tu walishuka kwa pamoja na basi la Princess Muro. Wakati wao wakikumbatiana Queen ye ye alikuwa bize kuwapiga picha na simu yake ya Motorola kipindi hicho inaitwa bapa. Calvin ye ye alikuwa anajaribu walau kumuongelesha Lulu ambaye alikuwa bize akijifanya anakagua kagua vitu kwenye simu yake mpya na iliyooonekana ghali ya Sony Ericson.

# 12

## WAKAMATA WINGU

**M**ashauri na Manka walitokea kusatana sana kiukweli, na katika darasa la mwaka wa kwanza la wanafunzi wanemosoma Electrical Engineering ambao walikuwa 60 tu, 10 ndio walikuwa wasichana. Na hivyo katika makundi 10 ya kujisomea darasani kila kundi lilikuwa na msichana mmoja na wavulana watano. Na katika kundi la Mashauri na wenzake wanne, Manka ndiye alikuwa msichana.

Mashauri na Manka ni kama walionekana pamoja kila mahali na kila wakati, Darasani walikuwa pamoja, Dini (Fellowship) walienda pamoja na mara kwa mara walipanda pamoja Cafeteria kwenda kula. Kwa haraka haraka kila mtu angelifikiria kwamba watu hawa ni wapenzi ama wana undugu au wamefahamiana siku nyingi sana. Japo ukweli ni kwamba katika yote hayo hakukuwa na jibu sahihi, maana sio wapenzi wala sio ndugu na wala hawajafahamiana siku nyingi, Ila imetokea tu kwamba wanaendana na wamepatana kwenye mengi.

Kwa asili Mashauri na Manka sio waongeaji wala watu wa kujichanganya sana, wote ni watu wanaopenda Maisha rahisi yasio na gharama wala kijitutumua ili kuonekana wote walikuwa

wanapenda sana Uimbaji hasa wa nyimbo zile za taratibu ambazo walokole wanapenda kuita za kuabudu. Wote walikuwa ni watu wa kusoma ule msuli mrefu haswa, sio kwa sababu hawana uwezo mkubwa ila walipenda sana akisema anaelewa kitu iwe ni anaelewa kweli kweli. Kila aliposoma Mashauri sio Mazengo Sekondary au Mzumbe, daima wenzake walikuwa wanamtania kwamba AMETUMWA NA KIJIJI. Yeye huwa ni mzee wa kukamia, akianza kusoma saa mbili usiku basi kwa uchache sana angemaliza saa sita au saba usiku ndio akalale, na hapo anaweza kujificha mahali na akaomba kwa lisaa lizima halafu ndio aende kulala.

Manka tangu anakuwa yeye ni mtu wa kampani za wavulana, isingekuwa umbo lake zuri la kike ambalo pamoja na kuvala kwake kama mwanaume bado lilionekana, kila mtu angeweza kuhisi yeye ni mwanaume. Na si unajua tena vile wanafunzi wa Engineering hasa wa umeme wa magari vile huwa wamevaa, kwa kifupi wao huwa rafu kila wakati. Hivyo Manka kuambatana na Mashauri kila wakati na kila mahali kwake haikuwa ishu kubwa wala jambo ya ajabu. Ndani ya miezi miwili tangu wakutane walishatunga nyimbo za kuabudu zaidi ya mbili na ambazo walizifanyia mazoezi kila walipopumnzika baada ya kuboreka kusoma.

Siku moja Atupele akiwa anatoka kwenye madarasa yao ya watu wa Computer Engineering majira kama ya saa kumi na mbili za jioni, akawa anasikia kwa mbali kuna watu wanaimba mahali, na kwa kadri alivyokuwa anasogelea madarasa ya wanafunzi wa Electrical Engineering kwa mbali akawaona Manka

na Mashauri wamekaa kwenye vimbweta karibia na uwanja wa Basketball halafu wanaimba. Ikabidi awafate pale,

**“Wewe ee we ni Mungu Mkuu, Weweee eeeh ni Mungu Mkuu,  
Peke yako oooh ni Mungu Mkuu, Peke yako oooh ni Mungu  
Mkuu!!”**

Ndivyo Mashauri na Manka walikuwa wakiimba maneno haya ya kumsifu na kumuabudu Mungu kwa sauti zilizopangika vema na kwa ustadi sana. Mpaka Atupeke amewafikia na akasimama nyuma yao, hakuna yejote kati yao hata alihisi kuna mtu kwa namna ambavyo walikuwa wamezama na kunogewa na vile wamemachi kwenye kuimba. “Wapendwa mmenibariki moyo wangu sana, sio kwa kushusha huko wingu la BWANA maengineer!!” Alisema Atupele, ndio wakashtuka sana na kuona kumbe Atupele alikuwa nyuma yao kitambo. “Amina Mtumishi!” Wakaitikia kwa pamoja kama walikuwa wamepanga. Haya ndio yalikuwa Maisha ya awali ya chuoni ya Mashauri na Manka.

# 13

## KULA UJANA

**G**ari aina ya Prado TX mpya ya rangi nyekundu yenye usajili TZS 942 ilionekana kupaki mbele ya Hosteli ya wasichana BLOCK E ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ndani yake alionekana Mbaba wa haja mwenye asili ya Kihindi, tangu asimamishe gari hapo hakushuka, bali alionekana kupiga na kuokea simu mbili tatu. Mara baada ya dakika kama kumi hivi, Queen yule msichana ambaye ni Rafiki yake na Irine, na ambaye anaishi chumba kimoja na Lulu alionekana kushuka ngazi za Hosteli na kuelekea lilipo lile gari. Alikuwa amevalia mini-sketi fupi sana iliyokuwa juu sana ya magoti ya rangi nyekundu, na juu alivalia top ya njano iliyombana sana huku kitovu kikiwa nje. Na kwa namna alivyokuwa mrefu wa haja, na mweupe wa wastani, tena mwenye umbo la wastani sio mnene na wala sio mwembamba, huku hipsi zikiwa zimepangika vizuri na huku nyuma ndio usiseme. Kila aliymuona kama alikuwa anatembea alisimama kidogo kushangaa, waliokuwa Hostel magorofani kila mmoja aliacha anachofanya wakaitana kumuona binti yule mrembo aliyevaa kama changudoa au watu waliopo CLUB na CASINO.

Yule baba mwenye asili ya kihindi alipoona Queen amefika karibu na gari, akashuka na kwenda kumfungulia mlango wa mbele wa abiria. Kisha baada ya Queen kupanda, akamfungia mlango kisha akazunguka kwenda nafasi yake ya dereva. Na baada ya dakika mbili Prado TX likawa linaambaa kwa maeneo ya Chuo kuelekea ilipo Mlimani City, halafu likashika njia ya kuelekea Tegeta. Kumbe hii siku huyu Mbaba Maliki Pateli Tajiri mkubwa wa yards za magari Jijini Dar es Salaam, alikuwa amekubalia na mrembo Queen waende zao Bagamoyo kuspendi weekend.

Haya ndio Maisha ya Queen rafiki wa karibu wa Irine, tangu alipokuwa kidato cha tatu mara baada ya Dada yake kupunguzwa kazini kwenye kiwanda cha Urafiki. Queen alikuwa wa kumtegemea dada yake huyo kwa kila kitu, yeye na Dadake ni mabinti pekee kwenye familia yao iliyopo kule Kasulu Kigoma. Familia yao ni masikini mno, na mwaka mmoja tu uliopita Baba yao Mzee Kishangwe alifariki dunia. Mara baada ya kumaliza darasa la saba ilimbidi dada yake amchukue Queen ilia je kuishi nae na kumsomesha huku Dar es Salaam. Alipofaulu darasa la saba na kupangiwa shule za kule, Dadake alihangaika mpaka alipata nafasi Jangwani Sekondari japo alisoma DAY. Kwa hiyo baada ya Dadake kupunguzwa kazini na Maisha kuwa magumu, Queen alijikuta anajilingiza kwenye mapenzi na Wanaume ili kujikimu mahitaji yake kama msichana. Na kwa uzuri aliojaliwa na Mungu, wanaume wengi wenye pesa walijibaraguza sana kwake. Na yeze kwasababu ya Utamu wa hela na starehe aliwapanga ipasavyo. Na kwa yeote ambaye angegundua kwamba wako wengi na kujaribu kumgombeza Queen, basi Queen

alitishia kumshtaki shulen na angefungwa kwa sababu yeye ni mwanafunzi. Queen alikuwa makini kuanzia kwenye kucheza na kalenda, kutumia vidonge vya majira ili kuzuia mimba, na asingekubali kulala na mtu bila kutumia kondomu. Kwake usalama ulikuwa kipaumbele na pamoja na kujifunza kunywa Wine bado alihakikisha halewi hata siku moja. Mchezo wake huu ulimfanya akasoma na hatimaye sasa nyupo Chuo Kikuu. Na katika Maisha yake, yeye hajui suala la kumpenda mwanaume. Anachokiangalia anapokupa mwili wake anafaidikaje na wewe, na ndio maana huwa hachagui rika, anachojali ni pesa.

Hii Ijumaa Alasiri wakati Queen akiwa anaelekeea na mhindi wake Bagamoyo kwa mapumziko ya wikiendi, Irine na Hamidu wao walikuwa kwenye nyumba ambayo Calvin alipewa na mama yake aishi kule Sinza Mapambano. Calvin aligoma kabisa kuishi Hostel, na baada ya mama yake kujua kuwa Calvin amegoma jumla, na kwa kuwa huwa hapendi mwanae akose raha aliamua kumuhamisha mpangaji aliyekuwepo kwenye nyumba yake ya Sinza Mapambano, na kisha akampa Calvin na kumuwekea kila anachokitaka ndani.

Wakati Hamidu akiwa jikoni na Irine aliyekuwa anaandaa mahanjumati, Calvin alikuwa sebleni ametulia tuli kwenye kochi. Movie matata ya No Retreat, No Surrender ilikuwa inaendelea kwenye screen kubwa iliyokuwepo pale sebleni lakini Calvin hakuonekana kuielewa kabisa. Alionekana amezama kwenye dimbwi la mawazo makali sana, mwishowe alisikika tu pale sebleni akisema kwa sauti “NOT MEEEEEE!!!!” halafu akagonga meza iliyokuwepo mbele yake ya kochi alilokuwa amekalia.

Hamidu aliyejikuwa na mpenzi wake Irine jikoni wakijipikilisha huku wamekumbatiana muda wote walisikia ule ukelele wa Calvin alioupiga sebleni ukiambatana na kugogwa meza. Waliposikia hayo, Hamidu akamuacha Irine aendelee na mapishi jikoni kisha yeche akaenda sebleni kujua kilichomsibu swahiba wake. “Hoyaa Arifu nini shida aisee??!!” Hamidu aliuliza, “Yule manzi Lulu mwanangu!” Calvin alisema kwa masikitiko sana. Halafu akaendelea “Mimi Calvin mtoto wa Waziri, mwenye Mama BOT nashindwa kumpata yule demu kweli miezi miwili sasa aisee??!!” “Halafu kuna Mshamba mmoja anazunguka nae tu chuoni aisee, NASEMA SIKUBALI na SITAKUBALI!” alisema Calvin. Pamoja na Queen na Irine kuishi chumba kimoja na Lulu na kujaribu kujenga ukaribu na urafiki nae, na hatimaye wamlainishie Calvin, Lulu hakupenda kabisa mifumo ya Maisha waliyokuwa wanaishi Irine na Queen, sio kwamba Lulu alikuwa Mcha Mungu sana au Mtu wa Imani kivile. ILA basi tu aliwaona wale wadada wanaongea sana, wanajifanya wao ni wajanja sana wanalijua Jiji na hivyo wanataka kumfundisha Maisha. Lulu alikuwa anashangaa sana namna ambayo Queen alikuwa akiongea kwa simu na wanaume tofauti tofauti na vile alivyokuwa anawapanga kwa ustadi wa hali ya juu. Lakini pia alimshangaa sana Irine vile ambavyo anaendeshwa na Hamidu kana kwamba tayari ni mke wa Hamidu, Maisha ya hawa mabinti hayakumuingilia akilini hata kidogo. Na ndio maana walishindwa kabisa kujenga nae ukaribu walidhani itakuwa rahisi, na takribani miezi miwili sasa na wameshindwa kumshawishi kwa lolote zaidi ya kuongozana nae darasani tena muda wa asubuhi tu.

“Calvin, Lulu ana mtu wake tena huwa anakuja kumchukua chuoni kila Ijumaa jioni au Jumamosi asubuhi na Mark II flani hivi mpya, mwenyewe anaonekana Mbaba mbaba hivi” Irine alimwambia Calvin ambaye alionekana mpaka kupoteza hamu ya chakula. “Una hakika lakini??, Ila hata kama, kwanza hilo gari lilimleta siku ile siku ya kwanza tu aliyokuja chuo”. Aliuliza, akajijibu na kutolea maelezo ya kina mwenyewe, huyo ndio Calvin mjuaji na asiyeshindwa.

“Jamani yule Masai kweli ni mzuri, tena mzuri has ahata sisi tunakubali, ila dharau na maringo aliyonayo ni hatari tupu. Na anavyojifanya kushangaaa Maisha yaw engine wakati yeye mwenyewe anatembea na libaba likubwaa!” Alisema Irine kwa msisitizo.

“Kevo, sisi ni timu HATUSHINDWI. Kwanza Makongo mpaka Jiteute wanatujua. Peace and Love Swahiba, Mtoto lazima aingie kwenye kumi na nane zako!!” Alisema Hamidu kwa mbwembwe huku akimpa tano Calvin.

Vijana hawa watatu kwa pamoja walikaa Dining room wakala na kunywa na ilipofika usiku kama saa nne hivi wakaanza safari na gari yao aina ya Rav 4 ambayo Calvin alipewa na mama yake imsaidie kutoka nyumbani kwenda Chuoni. Usiku huu walikuwa wakielekea Club BILCANAS ambapo Msanii O TEN na Q CHIEF walikuwa wanapiga bonge ya SHOW.

# 14

## MATUNDA YA MWANA!!

**B**i Wankembeta Makalla alionekana mwenye Furaha sana hii siku, ni baada ya mdogo wake Lumba kutoka makao makuu ya wilaya kwenye ofisi za Posta ambako alienda kuchukua kiasi cha Fedha ambacho Mashauri alikuwa amewatumia. Baada ya Mashauri kupata Fedha yake ya kwanza ya mkopo, chuoni wanaita BOOM, kiasi cha fedha zaidi ya laki tano. Aliamua kumtumia mama yake laki na themanini kupitia Posta kwa njia ya EMS, lengo lake ilikuwa ni iwasaidie kwa matumizi ya hapa na pale nyumbani lakini kiasi kikubwa ilikuwa ni kwa ajili ya kununua mabati na mba. Mashauri alidhamiria kwamba atajitahidi kujinyima chuoni ili walau kila anapopata BOOM alitume nyumbani kwa malengo walau ya kumjengea Mama yake nyumba yenye vyumba viwili, chumba na sebule za matofali ya kuchoma, halafu na iezekwe kwa bat.

Kwa hiyo ndio aliamua sasa aanze kununua kidogo kidogo mabati na mba, halafu baadae inakuwa ni kufyatua matofali tu na kuchoma pamoja na hela ya fundi. Bi Wankembeta alifurahi sana kuona kile ambacho Mashauri alimuahidi kinaanza kutimia taratibu. Mtoto wake huyu wa uzeeni na wa pekee anafanyika baraka sana, basi alichofanya akachukua hela kidogo akampatia

Lumba walau aende sokoni akalete nyama nusu “nama” na mchele “mshele” nusu ili walau leo wafurahie pilau ya matunda ya kumlea Mashauri au “Masha”.

Mashauri Jonathan Mkumbo, kijana wa Kinyiramba aliyefanya maamuzi ya kumpokea Yesu Kristo kuwa BWANA na Mwokozi wa Maisha yake tangu alipokuwa kidato cha Tatu, hii ilitokea kwenye Mkutano wa PASAKA wa UKWATA mkoa wa Dodoma wao hupenda kuita EASTER CONFERENCE. Tarehe 8/04/2004 wakati Mwalimu wa Neno Kuu la Mkutano huo toka,

**Ayubu 22:21 “Mjue sana Mungu ili uwe na amani, ndivyo mema yatakavyokujia”** Anamalizia kufundisha, aliita watu wanaotaka kumpa Yesu Maisha yao wapite mbele. Mashauri alikimbia kama risasi, Roho Mtakatifu alimshuhudia ndani yake ya kwamba anahitaji kubadilika na kujungamanisha na Mungu. Tangu wakati huo Mashauri hakuwahi kurudi nyuma.

Kila wakati alipokaa na marafiki zake kina Manka na wengine, alikuwa akishuhudia jinsi ambavyo Mungu amekuwa akimuinua hatua kwa hatua, Imani hata Imani na Utukufu kwa Utukufu. Alikuwa na mfano wake mmoja ambao wengi walikuwa wanamchukulia kawaida, lakini yeze aliamini na aliupa uzito sana. Mashauri alikuwa anasema hivi “Mungu ameniinua kutoka Nkito-Singida, Akanipeleka Mazengo-Dodoma, akaniinua tena kwenda Mzumbe-Morogoro, na sasa kanileta Mlimani-Dar es Salaam. Na kama mjuavyo hapa kuna Airport!!!!” Kwa hiyo yeze aliniamini hii Singida-Dodoma-Morogoro-Dar es Salaam ni ishara ya kuinuliwa toka hatua moja kwenda nytingine. Mwenyewe huwa anakiri na kusema yeze ni muujiza unaotembea, aliamini sana

atafika mbali. Kama ungemuuliza Mashauri swali kuhusiana na mapenzi, wasichana pamoja na kuoa, basi ungekuwa umepotea njia. Yeye alikuwa anaamini kwa sasa mwanamke wa Maisha yake ni mama yake tu, hakuwahi kufikiria tofauti na hapo. Na kwa hiyo wasichana wote waliokuwa karibu nae sio Lulu wala Manka na wengine wote wa Fellowship aliwachukulia kama dada zake na sio tofauti na hapo. Na ndio maana mara zote alizoitwa na Lulu mahali basi lazima angeenda na Manka ama mara nyingine Mtumishi mwenzake Atupele. Yeye kwake hakuwa anajua haya mambo ya faragha wala nini, hata wadau wengine walipokuwa wanamwambia “Wee jamaa yule Mrembo anakupenda kinyama yaani” wala alikuwa hawaelewi zaidi ya kuwaambia hizo ni fikra za kipepo. Huyu ndie Mashauri bhana, ambaye alikuwa chuma kwelikweli tena kisichoyumbishwa na chochote. Unajua hata kile jitendo cha kumpa Lulu mkono ile siku pale Cafeteria akiwa na Manka kilimfanya ajutie sana kiasi cha kuingia kwenye maombi ya Toba siku tatu za mfungo.

# 15

## MAISHA YA HOSTELI

**M**aisha ya Lulu ndani ya hiki chumba cha Hosteli yaliyoonekana kuwa magumu kwa kadri siku zilivyokuwa zinaenda. Kila siku alikutana na Mkasa huu na kisa hiki. Queen na Irine waliamua kwamba wanahakikisha wanafanya lolote kumkomoa na kumuonyesha, wao walikuwepo kwenye hili Jiji kabla yake. Baada ya Queen na Irine kushindwa kumshawishi Lulu awe rafiki yao na hatimaye wamuunganishe na Calvin, sasa waliamua kuonyesha chuki na Uadui kwa Lulu tena waziwazi. Kama ujuavyo mambo ya Wasichana kuna wakati walimsema akiwemo hapo hapo na kuangusha cheko la kishambenga, lile la dharau na la kuudhi sana.

“Anajiona Mzuri mwenyewe kama haendi chooni mle, kwanza akienda hata huku hakukaliki kwa hiyo harufu!!” Alisema Queen kwa dharau. Na kisha wakagonga na Irine huku wakisema “Haloooooo, halo ya foma Bibi”. Wakati huo Lulu alikuwa kitandani kwake yupo na laptop yake anajaribu kupitiapitia baadhi ya slides za Business Law za Dr Kimaro.

“Imagine, eti anatoka sijui wanapaita Chuga, ila na ujanja wote anakataa vijana kisa libabu lenye Mark II, aibuuu!” alisema

Irine kwa mbwebwe huku kajisahau kwamba shosti ake Queen yeye huwa hachagui anapita na yeote na muhimu huwa ni hela. Baada ya Queen kusikia alichosema Irine, akaamua kupotezea “Shosti tusome, Dr Kimaro kesho test yake, shauri yako na unamjua jinsi alivyo na sifa!!” Halafu akaongeza, “Nasikia Yule Dr kila semester anatufundisha, na unaambiwa udhaifu wake ni watoto wazuri kama sisi, mimi bhana lazima nijilengeshe nipite nae, yaani hapo nakwambia kila Semister nina uhakika na A zangu mbili za bure bure!” “Mmmh mwenzangu wewe hushindwi ila ndio mpaka akutake sasa, na asipokutaka?” alisema Irine. “Kwa mshape huu, rangi hii na sura hii, mwanaume gani rijali atakataa mchezo??!!” alijibu Queen huku akisimama na kujitingisha tingisha. Wakati yote haya yakiendelea Lulu alikuwa kimya anajisomea tu japo alikuwa anaumia moyo sana kwa kusemwa tena bila kosa. Hakuwahi kudhani haya ndio maisha ya Chuo Kikuu ya watu wanaojiita wasomi, katika kusoma kwake kote kuanzia Precious Blood mpaka St Joseph hakuwahi kuona wala kukutana na vimbwanga vyta namna hii. Kwa miezi hii miwili sasa amejionea ubaya na ujinga wa kila namna kutoka kwa mabinti wawili tena anaosoma nao Sheria wanaojiita watoto wa mjini.

Mara kadhaa amekuta kuanzia mafuta, sabuni, dawa ya meno, manukato na vitu vyake kidogo kidogo vimetumika bila ridhaa yake. Na leo anasikia anasemwa eti kwamba anatembea na mwanaume ambaye huwa anamfuata na Mark II chuoni, bila Irine na Queen kufahamu kwamba Yule ni Saruni Mollel ambae ni Baba yake mdogo. Mara kadhaa Mr Saruni huja kumchukua Lulu Ijumaa chuoni ili akapumnzike nyumbani wikiendi hasa kama hana majukumu ya kimasomo wikiendi hiyo. Basi hicho kitendo

kikamfanya Irine na Queen wajue Yule ndiye Mwanume anayempa kiburi cha hela, na ndio maana hata kumsikia Calvin.

Unajua Lulu kwa namna alivyo huwezi kuamini kwamba hana mwanaume, Lulu ni wale mabinti waliolelewa kizungu tena haswa. Kwa hiyo kuanzia vaa yake ni ile ya mavazi ya kumchora na kumshika mwili, na kwa kuwa ana umbo zuri maungo yake yalioneckana namna yalivyo ya kuvutia na kupendeza. Halafu sasa Lulu anajipenda na anajua sana kucaa, na kwa kuwa hakosi chochote anachokitaka nyumbani kwao hivyo kila wakati ungemuona Lulu na nguo mpya na viatu vipyta na msuko mpya na simu mpya na harufu mpya. Hana maneno ya kihuni mdomoni lakini hakuna wimbo wa majuu wa R&B na Hiphop asioujua, kuanzia nyimbo za West Life, Boys 2 Men, Celine Dion, Jenipher Lopez, P Ordy, JayZ, na wengine wote maarufu asiojua. Lulu hakuwa mtu wa Imani kivile, Biblia yake yenyewe alikuwa anaikumbuka Jumapili hadi Jumapili, ama siku akiwa amekumbushwa na Mashauri juu ya kipindi kule Fellowship ya USCF Chapel. Na hii ndio sababu kubwa ya Irine na Queen kushindwa kuelewa kwamba ni kwa nini Lulu hataki kuambatana nao na hatimaye kuwa na Calvin.

Calvin na Hamidu walijaribu sana kujenga walau mazoea ya kawaida na Lulu ikashindikana kabisa. Tangu siku ile Lulu alipowashuhudia Irine na Hamidu wanakumbatiana na kubusiana darasani mbele za watu bila aibu wala uoga, Lulu alijua kuwa wale ni watu wasiojiheshimu. Na ndio mana hata wakati Calvin anajaribu kumuongelesha ile siku darasani aliamua kutokumpa ushirikiano. Miezi miwili sasa imepita wote wanashindwa

kujenga ukaribu na Lulu, pamoja na Lulu kufahamu kwamba Calvin ni mtoto wa Waziri wala hiyo haikunyesha kumbabaisha hata kidogo. Kwake aliona ni jambo la kawaida tu. Kihistoria Lulu hajawahi kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi na mvulana yejote, na wala bado hajui hata maana ya kupenda na kutoka kimapenzi na mtu. Huwa anashangaa anaposikia au kuona eti Msichana analia na wengine hata kufikia kunywa sumu kwa sababu ya mapenzi.

# 16

## WALOKOLE WAKUTANA

**S**iku moja mara baada ya Test ya Mathematical Engineering Mashauri alimwambia Manka “Wewe Mchaga, Mimi leo nimechoka sana kwakweli, nataka kubadilisha walau

mazingira!!”. “Ehehehehehehe, Engineer unataka kwenda Beach nini??!, Angalia usije kupotea Mtumishi!!” Manka alisema kwa utani. “Beach nikafanye nini mimi, kuna Mtumishi mmoja nataka nikamwone mahali!” Mashauri alijibu. “Wapi huko?!” Au kwa wifi mwenzangu maana hutaki kusema!” Manka alisisitiza. “Hamna bhana na wewe, nataka niende St Joseph University huko wanapaita Mbezi mwisho, nina rafiki yangu nilisoma nae Mzumbe anaitwa Mzava” Mashauri alitoa maelezo ya kueleweka sasa. “Eeh wewe, mbona na mimi nina rafiki yangu pale anaitwa Gwantwa, tenaanasoma Computer Science!” akaongezea kwa shauku “Umepanga uende mda gani? Sema mimi nina nguo chafu nyingi jamani, nilitaka nifue!” Manka alisisimka. “Kwani unataka kufua kwa muda gani??!!” Mashauri aliuliza. “2 hours very enough!” Manka alisema. Basi kwa kila mmoja anapenda kampani ya mwenzake, na baada ya mfululizo wa Test nyingi walikuwa wamechoka sana, hivyo walikubaliana baada ya masaa mawili wakutane ili waende kwa marafiki zao kule St Joseph.

Baada ya masaa mawili walianza safari yao kuelekea Mwenge kituo kikuu cha daladala, na walipofika Mwenge walipanda daladala kuelekea Mlandizi ila lengo lao ni washuke kituo kinachofuata Luguruni. Wote wawili walikuwa ni wageni sana kwenye Jiji la Dar es Salaam ila sasa walianza kulizoe Jiji. Wakiwa kwenye daladala mara Gafla Mashauri akaona majengo ya Chuo Kikuu cha St Joseph akapiga kelele “Wee Konda mbona unatupitisha tena jamani, nilikuambia Luguruni??!!”. Watu wengi kwenye ile daladala wakacheka sana. “Wee nani kakwambia hapa Luguruni wewe Mshamba??!” Konda alimjibu kwa dharau kidogo. “Mwanangu, Luguruni bado kidogo!” Mama mmoja

aliamua kumsaidia kwa maelekezo. “Haya Mwanangu sogea mbele maana mnakaribia kushuka” Yule Mama aliongea tena.

Waliposhuka kituoni kila mmoja alimkuta mwenyeji wake, Manka alimkuta Gwantwa, na Mashauri alimkuta Mzava. Cha ajabu sana Mzava alipomkuta Gwantwa kituoni akisema anamsubiri mgeni wake toka UD, na Mzava akamwambia na mimi ninamsubiri rafiki yangu kutoka UD pia. Hawakudhania kwamba wageni wanaowasubiri wangekuja na gari moja na eti kwamba wanafahamiana. Unajua Gwantwa na Mzava pia wanafahamiana vizuri sana na cha ajabu zaidi wamepangisha kwenye nyumba moja. Hii ilitokana na wote wawili kusali kwenye Fellowship inayoitwa TAFES, TAFES huwa na kawaida ya kuwapokea vizuri wanafunzi wa mwaka wa kwanza na kuwasaidia mambo mbalimbali ikiwemo kuwatafutiwa nyumba ambazo wataishi bila bughudha. Hivyo Mzava na Gwantwa walitafutiwa nyumba waliyopangisha na wanafunzi wanaosali pamoja wa TAFES. Lakini pia Mzava anayesoma Computer Engineering kuna baadhi ya vipindi vyta darasani wanasoma pamoja na Gwantwa anayesoma Computer Science.

Hivyo kitendo cha Mashauri kushuka kwenye gari moja na Manka kiliwashangaza sana, na cha ajabu Manka na Mashauri walionekana kufahamiana vizuri sana. Baada ya Manka kukumbatiana sana na Gwantwa, na Mashauri kukumbatiana na Mzava, Mzava Mpare mfupi sana mwenye maneno mengi ya Kiinjilisti akatania “Tuambieni enyi watu wa Mlimani mmeefahamianaje mpaka mkaja pamoja kiasi hiki”. “NI BWANA!” Mashauri akajibu kipendwa na kwa kifupi. Wote wanne kwa pamoja wakacheka sana na kufurahi pamoja.

Hivi ndivyo kufahamiana kwa hawa marafiki wanne walioshibana kulianza. Hii kwao ilikuwa siku kubwa sana, chakula chote kilipikiwa kwa Gwantwa, kilipoiva walikula na kunywa pamoja. Na baadae Mzava alishauri wapate muda wa kuomba mara baada ya hadithi nyingi za Mzumbe, Loleza, UDSM na St Joseph.

# 17

## BASH & BONANZA

**W**iki hii Chuoni kulikuwa na bashasha na shamrashamra sana, hii inatokana na Serikali ya wanafunzi DARUSO kutangaza kwamba ile WELCOME FIRST YEAR BASH ilikuwa imehairishwa zaidi ya mara moja itafanyika Ijumaa ya wiki hii. DARUSO ilikuwa inapitia skendo kubwa ya Ufujaji Fedha sana katika Uongozi huu unaoelekea kumaliza muda wake. Rais aliyekuwepo madarakani pamoja na mawaziri wake walikuwa wanashurutishwa na Bunge wajiuZulu, huu msuguano wa muda mrefu na vikao vyta hapa na pale ndio ulisababisha WELCOME FIRST YEAR ichelewe sana. Sio kawaida kwa tukio hili maalumu la kuwakaribisha mwaka wa kwanza kuchelewa

kiasi hiki, na kwa kuwa Rais na Mawaziri wake walinusurika kujiuzulu waliamua kuwapooza watu kwa kuwapa wanachostahili.

Kwanza Waliomba Uongozi wa Chuo kusitisha masomo kwa siku hii yote, kwa hiyo Ijumaa ilikuwa ni B&B WELCOME FIRST YEAR. B&B maana yake BONANZA & BASH, kwamba kuanzia asubuhi mpaka alasiri ingefanyika Bonanza na baadae jioni ndio hasa BASH ingeanza. Viongozi kupitia Waziri wa Michezo na Starehe Bashiri Mohamed almaarufu BaMo aliteua kamati ya Maandalizi ya B&B, na mionganivijana wa Mwaka wa kwanza waliokuwemo kwenye Kamati alikuwa Calvin na Queen. Na kamati ilidhamiria kuwaleta TWANGA PEPETA kama LIVE BAND, na Wasanii wa Bongo Flavour ambao ni O TEN, WANAUME TMK pamoja na Lady Jaydee. BASH ilipangwa kufanyika MAISHA BASEMENT iliyopo Mwenge alimaarufu siku hizi kama MAISHA CLUB. Na kama kawaida DJ KISHOKA ambaye anajua kuwarusha ipasavyo watu DISKO alikodishwa kuhakikisha siku hii inaenda sawa. Kamati iliamua Vyakula na Vinywaji havitakiwi kukatika Ukumbini hata kwa dakika moja. Kwa Matangazo haya kwenye POSTERS zilizobandikwa kila mahali Chuoni, jumlisha FREE TRANSPORTATION. Kilichokuwa kinachanganya kila mtu aliyekuwa na Interest za kuhudhuria ni nani atampa Kampani kwenye BASH, ila kuna kina Mr na Mrs Uhakika walitaka kujihakikishia Kampani kabla ya tukio lenyewe.

Na kwa kuwa TESTS 1 ndio kwanza zilikuwa zimemalizika, na BOOM la awamu ya pili kwa Semister hii ya kwanza nalo ndio lilikuwa limetoka. Vijana wa kiume na Mabinti

walionekana kuchanganyikiwa juu ya mambo mawili, moja ni KAMPANI, na mbili ni AINA YA MTOKO. Hiki ndicho kilichosababisha wiki hii ikawa na shamrashamra nyingi. Calvin pamoja na kuwa mwanakamati hiyo kubwa ya maandalizi, bado hakuwa na furaha kabisa kwa sababu ya Lulu. Kwa wiki mbili nzima alikuwa akijaribu kumuomba Lulu kwamba pamoja na amekataa kuwa nae, basi walau akubali kumpa kampani kwenye hiyo BASH ya aina yake.

Huku upande wa pili, wao UCSF walitangazia waumini wao kwamba mara baada ya BONANZA la michezo mchana, jioni kungekuwa na SEMINA maalumu ya LIFE ON CAMPUS itakayofundishwa na Mtumishi kutoka Arusha. Hivyo jamii nzima ya kina Mashauri, Manka, Atupele na wengineo wao hawakuwa hata na tone la mawazo kuhusu BASH maana sio kitu sawa kwa mujibu wa imani yao. Wao walitamani sana jioni ile ifike ili wakamsifu Mungu na kusikiliza Mafundisho yale Adimu kutoka kwa Mtumishi wa Mungu Engineer TT Mzava toka Arusha.

Kwa wiki mbili zote zile za Test 1 mawasiliano kati ya Lulu na Mashauri yalikuwa yamesuasua sana, kikawaida wanafunzi wa Engineering ni watu busy sana kutokana na nature ya masomo yao. Na wanapokuwa kwenye Test ndio kabisa kusahau hata kama wana simu za mkononi. Kila Lulu alipokuwa anajaribu kuandika “Masha” kwa sms, aliona zinapokelewaila hazijibowi kabisa. Aliandika sms kama hizo zaidi ya 10 bila majibu yoyote kutoka kwa Mashauri. Mwishowe aliamua kunyamaza kabisa, na kwa kuwa wiki hizo mbili hakuhudhuria kabisa Fellowship kule CHAPEL. Baada ya Lulu kuona Mashauri hajibu kabisa sms zake kuna kitu akawa amekumbuka, Ijumaa ya wiki

moja iliyopita wakati akiwa amekuja kuchukuliwa na Baba yake Mdogo Mbezi Beach. Akiwa njiani maeneo ya Survey unapotoka Chuoni aliwaona Mashauri na Manka wakiwa wanapanda daladala pamoja inayoelekea Mwenge. Kwa akili za haraka haraka Lulu aliamini pengine Mashauri na Manka waliamua kuwa wapenzi maana walifanana kwa mengi, na hiki kimya cha Mashauri ni makubaliano yao na Manka kwamba Mashauri akae kabisa mbali na Lulu. Hii ilimuumiza Lulu japo kiuhalisia alikuwa hafahamu sana ni kwa nini alikuwa anaumwa ili hali Mashauri ni kijana tu walikutana na wakazoeana ile kawaida.

Hatimaye siku ya B&B WELCOME FIRST YEAR ilifika, hii ilikuwa Ijumaa yenye shamrashamra nyingi sana, Wanafunzi wote Chuoni walikuwa wakijipanga kwa michezo mbalimbali kulingana na vitivo, madarasa na miaka ya masomo yao sawasawa na utaratibu wa Mashindano ulivyopangwa. Kila aina ya michezo ilichezwa, kuanzia kukimbia, kuruka juu na chini, kurusha tufe, mipira ya aina mbalimbali kuanzia mpira wa miguu, mikono, wavu, pete na wa mezani. Kelele za furaha zilisikika za kushangilia toka viwanja mbalimbali vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hakika ilikuwa furaha isiyokuwa ya kifani.

Hatimaye alasiri Bonanza lilihitishwa na Washindi walitunukiwa zawadi na vyeti mbalimbali. Na Waziri wa Michezo na Starehe alitangaza USAFIRI WA BURE utakuwepo kuanzia saa 2 usiku kwenye vitivo mbalimbali tayari kwa BASH la aina yake usiku huo.

Lulu kwa kuwa naye alikuwa kwenye Bonanza alisikia lile Tangazo, na gafla akatamani moyoni mwake aende walau aone

yanayojiri kwenye hilo BASH. Aliporudi Chumbani Hosteli akawakuta Irine na Queen wanabishana juu ya namna watatokezea kwenye mtoko ule wa usiku wa aina yake, walipomuona anaingia wakanyamaza gafla. “Shosti, twende wote basi kwenye BASH mpenzii!!” Queen alizungumza kwa upole huku akimsogelea Lulu. “Mwenzangu natamanije, japo usalama ndio nahofia jamani!” Lulu alisema kwa maringo kidogo huku akionyesha kualainika. “Usijali Mpenzi, Mimi ndio Mwanakamati so nitakuwa sehemu nzuri utakuwa salama na utainjoy sana!!” Queen alisema kwa ujasiri na msisitizo.

Baada ya nusu saa walionekana wote watatu wakichagua namna ya kuva. Kwanza waliamua wote watatu wavae min-sketi na vitop japo rangi tofauti tofauti, halafu chini wavalie high heels yaani viatu vyenye visigino virefu. Lulu yeche kwa kuwa ni mweupe sana na umbo pana la kati na urefu wa haja, alivalia min-sketi nyeusi na top nzuri ya pink, Queen alivalia min-sket ya chocolate na top ya purple, halafu Irine kwa sababu ya weusi wake wa kuteleza alivalia min-sket nyeupe na top nyekundu.

“Wewe boyo niandalie Elfu 50 chaap, Mtoto ameingia line huku” Queen alimtext Calvin chaap. “Acha Masihara bhana, Una uhakika!!! wewe mpenda hela?” Calvin alijibu. “Hutaki Acha, nimwambia abaki!” Queen alimjibu Calvin. “Natania Mama, 50 yako umepata!” Calvin aliamua kuwa mpole.

Hatimaye saa mbili na nusu ya usiku Warembo watatu wa maana walionekana wakiingia kwenye gari Rav 4 ya Calvin ambayo wakati huo ilikuwa ikiendeshwa na Hamidu. Calvin baada ya kuambiwa Lulu anaenda BASH akamwambia Hamidu awafate

na gari ili wasipande magari ya wanafunzi wote ambayo ni daladala walizokodishiwa na Kamati. Hamidu aliye kuwa ameketi na Irene mbele huku akiendesha gari hakuamini kwamba ni Lulu kweli yupo kwenye gari yao, kila wakati alidhani kwamba anaota. Yaani ndege aliye wasumbua kumwinda kwa siku zote hizo hatimaye ameingia mtegoni mwenyewe bila hata usumbufu. Gari aina ya Rav 4 ilionekana kupita maeneo ya Mwenge Stendi kwa kasi na baada ya dakika mbili ilifika maeneo ya ITV na kukata kulia, liliingia maeneo ya MAISHA BASEMENT CLUB, eneo ndio hasa UNIVERSITY BASH WELCOME FIRST YEAR ilikuwa inafanyika. Nje ya MAISHA BASEMENT alione kana kijana mfupi, mweupe na mnene aliye valia maridadi sana kama Mbunge akilisimamisha lile gari. Ni Calvin John Sanga, Mtoto wa Waziri wa Nishati na Madini Brigedia Jenerali John Sanga. Wakati huu akiwa moja ya Wanakati ya Maandalizi ya Tukio hili la aina yake. “Welcome Queen, you look so amaizing, gorgeous and wonderful like Angels!” Alisema Calvin wakati akiwafungulia mlango Lulu na Queen waliokuwa wamekaa siti za nyuma za gari. “And guess what??!” You are the VVIP!” aliongezea Calvin akiwajulisha kwamba amewa andalia nafasi sehemu ya wageni rasmi na wa heshima. Kila wakati alikuwa akimu angalia Lulu kwa Uchu sana, aliangalia namna yale mavazi yalivyokuwa yameshika sehemu mbalimbali za Mwili wa Lulu, kuna wakati alipoteza network mpaka akawa anaongea vitu havieleweki.

Majira ya saa nne za usiku BASH ilianza Rasmi, TWANGA PEPETA ndio waliliamsha kwa nyimbo za kusisimua vijana. Ukumbi ulifurika vijana wa Chuo maelfu, Mabinti wengi

walivalia nusu uchi, huku wengine wakiwa wamebanwa kweli kweli. Yalionekana makundi makubwa ya aina tatu, wale walionekana ni wapenzi walikuwa wakikumbatiana na kubusiana kila muda, pili walionekana wale waliokuwa bado wanabembelezana kwa maana bado walikuwa hawajakubaliana kupeana kampani usiku huu, na mwisho ni wale wasiojali sana mara wacheze na wavulana wenzao ama na wasichana wenzao na muda mwengineacheze na msichana huyu na baada huyu ilimradi kufurahia BASH.

Ukumbi ulikuwa na taa za rangi mbalimbali zinazowaka katika namna ya kuvutia sana vijana yaani kuwaka na kuzima. Wakati LADY JAYDEE anaimba moja kati ya nyimbo zake nzuri za mapenzi, Lulu alionekana kuvutiwa sana na ule wimbo akaanza kujitingisha tingisha japo kiogakioga huku ameshika glass yake aliyochanganya RED BULL na Soda ya Sprite.

Kwa namna maumbile ya Lulu yalivyo Calvin akashindwa kujizua japo alikuwa hajalewa bado maana ndio kwanza alikuwa amemaliza Kilimanjaro moja, akamsogelea Lulu na akauzungusha mkono wake kwenye kiuno cha Lulu ambaye wakati huo kwa kuwa alikuwa ameketi kwenye kiti kirefu, ile top aliyokuwa amevaa alikuwa imeachana na sketi na hivyo ikaacha sehemu ya kiuno chake wazi. Alisikia kitu cha baridi sana kimemshika kiuno chake, kabla hajakaa vizuri Calvin alisimama mbele yake na kumbusu mdomoni, “Please Lulu don’t kill Me” alisema Calvin, “What!! Are you Mad!!” kwa hasira na ukali wa hali ya juu huku akimtoa Calvin kwa nguvu. “Lulu jamani mbona hivyo, msikilize mwenzako jamani!” Irine aliyekuwa amekumbatiwa mno na Hamidu huku wakicheza na kunyweshana mvinyo alimuomba

Lulu. “C’mon, I’m not this kind of girl, Am here to enjoy AND not for men!!!” Alisema Lulu huku akishuka kwenye kitu na kusimama kwa shari, wakati huu Calvin alikuwa chini kapiga magoti huku anasema “Baby, atleast for today ..... atleast you dance with me..... please please”. “Lulu sio sawa unavyofanya ujue, mbona Usekondari haukutoki wewe” Alisema Queen kwa hasira sana. Lulu alipogundua wote wanampigia debe Calvin, akawaambia kwa upole maana wote walionekana kulewa “I am very sorry guys, We didn’t agree on this! Calvin Am sorry!!” Halafu akamnyanya Calvin pale chini, akamnong’oneza sikioni “Worry out, tulia tutaongea!” Halafu akanyanyaaka akeleke Washroom akiwa peke yake.

“Dadangu Lulu, Uko wapi mbona sikuoni Fellowship Seminar Mtumishi wa Mungu?!” Hii ni sms ya kwanza Lulu kuikuta kwenye simu iliyokuwa imetoka kwa Mashauri tangu saa nne na nusu usiku huu. “Lulu, unaogopa kutoka mwenyewe Hosteli niye na Manka kukuchukua, hii semina ni muhimu sana kwetu!” Kucheki ivi ni sms ya pili kutoka kwa Mashauri akitaka kumfuata Hosteli. “Mbona hunijibu jamani, soon tutaanza kuhudumu na sitaweza tena kukujibu Dadangu!” Sms ya tatu kutoka kwa Mashauri. “Dada Lulu ujue mimi ni mgeni wa kutumia simu, kumbe niliweka namba yako blacklist bila kujua, so sikuwa naona sms zako kabisa, sijakusudia kutokukujibu. Nijibu tafadhali!!” sms ya nne kutoka kwa Mashauri. Lulu akiwa Msalani alijisikia kuchanganyikiwa, alijihisi mkosaji sana maana alimfikiria Mashauri vibaya. Na zaidi alijiona mpumbavu kwa kuja huku BASH na kukutana na swahibu ya Calvin. Alipoangalia saa aligundua ni tayari saa 6 na nusu usiku, alijiuliza ajibu mda

huu au aache. Alipofikiri kurudi ukumbini akaona ni hatari zaidi maana watu wameanza kulewa na kutojielewa kabisa, alipokumbuka namna ambavyo Calvin alimshika kiuno chake na kumbusu usoni, alijisikia vibaya sana alitamani anawe hata uso. Mwishowe akasema itakavyokuwa na iwe “Masha najuta sana, nipo huku BASH Mkisha Basement. Tafadhalii najua upo Semina Mkeshani, naomba fanya unaloweza njoo nichukue sasa hivi na tax, NITALIPA GHARAMA ZOTE!” aliandika sms kwa kujikaza sana maana alijiona mkosaji sana. “Yesu Wangu!” Alitamka Mashauri akiwa karibu na Atupele. “Nini Mtumishi?!” Atupele aliuliza. “Lulu yupo DISCO kule BASH, na anasema yupo hatarini nimfate nikamchukue!!” Alijibu Mashauri. Hebu mchukue Manka twendeni mara moja!” Atupele aliagiza, kikawaida Atupele ni mtu wa kazi huwa hataki maneno mengi. Baada ya dakika 20 Tax ikiwa na Manka, Atupele na Mashauri ilipaki mbele ya CLUB ya MAISHA BASEMENT. Kasha Lulu aliyekuwa amevelia nusu uchi akatokea mlango wa nyuma kwa aibu akazunguka mbele akawahi akaingia garini, Manka alikuwa na mtandio akampa akajifunga, huku chini walau kujisitiri. Gari ikaanza kurudi tena Chuoni. “Ahsante YESU Uuuuuh!” Alisikika Mashauri huku akishusha pumnzi kwa nguvu.

“Huyu Mshamba mbona harudi jamani??!!” Aliuliza Hamidu ambaye ndio kwanza alikuwa amelewa chakari. “Lulu wangu jamani, mbona harudiiii????!!” Calvin aliuliza kwa huruma. Queen akamsogelea kwa karibu sana Calvin halafu akamwambia “Niangalie vizuri kuanzia juu hadi chini! Nakufaa au Sikufaii??!!” Calvin kwa kuwa alikuwa ameleta sana akajikuta amemkumbatia Queen kwa nguvu na mara wakaanza kunyonyana ndimi.

Asubuhi ya Jumamosi kama saa tano hivi, Sinza Mapambano nyumbani kwa Calvin, Hamidu alikuwa amelala na Irine chumbani kwa Hamidu, na Calvin alijikuta amelala na Queen chumbani kwake. Na wote hawaku jua lolote lililotokea jana kwa Lulu.

# 18

## SIKU KUU!!

“ Mbona umevaa hivyo unaenda wapi Wewe?!!” Halafu ni nini kutufanya wenzio wajinga kutuacha solemba?!!” Queen alimuuliza Lulu aliyeonekana kuvalia nguo yake ndefu sketi na blaazi za kitenge iliyoshonwa vizuri sana. “Jamani eeh mbona kuulizana hivyo! anyway naenda zangu Ibada Chapel. Na kuhusu BASH niliondoka maana sio mazingira niliyoyazoea, na wote nyie mlishalewa!” Lulu alijibu kistaarabu sana. “Halo haloo halooo!!!” Queen na Irine waliangua vicheko vile vya kishambenga halafu wakagonga, kisha Irine akasema “Aya Church Girl, Ibada njema. Tena ukatubu maana juzi ulikuwa BASH mmh swiiiii!” akamalizia kwa kusonya. Lulu hakutaka maneno zaidi akatoka zake nje na Biblia na Notebook yake mkononi.

“Kaka Masha ndio napanda Chapel!” Lulu alimtumia sms Mashauri. “Karibu sana Dadangu, Mimi nilishafika karibu Ibada itaanza. Mashauri alijisikia vizuri sana juu ya muelekeo mzuri wa kiimani alioanza kuuonyesha Lulu, ikiwa ni siku moja tu baada ya ye ye na rafiki zake kwenda kumchukua kule MAISHA BASEMENT kwenye BASH. “Ahsante Yesu!” Alisikika Mashauri baada ya ile tafakari. USCF-CCT Chapel ilioneckana kujaa sana leo kuliko kawaida, hii ni kwa sababu ya Semina nzuri

aliyokuwa ndio kwanza inamalizika inayoongozwa na Engineer TT Mzava. UCSF Praize Team ilikuwa imeshaanza kuhudumu ikiwaongoza watu katika KUSIFU na KUABUDU. Wakati huu kama kawaida First Year ndio walikuwa walengwa wakubwa wa Semina ya LIFE ON CAMPUS, walipewa kipaumbele kuongoza KUSIFU na KUABUDU. Kulikuwa na Utulivu wa aina yake Nyumbani mwa BWANA hii siku, Lulu alikuwa ametulia kimya akiwa amesimama na kunyoosha mikono yake juu. Mara ikasikika Sauti ya Manka,

**“Nigusee, Nigusee Roho wa BWANA Nigusee ×2  
Jana Imepita na Leo Nakuhitajiiii  
Roho wa BWANA Nigusee!”**

Kanisa lilipokelea wimbo huu kwa sauti, kila mmoja akitamani Roho wa BWANA amguse. Lulu alijikuta anasema maneno machache tu tena matatu “Roho wa BWANA Niguse!”. Manka aliendelea kuuimbisha ule wimbo kwa kuzama zaidi uweponi. Sasa ilisikika sauti ya vyombo tu vilivyopigwa kwa ustadi sana na kwa utaratibu, watu walisikika wakibubujika nyumbani mwa BWANA. Wakati huu Mashauri alipewa kipaza sauti na Manka, Mashauri kabla ya kuimba akasema “Nisikilizeni Watoto wa Mungu, Twende tukamwambie Mungu ATUGUSE TENA” Baada ya kusema Maneno hayo wa kuwatayarisha watu Mashauri akaanza kuimba kwa upole na utaratibu sana

**“Niguse Tena, Niguse Tena, Ninaomba BABA,  
Uniguse Tena, Niguseeee!!!!”**

Kanisa sasa liliomba na kuimba kwa sauti sana, Lulu alianza kuona utofauti na kuufurahia sana Uwepo wa Mungu uliokuwa umetamalaki na kulijaza Hekalu. Alijikuta amepiga magoti huku machozi mengi yakimtoka machoni, Lulu akasema “Mungu mimi sikufahamu vizuri, nimekuwa nikisikia tu Habari zako, tafadhali Niguse na Mimi Ninaomba!” Mara Mwalimu wa ile Semina Engineer TT Mzava alipokea kipaza sauti, akaonyesha ishara ya kwamba mziki usipigwe tena na pawe kimya kabisa, kisha akasema “WANANGU, Maisha ya Vijana Wengi pamoja na Malengo yao makubwa huharibiwa vibaya sana hapa Chuoni!” akaendelea “Miaka mingi iliyopita nilisoma hapa Mechanical Engineering kwa miaka mnne, na niliona FUTURE na HATIMA za wengi zikiharibiwa vibaya hasa wale ambao hawakuamua kutembea na Mungu na wakazitegemea akili zao.” Akanyamaza kidogo kisha akasema ‘‘Ni heri uonekane MSHAMBA, narudia Ni heri uonekane MSHAMBA lakini ukachora mstari na zaidi ukasimama na miguu yako!’’ Yale maneno yaliingia moyoni mwa Lulu kama mkuki na yakaanza kujirudia “Chora Mstari, Simama kwa Miguu yako!!!”. Mtumishi wa Mungu akaruhusu watu wakae, na kisha akasema “Leo tunapomalizia Semina yetu tulioanza na Mkesha nitafundisha kitu kidogo sana chini ya kichwa kisemacho **“USALAMA NA UHAKIKA WA MAISHA YAKO UMEFICHWA NDANI YA KRISTO”**. Mtumishi wa Mungu alifundisha kwa muda mfupi sana na kwa kina, wakati wote huu Lulu na vijana wengine walikuwa wakimsikiliza na kuandika. Moja kati ya maneno yaliyoingia moyoni mwa Lulu ni “Mtu anapookoka na kumpokea Kristo, Uhai, Usalama na Uhakika wa Maisha ya huyu mtu unakuwa ndani ya Kristo” kisha Lulu akakumbuka tena alichosema Mtumishi kwamba “Wewe ni

kama mboni ya JICHO LA MUNGU, amekuchora katika VITANGA VYA MIKONO yake, na tena anakutambalia kama vile kuku akumbatiavyo vifaranga vyake!”

Baada ya Mtumishi kumaliza kufundisha akasema “Ninasikia Wimbo wa TENZI ndani yangu, Praise Team mtanisaidia na tuimbe pamoja!” Mashauri akashika kipaza sauti, Na akaaongoza watu kuimba

**“Tufani inapovuma Sana Moyoni mwangu,  
Huona pakujificha Mkononi mwa Mungu.  
Hunificha, hunificha Adui hatanipata,  
Hunificha, hunificha Mkononi mwake.  
Adui wakiniudhi Nami nikisumbuka,  
Mungu atavigeuza Vyote viwe Baraka”**

Kila walipofika kwenye kibwagizo cha Hunificha, Lulu alilia kwa sauti sana na kwikwi. Alijisikia kumhitaji sana Mungu. Mashauri akaendelea kuongoza ule ubeti wanne.

**“Niishipo duniani Ni tufani daima,  
Anilindapo rohoni Nitakaa salama.  
Hunificha, hunificha Adui hatanipata,  
Hunificha, hunificha Mkononi mwake.**

Baada ya kumaliza Wimbo huu, Mtumishi wa Mungu akaita Watu ambao wangependa kumpa Yesu Maisha yao wakimbie mara moja mbele. Lulu alikuwa wa kwanza kukimbia haraka sana na mamia ya wanafunzi waliungana nae kwenda mbele ili kumpokea

Yesu awe BWANA na MWOKOZI wa maisha yao. Wakati huu Manka alianza kuimba

**“Karibu Yesu Maishani mwangu  
Karibu Yesu Maishani mwangu!”**

Kisha Chaplain Mchungaji Leon Chizza akawaongoza sala maalum ya kumpokea Yesu. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa maisha ya kiroho ya Lulu, Ijumaa alionekana BASH Maisha Basement halafu Jumapili anaonekana CHAPEL akiwa mionganini mwa wanafunzi waliookoka.

# 19

## KASHI KASHI DARASANI

**I**likuwa ni siku tulivu kwa Darasa la Mwaka wa kwanza Sheria, Dr Kimaro alikuwa anafundisha BUSINESS LAW kwenye kipengele cha LAW OF CONTRACTS. Kama kawaida yake ni Mwalimu machachari sana na anayejua mno, kila wakati alikuwa akiangalia sana upande aliokaa Lulu. Ikafikia mahali akauliza darasa kitu Fulani halafu akasema “I have full authority to choose randomly!!” wakati huo akipandisha pandisha suruali yake na kushusha kidogo miwani kama mtu anayechungulia kwa kuibia. “Hey, Lady with a Black tshirt written ‘Awesome God’ please tell us”, Alieleza Dr Kimaro akimaanisha Lulu. Lulu Stephen Mollel alisimama kwa ujasiri mkubwa na kuanza “First and Foremost as far as the Law of contract is concerned, the answer is NO, this is because.....” akaendelea kutoa ung’eng’e wa kina ambao sio darasa tu lilitaharuki, bali hata Dr Kimaro mwenyewe aligundua huyu binti sio amejaliwa tu uzuri wa rangi, umbo bali na akili,. Please Honorable Madam Judge have your seat please”, Alisema Dr Kimaro kwa bashasha kama kawaida yake. Halafu akamuuliza Lulu tena “What is you name again??!”, “Lulu Stephen Mollel” alijibu Lulu. Kitendo cha Dr Kimaro kumsifia vile Lulu tena mbele ya darasa kiliwahudhi sana

Queen na Irine na baadhi ya Wadada mle darasani. “CR please submit Assigments to my office right now!” Alisema Dr Kimaro baada ya kumaliza kipindi na kutoka darasani.

“Duuuh jamani Yule Demu noma kishenzi” alisikika mvulana mmoja akiwa anawaambia wenzake. “Mwanangu mboga saba Yule, amezaliwa nacho ati!” mwengine akaongezea, “Mademu wengine sio hata wa kuwafata utaishia aibu tu!” alisema jamaa mwengine, kisha Yule wa kwanza akajazia “Mali za wakubwa zile”. Yaani ghafla habari kuu kwenye lile darasa likawa Lulu na namna alivyoachilia majibu yaliyoshiba kwa Dr Kimaro.

Baada ya CR kukusanya zile Assignments na kumpelekea Dr Kimaro ofisini kwake, “CR call for me Lulu Stephen Mollel” aliagiza Dr Kimaro. “Sawa Sir” alijibu CR, “Don’t call Sir, say Dr!” alimkosoa Dr Kimaro. “Sorry Dr!” alisema CR, “Absolutely Right!” akasema Dr Kimaro.

“Beautiful Bright Girl, welcome to my office Awesome Masai!” hayo yalikuwa maneno mengi ya Dr Kimaro akimkaribisha Lulu ofisini kwake. Baada ya Lulu kuketi akasema “Here I am Dr”, “I can see, tell me your dream!” Dr Kimaro akauliza kwa bashasha. “Standing for Human Rights in United Nation!” alijibu kwa kifupi kinachoelewaka sana kwetu wanasemagga “Short and Clear!”. Basi Dr Kimaro akaendelea kumdodosa na maswali mengi sana na kisha akamuuliza “Do you have boyfriend?!” “That is very personal Dr!” Lulu alimjibu Dr Kimaro kwa ujasiri. “Anyway Lulu, you better be very careful!” Dr Kimaro akamtahadharisha Lulu. “I do, thanks Dr!!” Lulu akashukuru. Kisha Dr Kimaro akamwambia Lulu angependa

kumsaidia na kumshauri ili afikie ndoto zake, hivyo akachukua namba za simu za Lulu ili kurahisisha mawasiliano. Lulu alitoka kwenye hii ofisi akiwa na wasiwasi sana, na hii ni kutokana na namna Dr Kimaro alikuwa akimuangalia kwa macho yanayoonyesha kwa udhahiri yamejaa uchu na tamaa mbaya. Na hasa wakichukuliana kwamba katikati ya maongezi Dr Kimaro alimuagiza Lulu amtolee kitabu Fulani kwenye moja ya Shelf zilizopo pale ofisini kwake, ambayo Lulu aligundua ni mbinu ya Dr kumuona yeze vizuri namna alivyoumbika maeneo yake ya nyuma. Lulu alitoka kwenye ofisi ya Dr Kimaro huku taa nyekundu ikawaka moyoni mwake. Wakati anatoka mlangoni akashangaa anapishana na Queen mlangoni, “Mmh swiii!” Queen alimsonya Lulu kwa dharau. Kumbe wakati Lulu anapewa ule ujumbe na CR kwamba anahitajika ofisini kwa Dr Kimaro, Queen alisikia na kwa wivu aliona akaamua kumfuatilia kwa nyuma. Kwa hiyo Muda wote Lulu akiwa ofisini kwa Dr Kimaro, Queen alikuwa akimsibiru tu kwa nje. Na alipotoka ndio akaamua na yeze aingie. Queen huwa anaamini siku zote WANAUME NI WADHAIFU sana kwa wanawake wazuri kama yeze. Siku hii aliamua kumuonyesha Lulu kwamba yeze ni zaidi yake, na ndio maana alipotoka tu na yeze akaingia. Huwezi kuamini kwamba Dr Kimaro hakuwahi kujua kwenye lile darasa kuna binti mwenye muonekano kama wa Queen. Queen alikuwa mrefu wa haja, sio mweupe sio mweusi, sio mnene sio mwembamba, hipsi zinazoonekana bila kutafuta, aliyejazia nyuma kwa mpangilio maalumu. Mwenye kiuno chembamba na kifua kilichopangika vema, ukimuangalia usoni usingetumia nguvu kubwa kuona sura nzuri na mashavu yaliyobonyea kulia na kushoto kwa dimpozi. Na hatari zaidi alikuwa anajua kuvaan guuo za mitego kila wakati

ambazo zilikuwa zinaweka wazi uzuri aliokuwa nao. “Are you a Law student??!” aliuliza Dr Kimaro kwa mshangao huku akishangaa ugeni huo wa ghafla wa mrembo ambaye anaamini hajawahi kumuona. “Why NOT” alijibu Queen huku akikaa kwenye kitu bila kumbiwa akae, halafu akakisogeza nyuma kidogo kuhakikisha Dr Kimaro anamuona vizuri. Queen aliyejkuwa amevalia min-skirt nyeusi iliyomkamata vizuri mwili wake na kuacha sehemu kubwa ya miguu yake wazi, na juu alivalia top ya rangi nyeupe aliyombana kifua chake vema na kuonyesha namna asivyo hata na tone ya kitambi. Dr Kimaro aliyeanza kuchanganyikiwa na ule ugeni wa ghafla wa mrembo wa ajabu, alianza kulamba midomo yake huku akiwa na uhakika wa anachokiona. “Which year are You?!” aliuliza Dr Kimaro ambaye wakati huu alikuwa haelewi tena hata aongee nini. “First Year, Am called Queen, I need your help Amaizing Doctor” alisema Queen kwa kujiamini huku akikisukuma kitu cha matairi alichokalia mbele na nyuma. “Which help Beauty Girl??!!” Dr Kimaro akajiongeza, “Your knowledge” alijibu Queen kwa kifupi. Kisha akasimama akampa Dr Kimaro mgongo kwa muda na kisha akamgeukia tena, akalamba midomo yake yenye lipsi pana za kuvutia halafu akamwambia “I have your offer before you say YES Dr!” alisema Queen kabla Dr Kimaro hajajibu chochote. Na baada ya hapo akanyoosha mikono yake kama ishara Dr njoo nikumbatie, Dr Kimaro aliyejkuwa bado amepigwa na butwaa kwa tukio hili la kushtukiza alijikuta ananyanyuka kwenye kitu na kumfuata Queen alipo. Queen akamkumbatia Dr Kimaro kwa nguvu huku akilegeza mwili wake ili Dr aushikilie vizuri, halafu kwa suti ya kimahaba ya kunong’oneza akamwabia “Anytime today, any hotel of your choice, let me know!” halafu akambusu

akamwachia, akaandika namba zake kwenye karatasi juu ya meza ya Dr Kimaro akatoka nje.

# 20

## 006 MAFIAN GANG

**B**arabara ya Bagamoyo katika eneo la Mapinga unapoingia ndani zaidi kwenye kijiji cha Kibosha msituni, anaonekana Chacha Marwa, huyu ni pande la mtu la miraba mnne lililojazia kifua na lenye misuli ya haja. Ukimuangalia kwa haraka unaweza kutambua kwamba kofi lake moja tu likikupata unaweza ukaona nyota nyota za ahera

madukani. Chacha ni mwanajeshi aliyehasi jeshini baada ya kufukuzwa aliamua kuanzisha kundi lake la 006 MAFIAN GANG ambalo limekuwa likifanya shughuli za ujambazi, utesaji, utekaji na uuaji. Chini ya Chacha Marwa ama Captain kama wenzake wanavyomuita ana vijana kumi na tatu ambaye kila mmoja ni mahiri katika eneo flani kulingana na kazi wanazozifanya. Pamoja na umahiri wa mtu kwenye eneo flani bado ilimlazimu kila mmoja kupata mafunzo maalumu ya kijeshi ya kujilinda na kupambana, ambayo Chacha mwenyewe au Captain anayaita D&O TACTIC. D&O TACTIC hutolewa kwa siku 90 mfululizo na baada ya hapo mtu amehesabiwa kukamilika kwenye kikosi cha 006 MAFIAN GANG.

Kwenye kundi la 006 MAFIAN GANG kuna watu mahiri kuanzia kwenye kuua kwa silaha yaani wale wadunguaji makini (Snipers), madereve wanaoendesha magari kaasi mno, wataalamu wa kuvunja milango na mageti bila nguvu nyingi, wataalamu wa teknolojia ya Computer, wapelelezi hatari, wataalamu wa kutapeli na kubadili sauti, wachora ramani na mishe nzima na wapigaji na waliobobea kwenye utesaji. Kwenye mafunzo ya D&O TACTIC mtu hufundishwa jinsi ya kujilinda na kupambana kijeshi, miezi hii mitatu huwa miezi migumu sana kwa vijana wanaoandaliwa kujiunga rasmi na 006 MAFIAN GANG. Kila anayejunga kwenye kundi hili licha ya kufundishwa Utii kwa kiongozi wao, kutokukubali kutoa siri unapokamatwa hata wakikuua, zaidi Chacha huwaambia jambo moja “Mnadhani kwa nini kuna namba 6 kwenye jina letu?!!” “Namba 6 means MAN WITHOUT GOD COMPLETELY yaani MTU ASIYE NA MUNGU KABISA, so

hana hamna Imani, hamna Haki wala hamna Huruma hapa ni KAZI TU!”

Kundi hili limekuwa likiwalipa watu wake mishahara na marupurupu mazuri sana, yanayowafanya waishi maisha bora sana na familia zao. Hii ni kutokana na matajiri wengi wanaofanya biashara za magendo kulitumia kundi hili kwenye Nyendo zao na kuwalipa fedha nyingi sana. Hata na hivyo leo Captain Chacha Marwa anaonekana amekuja na ishu kubwa zaidi. Wakiwa wamekaa kwenye mduara wa meza zao huku wakipata huduma ya Nyama choma ya Pofu na Mvinyo, Chacha alionekana kuwa na umakini ambao haujawahi kutokea kabla “Mafiani, we have HEAVY DEAL but so TOUGH!” Chacha alisema huku akipiga fundo moja la Whisky. “Mr Kobre ana madai yake ya 2 billions kwa Mhindi wa Kariakoo, na anasema ni miaka miwili sasa Mhindi anamzungusha. Ametupa dili la kuhakikisha analipwa in 5 days!” Aliendelea Chacha huku akiwatazama vijana wake machoni namna wanavyopokea dili hili. “Mr Kobre kaniambia ye ye hatupangii la kufanya ILA anachotaka ni alipwe pesa yake ndani ya siku tano!” alimalizia Chacha. Baada ya kumaliza moja ya vijana wake hatari Carlos Chota akauliza kwa bashasha “Payment!!!” “20%” Akajibu Chacha. Kila mtu akilini mwake akafanya mahesabu juu ya asilimia 20 ya bilioni 2 akajua ni milioni 200. Kwa haraka haraka wakapanga mikakati na mbinu za kufanya kuhakikisha Mr Kobre analipwa fedha zake na Mhindi wa Kariakoo.

Kwanza akatumwa mpelelezi na mchora ramani hatari Jimmy “The INVISIBLE” kwenda Kariakoo kupeleleza nyendo za Mhindi na familia yake, kisha achore ramani na misheni nzima

itakavokuwa. Jimmy “The INVISIBLE” kama anavyojiita ni mtaalamu wa mambo ya INTELLIGENCIA and TRACKING, Yeye sio mzuri wa kwenda FRONT kwenye tukio ila anaweza kupeleleza na akasoma ramani na kisha kutoa ramani na mkakati wa kila kitu. Chacha alimtaka Jimmy “The INVISIBLE” kutumia siku moja yaani kesho yake. Kwa hiyo chchote kisifanyike mpaka Jimmy amemaliza kazi yake.

Asubuhi ya kesho yake alionekana kichaa mpya kwenye Mtaa wa Congo pale Kariakoo. Kichaa huyu alionekana kuchafuka vumbi miguuni kama aliyetoka mkoani, lakini zaidi alikuwa na mfuko wa salfeti wenye vitabu na makaratasi kibao. Kila alipokaa mahali alichukua baadhi ya vitabu na makaratasi na kuwa bize sana kuyasoma, na wakati mwengine kuandika vitu visivyo eleweka. Pamoja na kuzurura huku na kule, mara nyingi akiongea mwenyewe lakini kila baada ya dakika kumi kupita alipita mbele ya duka kubwa la Mhindi na kukaa chini karibu na mlango halafu akawaanasoma mavitabu yake na kuandika andika vitu visivyo eleweka. Wakati flani mchana akapotea kabisa hasa mida ambayo Mhindi hufunga duka kwa ajili ya Lunch. Majira kama ya saa tisa alasiri akaonekana maeneo ya jirani na kwa Mhindi ila kwa upande mwengine amekaa halafu anasoma mavitabu kutoka kwenye gunia lake na kuandika kwa utulivu sana. Kama saa kumi na moja karibu na Mhindi kuanza maandalizi ya kufunga, akatokea mtu mmoja ambaye alionekana kama anataka kumnyang’anya yule kichaa moja ya vitabu vyake. Mara kichaa akiwa na fuko lake akaanza kumkimbia yule jamaa, yule jamaa akakimbia mpaka dukani kwa Mhindi na kichaa naye akaingia mpaka dukani. Yule jamaa akatoka, na kichaa akatoka

nae anamkimbiza tu bado baada ya muda kichaa hakuonekana tena.

Jimmy “The INVISIBLE” asiyeonekana kama lilivyo jina lake alikuwa ameshamaliza kazi yake ndani ya siku moja, kwa muda aliojifanya kichaa alishajua mtoto wa Mhindi anasoma wapi, anachukuliwa na gari gani na saa ngapi. Lakini pia alishajua kwamba mke wa Mhindi hutoka na kutembea tembea kunyoosha miguu saa ngapi na maeneo gani. Aliandika na kuchora taarifa zote muhimu na mwisho akaandika KAZI KWENU, AM DONE. Chacha Captain akateua kikosi cha kazi na kesho yake kazi ilianza.

Mhindi alishangaa ameona gari la shule likimshusha mtoto na likaondoka ila ghafla haoni mtoto akiingia ndani. Na kwa kuwa alikuwa na wateja wengi akahisi labda mtoto wake ameingia ila pengine hajamuona hivyo akapotezea. Kwa kuwa mtoto wake hurudi saa 10 na mkewe huanza mazoezi ya kutembea saa 11 ili apunguze uzito pamoja na miguu kuvimba, wakati ye ye Mhindi hufunga duka saa 12. Hivyo ilipofika saa 11 bado hamuoni kijana wake akajua labda leo ameamua kutoka na mama kutembea tembea.

Saa 12 mpaka anafunga duka sio mtoto wala mama aliyekuwa anaonekana, kuulizia wafanyakazi wake wakamwambia hata kijana wake wa shule leo bado hajarudi. Akashangaa sana maana alimuona kwa macho yake akishuka kwenye gari la shule ila hakumuona tena, alipojaribu kumpigia mkewe kwamba amefika wapi akawa hapatikani. Ilipofika saa moja wakati bado hajui la kufanya, yule kichaa mwenye salfeti

lenye vitabu akamuona Mhindi alivyochanganyikiwa akamsogelea kwa karibu wakati akiwa nje anasubiri vijana wake walioenda kwenye njia mama anazopita wamletee taarifa ili kama hayupo akaripoti Polisi. Kichaa akashusha salfeti na akampa karatasi cheupe kilichoonekana kisafi sana, hali ya usafi wa ile karatasi ilimfanya Mhindi apokee. Alipokipokea tu wakati anakikagua ili aone kuna nini kichaa akapotea.

**“USIHANGAIKE WE HAVE THEM (Wife & Kid),  
TUMEWANYAKUA”**

**006 MAFIAN GANG- Let's Talk 0754.....**

Huo ndio ujumbe ambao Yule kichaa alimpatia Mhindi halafu akatoweka. Jimmy “The INVISIBLE” huwa anapenda kuanza yeeye mission na kumaliza yeeye. Jana yake alipeleleza nyendo zote na kuchora ramani zote na leo anaonekana tena akimpa Mhindi ujumbe wake. Mhindi baada ya kupokea kile karatasi na kusoma ule ujumbe ndio akajua yule kichaa aliyeonekana jana hakuwa kichaa bali mtu mbaya sana kwake. Alishangaa jinsi watu muhimu wa familia yake walivyotekwa kirahisi sana bila kelele.

Kumbe mtoto alivyoshuka kwenye gari la shule akaona mtu anamuita kwenye gari la Babake, hivyo akaacha kuingia ndani akaenda kwenye gari la Babake. Na Mama alivyokuwa anafanya mazoezi yake ya kutembea alipofika mahali flani akaona anapigiwa honi kwa nyuma, kuangalia hivi ni gari la mume wake, halafu lile gari likampita likasimama mbele yake akalifata kujua kulikoni Baba anamfata na gari leo. Alichokifanya Jimmy “The

INVISIBLE” jana ni kujua nyendo na vitu vya familia ya yule Mhindi, na kisha wakaweka namba za lile gari na ndivyo walinyakuliwa kirahisi. Kwa hiyo kila aliyeona haya matukio asingedhania ni watu wabaya wamewachukua.

Wakati Mhindi anawaza ni nini hii akasikia sms imeingia kwa simu yake

**“HAPA NILIPO NAKUONA, USIJARIBU KWENDA  
POLISI MAANA UTAKUTA MIILI YA MKEO NA  
MWANAO TUMEKUTUPIA HAPO ASUBUHI”**

### **006 MAFIAN GANG**

Mhindi akajua hawa watu ni hatari sana, akikumbuka tu kuhusu yule kichaa anagundua wana akili sana. Mhindi akaamua kuwa mpole. Akanyanya simu akapiga, ilivyoita mara moja tu akasikia “Miaka miwili iliyopita kuna dili chafu mlilifanya na mtu la hela nyingi sana, unakumbuka?!” sauti kutoka upande wa pili alimhoji bila hata salamu. “Ndio ndio ndiooo!” Alijibu Mhindi kwa uoga sana. “Nyie tokeni hapa kwenda mbali kuleee!” Mhindi alisikika akifukuza wafanyakazi wake ambao ndio kwanza walikuwa wamerudi kumpa habari kwamba Mama hajapatikana.

“Fanya hivi, kesho saa tatu weka bilioni mbili unayodaiwa kwenye salfeti la Yule kichaa litakuwa mlangoni kwako. Kisha litoe nje na kufunga mlangano kwa ndani!” Sauti ya upande wa pili iliamuru. “Sawa sawa nitafanya hivyo, please usiwaumize mke wangu na mwanangu.” Mhindi alijibu huku anatetemeka. Unajua kwa sababu walilolifanya lilikuwa ni dili chafu Mhindi

asingeweza kwenda Polisi, lakini pia alichohofia sana ni Mke na Mtoto wake kuuawawa.

Ile anaamka asubuhi anakuta salfeti la yule kichaa pale nje, analivuta ndani anaweka fedha halafu analitoa nje anafunga mlango. Kitendo cha hajamaliza kufunga mlango yule kichaa anapita analibeba halafu inapita gari ile kama ya Mhindi inambeba kichaa na salfeti lake. Saa nne kamili anapigiwa simu kutoka shulen i kwa Mtoto wake kwamba “Tunashukuru gari la shule lilimuacha mwanaao ila ameletwa hapa na gari lako na vijana wako.” Anashangaa gari lake lipi na vijana wake gani, anaamua kupotezea. Saa tano kamili Mke wake anashushwa nje ya duka lake na gari lake. Anaangalia uani kwake gari halisi lipo. Anashangaa mke wake hana hata mchubuko, na anaonekana hana wasiwasi anamuuliza “Kulikoni” Mke wake anamwambia “NILINYAKULIWA!” Ila nilikula vizuri na nikalala vizuri, na mwanangu yupo shule. Mhindi akiwa bado haelewi sana, simu inaita na anaangalia jina ni Mr Kobre, anasita kupokea ila baadae anapokea “ AHSANTE SANA, HAKI YANGU HUWA HAIPOTEI, NAAMINI SUJAKUTENDEA UBAYA JAPO ULIKUWA MBAYA, tukutane Land Mark Hotel tupate kikombe cha Kahawa!!” Alisema Mr Kobre kwa furaha.

# 21

## AKISI YA MSHAMBA

**J**ioni hii Mashauri alionekana amekaa kwa ukimya sana mbele ya madarasa ya Engineering karibu na Uwanja wa Basketi. Alikuwa anashangaa kwa namna alivyokutana na Lulu siku ya kwanza kwenye foleni ya usajili. Jinsi Lulu alivyomxitiri ile siku kutohana na njaa kali aliyokuwa nayo huku akiwa hana hata shilingi mfukoni. Namna alivyoshikana mkono na Lulu pale Cafeteria kwa ishara ya ahadi ya kumsaidia Lulu Kiroho, lakini jinsi walivyoenda kule MAISHA BASEMENT Club kumchukua Lulu BASH. Na mwishoni anakumbuka Jumapili ambayo Lulu aliamua mwenyewe Kuokoka, Mashauri akashusha pumzzi kwa nguvu akasema “NI BWANA, AHSANTE YESU!” Tofauti hata na wavulana wengine Waliookoka kama yeche Mashauri hakuwahi kuvutiwa wala kumtamani Lulu kwa namna yeyote ile kimpenzi. Yeye aliamini tu kwamba hawakukutana kwa bahati mbaya, na baada ya tafakari hii Mashauri anaamini Mungu alimkutanisha na Lulu ili aokoke. Hii ilimtia moyo sana, na aliamini bado ana kazi

moja kabisa ya kumsaidia Lulu kuukulia Wokovu mpaka atakapoweza kusimama vizuri katika Imani yake ndani ya Kristo.

“Mtumishi una mgeni wako anakutafuta kule darasani, Babu unatisha sana, hiyo dawa yako nitakuja unipe na mimi!” alisema Jabiri moja kati ya wanafunzi anasoma nao Engineering. “Sijakuelewa Kaka, Dawa gani?!!” alisema Mashauri. “Mtumishi kwa uzuri wa yule binti, na kwa wewe ulivyo ni lazima kuna namna umemloga yule binti wa watu, nenda bhana anakutafuta kule!!” alisema Jabiri. Hapo sasa Mashauri alimuelewa Jabiri, alichokifanya ni kuinuka alipokaa na kuondoka kuelekea darasani alipoambiwa anatafutwa. “Hupatikani Masha, Shalom!” Lulu alimwambia Mashauri, “Nisamehe, nilizima simu kidogo nipate muda wa kutafakari, pole kwa usumbufu!!” alijibu Mashauri kwa ustaraku wa hali ya juu. “Umemaliza WAEFESO Dadangu?!!” aliuiliza Mashauri. “Ndio Mtumishi, Namshukuru Roho Mtakatifu naendelea kuyaelewa maandiko!” alijibu Lulu. Alichokuwa anakifanya Mashauri ni kumpa Lulu kazi za kutosha za kujifunza NENO na mfululizo wa MAOMBI ili kumuimarisha kiimani, lakini walikuwa wanapata nafasi ya kukaa wawili kujifunza NENO na wakati mwagine wanakutana wanne yaani Mashauri, Lulu, Manka na Atupele na wanajadili mambo yanayohusu Imani yao katika Kristo.

Tangu Kuokoka kwa Lulu, ukaribu wa Lulu na Mashauri uliongezeka maradufu. Ungeweza kudhani wanasona kozi moja kumbe wala, ilianza kuwa adimu sana kumuona Lulu Cafeteria au Chapel bila Mashauri pembedi. Mashauri ambaye kuva vizuri bado kunamshinda na Lulu ambaye kwa asili ni mtoto wa mjini tena anayetoka familia yenye uwezo kifedha, walionekana

kutokuendana kabisa, kule Chuoni tunaita kumatch. Mashauri daima alivaa mishati mikubwa, suruali zake pana sana na chini moka za mitumba, na wala kwake ilikuwa haimpi shida hata kidogo.

Lulu alipoangalia saa yake akagundua ni saa moja kasiro, na kwakuwa ndio walikuwa wanaelekeea mitihani ya mwisho wa Semister maarufu UE. Lulu akamwambia Mashauri “Masha, nina discussion kwa ajili ya UE saa mbili, kama hutojali naomba twende Cafteria tupate dinner pamoja then tuachane!” Masha hakubisha, baada ya dakika mbili walianza kushuka chini kwenye moja ya Cafteria. Wakiwa kwenye barabara kubwa ya magari, ghafla ikapita Rav 4 kwa kasi kisha ikaenda kusimama mbele yao kwa breki kali. Kumbe Calvin na Hamidu wakiwa wanaelekeea nyumbani waliwaona Lulu na Mashauri, wakageuza gari na kuanza kuwafatilia kwa nyuma.

“Yaani huyu Mshamba ndio anakuchanganya demu mzuri kama wewe kweli!!” Hamidu alisema kwa dharau huku akimtazama Mashauri kuanzia juu mpaka chini. “Sio bure wewe jamaa ni mchawi ila dawa yako inaiva!” alisema Calvin kwa hasira. Wakati huu wote Lulu na Mashauri walikuwa kimya wanawaangalia tu. “Lulu wewe ni boyo sana, hivi ukijiangalia unaendana na huyu Mshamba kweli??!!” Hamidu aliendelea kuporomosha maneno. “Dada Lulu mbona mimi sielewi??!!” Masha alisema kwa kujihami, “Masha, Relax!!” alisema Lulu. “Eti Dada Lulu, kaone kalivyo kafupi na keusi hata kuvaa hakajui!! Sio bure Babu yako lazima ni bonge ya mchawi!” aliropoka Hamidu. “BWANA utete nao, wanaoteta nami,

BWANA pigana nao wanaopigana nami, katika Jina la Yesu!!” alisema Mashauri halafu akaanza kuomba.

# 22

## UFUSKA KAZINI

**I**likuwa ni kawaida ya Irine kwenda Sinza Mapambano wanapoishi Hamidu na Calvin kila siku za Ijumaa na kurudi Chuoni Jumatatu asubuhi. Ijumaa hii ya wiki ya mwisho kuelekea mitihani ya mwisho yaani UE, Hamidu alimtaarifu Irine asiende kwani hawatakuwepo kabisa na badala yake watakwenda nyumbani kwa kina Calvin kule Masaki. Irine alielewa na akaamua kubaki Hosteli huku akijisomea, wikiend hii Queen hakuwepo maana alikuja kuchukuliwa na kijana mmoja shombeshombe wa kizungu na akasema wanaenda MBUDYA ISLAND kwa Matanuzi.

Asubuhi ya Jumamosi Irine alianza kujisikia kichefuchefu na ghafla akaenda kutapika kwenye sinki, wakati huu Lulu alikuwa anamuangalia tu mle chumbani. Hofu ilianza kumuingia kwa maana alianza kuhisi kabisa zile zilikuwa ni dalili za ujauzito, kwa haraka haraka akamuandikia sms Queen “Shosti mbona kama nina mimba jamani?!!” Uuuuwiiiiii!!!!” Halafu Queen akajibu “Utajiju, Mambo ya BASH hayo. Polee kimbia Pharmacy ucheki

faster huwa wanauzua vipimo!”. Basi Irine bila kupoteza muda akaenda Pharmacy akanunua kipimo na alikuwa hajui kukitumia akaomba asaidiwe pale Pharmacy. “Dada ni kweli una ujauzito!!!” alisema Dada wa Pharmacy, Irine alijihisi kuchanganyikiwa, akajikaza akarudi Hosteli akiwa hana amani kabisa. “Irine, Are you oky??!” Lulu aliuliza kwa upole, “Soma, Hayakuhusu haya!” Irine alijibu kwa ukali sana. Lulu alipoona hivyo akasema tena kwa upole “Nisamehe Irine！”, halafu akaendelea na mambo yake.

Irine kwa namna alivyokuwa amechanganyikiwa ilibidi aanze kumsaka Hamidu kwenye simu, alijaribu kwa muda mrefu kupiga na kutuma sms bila mafanikio. Simu iliita tu bila kupokelewa, na sms zilionekana kusomwa bila majibu yoyote. Mara akapata akili ya kumpigia Calvin, na ye ye simu yake ikawa inaita tu bila kupokelewa. Kwa kuwa ilikuwa Jumamosi Irine aliamua kutulia kimya huku akijilazimisha kusoma mle chumbani, aliwaza mengi sana. Kwanza aliwaza kuitoa ile mimba ila akawa anaogopa kufa au kuharibu kizazi, pili akawa anawaza kuzaa akaona kwa familia yao itakuwa aibu kubwa sana na Mzee wake kumsusa mazima. Aliwaza alifanya kosa kubwa kama lile ili hali ndio kwanza Semister ya kwanza tu tangu amejiunga na Chuo Kikuu. Akaanza kukumbuka ule usiku wa BASH alivyokuwa ameleta na hakuweza hata kukumbuka alikuwa kwenye siku za hatari ili walau wangetumia kinga, au kesho yake angemeza vidonge vile vya kabla ya masaa 24. Aliendelea kuwaza na kuwazua mwisho wa siku aliamua kumtafuta Hamidu ili wapate muafaka kwa pamoja.

Kama saa 11 za jioni Irine aliamua kukodi Bajaji ili impeleke mpaka Sinza Mapambano kwa Calvin, ili akahakikishe

kwamba ni kweli hawapo halafu ndio atajua cha kufanya baada ya kuwakosa. Tangu asubuhi ile amekuwa akiwapigia hawapokei na alipofika alasiri ikawa wote wawili hawapatikani tena. Dereva wa Bajaji aliendelea kuambaa na barabara, na sasa alianza kuingja mitaa ya Sinza Mapambano kabla Irine hajamwambia “Niache hapohapo” “Dada inaonekana una mawazo sana leo, sio kawaida yako!!” Dereva wa Bajaji alimwambia Irine. Irine bila kujibu alimpa noti ya shilingi Elfu Tano, Yule dereva akampa Elfu Tatu yake kisha akaondoka.

Irine alimuamuru dereva amshushe kama mita 50 kabla ya ilipo nyumba ambayo Calvin alipewa na Mama yake ambayo ndiyo anaishi na Hamidu. Yeye alipafahamu hapa vizuri sana maana Semister hii yote wikiendi zake zinaishia hapa. Aliendelea kusogea mpaka geti la mbele na ghafla akaanza kusikia mziki mkubwa ndani pamoja na kelele flani. Hakuamini sana masikio yake na akaamua kujiaminisha pengine ni kwa jirani maana nyumba zilikuwa zimebanana sana. Alipofika getini ndipo aliamini ule mziki na zile kelele zilikuwa zinatoka mle ndani, na alipojaribu kuchungulia akaona ile Rav 4 ya Calvin ipo pale nje. Alijaribu kugonga geti la mbele ila hakuna aliyesikia kutokana na zile kelele mle ndani. Kwa kuwa yeye ni mwenyeji aliamua kutumia geti dogo la nyuma ya nyumba, na kwa bahati nzuri lilikuwa wazi. Alipoingia tu ndani ya geti hapo sasa ndipo aliusikia ule mziki vizuri na aliweza pia kusikia sauti za wasichana na wavulana wakionekana kufurahia ama kusheherekeea. Akili yake ilimwambia azunguke kwa mbele ili akashuhudie kwa dirisha kubwa la sebuleni kwamba ni nini kinaendelea na ni kina nani wamo humo ndani leo. Alipozunguka na kufika dirishani,

hakuamini macho yake juu ya kile anachokiona, kwanza alianza kumuona Calvin aliye kuwa kifua wazi na boxer tu akiwa amezungukwa na wasichana wawili, mmoja anampapasa mgongoni na mwininge amempakata, huku hao mabinti wakiwa kama walivyo zaliwa. Alipopitisha macho upande wa pili aliweza kumuona mpenzi wake Hamidu akiwa na boxer tu pia, huku wasichana wawili wakiwa wame mlilia kulia na kushoto huku nao wakiwa kama walivyo zaliwa. Mezani aliona chupa nyingi na mivinyo na pombe zingine kali, huku akishuhudia mabaki ya nyama choma na vyakula mbalimbali vya gharama. Ilibaki kidogo azimie ila akakaza moyo akarudi nyuma ya nyumba halafu akaingia ndani ya nyumba kwa kutumia mlango wa nyuma.

“Hongereni Vijana naona mpo Masaki, Hamidu Ahsante sana!” Irine alisema maneno haya kwa uchungu huku akitoa kilio kilichowapa taharuki wote pale ndani japo walikuwa wamelewa chakari. “Disko limeingiliwa na Masai!!!” Alisema mmoja kati ya wale wasichana na kwa dharau. Hamidu akashtuka sana, akawasukuma wale wasichana pembeni halafu akawa kama anamfata Irine, kwa akili ya haraka ungeweza kudhani anaenda kumuomba msamaha. Ila alipofika karibu na alipo Irine akamfokea “Weee mbwa kwanini unanikosea adabu na kuni haribia starehe zangu aisee!!!!” akanyanya mkono wake akamchapa Irine kofi la haja lililompeleka Irine chini halafu akazimia hapohapo. Kwa namna alivyo na roho mbaya na jeuri, akawaita wale mabinti aliokuwa nao akawaonyesha ishara wa endelee na walichokuwa wanafanya. Calvin baada ya kuona alichokifanya Hamidu alitaharuki mpaka pombe yote ikaisha kichwani, “Hamidu hii ni Murder Case Umeua wewe, Umeua

nakwambia!!!!” alisema Calvin huku akikimbia pale alipo Irine. “Kevo, kula maisha bado anahema huyo!!!” Hamidu alijibu bila kujali. “Jamani huyu kafa mbona katulia hivi, mmh hebu tulipeni sisi tuondoke!!!” alisema mmoja kati wa wale wasichana wanne.

Kumbe walichokifanya Calvin na Hamidu walienda usiku wa Ijumaa Sinza Kumekucha wakawanunua wasichana wanne wanaojiuza, tena wakawachagua wale ambao bado ni wadogo wadogo ili wastarehe nao usiku wa Ijumaa mpaka Jumapili asubuhi. Na ndio maana Hamidu alimzuia Irine kuja huku Sinza nyumbani kwa Calvin anapoishi. Calvin huwa ni muoga sana, alichofanya aliwalipa wale machangudoa wakaondoka na kisha akaanza kumpepea Irine ili walau aamke. Wakati wote huu Hamidu alionyesha kutojali kabisa kile kilichomtokea Irine. Baada ya kama lisaa limoja hivi, Irine akazinduka halafu akaendelea kulia sana. Muda wote huu Calvin alikuwa akimbembeleza na kumwomba atulize hasira, wakati Hamidu ndio kwanza aliwapa mgongo na kuendelea na mambo yake kama haelewi kilichotokea. “Hamidu Ahsante sana, Nilikuwa sikufahamu vizuri kumbe, ila leo nimejua namna ulivyo katili na muuaji!!” Irine alisema kwa uchungu sana. “Sema kilichokuleta, uondoke na kiherehere chako fala wewe!!” Hamidu alifoka kwa hasira na wakati wote huu alikuwa kampa mgongo Irine hataki hata kumuona. Kwa Hamidu Msichana kwake ni kama chombo cha starehe tu na sio vinginevyo. “Hamidu, nina mimba yako hiki ndicho kilichonileta!!” Irine alisema huku bado analia sana. “Aya, nisiiione hiyo mimba. Hakikisha haifanyi na wewe mtihani. Ondoka haraka nisiiharibu hiyo mimba kwa mikono yangu!!!” Hamidu alifoka zaidi huku anageuka na kuanza kumsogelea Irine

tena ila Calvin akamzuia. Wakati huu wote Calvin hakutia neno, kwa kuwa alishakuwa kavaa tayari aliamua kumpeleka Irine chuoni kwa gari lake. Njiani Irine alilalama na kujilaumu sana “Nilikuwa Mjinga sana, siku ya kwanza nilipomuona Hamidu kwenye gari nilimpenda na nikamwamini sana, siku hiyo nilimpa mwili wangu!!!” “Relax Mama!!” Calvin alisema. “Nyie Wanaume ni wabaya sana na hamridhiki kabisa, Imagine machangudoa kweli!!!” Irine alilalamika mno. “Aya tumefika, Shuka!!!” Calvin alisema alipokuwa amepaki mbele ya Hosteli ya kina Irine.

“Lulu!!!” aliita Irine. “Abee Irine!!” Lulu aliiitikia kwa kuhamaki maana alimuona Irine namna uso ulivyokuwa umevimba, na macho yake yalivyokuwa mekundu kutokana na kulia. “You are Right, and I was wrong!!’ alisema Irine na kisha akaanza tena kulia upya. Lulu alitumia hiyo nafasi kumbembeleza mpaka akawa sawa. Kisha usiku huu wa Jumamosi wakiwa chumbani wao wawili tu, Irine alimhaduthia Lulu kila kitu tangu walipokutana na Hamidu kwenye basi, maisha waliyokuwa wanaishi kule kwa Calvin. Usiku huo huo Irine alianza kujisikia vibaya tumboni, ghafla akaanza kutokwa na damu. Lulu aliita wadada wengine wawili watatu wakampeleka Zahanati ya Chuo, kumbe wakati alipopigwa lile kofi na Hamidu akazimia, aliangukia tumbo na hivyo mimba iliharibika. Kwa hakika hii ilikuwa ni siku mbaya sana kwa Irine tangu amezaliwa.

# 23

## EXPERIENCING UTAMU

“ Dr Kim, niambie kama umeshawahi kukutana na hii from all years of your woman experience??!!” aliuliza Queen kwa majidai huku akimshikashika Dr Kimaro kichwani huku akiwa kajilaza kichwa chake kifuani mwa Dr Kimaro. “I’ve never kwakweli, this is the very new sweet experience ever!!” alisema Dr Kimaro huku akionekana kufurahia mautundu na ubunifu wa Queen. “Promise Me “A” in your every course every Semister na nitakufanya zaidi!!” alisema Queen huku akijipindisha kuuweka mwili wake mzima juu ya mwili wa Dr Kimaro na kuanza kumpapasa kifuani. Ukweli ni kwamba Queen alifanya yote haya kwa sababu tu alitaka kuwa zaidi ya Lulu kwenye kila eneo, na ndio maana alijitongozesha kwa Dr Kimaro kuhakikisha anaondoa kabisa mawazo yake kwa Lulu. Licha ya kwamba ni kweli kwamba alikuwa anataka ufaulu mzuri bila kutumia nguvu kubwa, lakini ushindani wake kwa Lulu ulikuwa kipaumbele zaidi. Haya yote yalikuwa yanatokea mara baada ya kuwa wamemaliza Mitihani ya UE kwa Semister ya kwanza. Queen alikuwa anakula starehe na Dr Kimaro kwenye moja ya Hoteli maarufu katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Kama ilivyo kwa wanaume wengi huwa hawawezi kuridhika na mwanamke aliyejileta mwenyewe, huwa wanajisikia kuwa wanaume zaidi pale anapohangaika kumpata msichana fulani kwa muda fulani halafu akafanikiwa kumpata. Halikadhalika kwa Dr Kimaro pamoja na yote aliyoanyiwa na Queen bado akili na hisia zake zilikuwa kwa yule msichana Lulu. Dr Kimaro alijiapiza kwa nafsi yake kwamba atatumia njia yoyote kwa gharama yoyote ili tu ampage Lulu. Na alidhamiria mno kwamba Semister ya Pili mapema tu amalize mchezo ili apate muda wa kufurahia maisha na mtoto mbichi mzuri wa kimasai.

“Ms Lulu, Congrats!!” Lulu alipokea sms kutoka kwa Dr Kimaro alipokuwa kajituliza nyumbani kwao Arusha likizo. “Good Evening Dr, Why Congrats?!?” alijibu Lulu. “You’ve done Excellent to all my course!!” alieleza Dr Kimaro kwa sms pia. “Oooh Ahsante sana Dr, Congrats too. You taught us very well!!” alijibu Lulu akimpongeza Dr Kimaro kwa kufundisha vizuri pia. “You will always do wonders to my Course as long as you will be supportive!!” Dr Kimaro alimsms tena Lulu. “Sorry Dr, Which Support??!” Lulu alihamaki ikabidi aulize. “See you coming Semister!!” Dr Kimaro alijibu kwa kifupi. Taa nyekundu iliwaka moyoni kwa Lulu, ukichukulia kwamba alishasikia habari nydingi ambazo sio nzuri hasa kwa wanachuo wa kike. Ghafla Lulu akakumbuka maneno kwenye Biblia yanayosema **“Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuzishinda hila za ibilisi....”** Na akaamua kushirikisha baadhia ya marafiki zake wachache akiwemo Mashauri ili waanze kuomba pamoja ikiwa bado mapema. Lakini pia kitu tu kikamwambia moyoni kwamba asizifute zile sms zote alizotumiwa na Dr Kimaro.

Zikiwa zimebaki wiki mbili tu kabla ya kufungua chuo Mashauri ye ye alikuwa kijiji kwao Kinyambuli kule Iramba akipambana na ujenzi wa nyumba ya Mama yake. Zile Fedha kidogo kidogo alizokuwa akizibana kila Semister na kuzituma nyumbani, zilifanikisha kufyetua matofali ya kutosha na mabati kwa ajili ya nyumba ya vyumba viwili na sebule. Kwa hiyo likizo hii aliweza kujenga na kupaua, na kwa kuwa hakuwa na fedha ya ziada ilimbidi kuyaziba madirisha kwa matofali na kuacha sehemu ndogo ya hewa kuingia, halafu akatafuta sehemu mlango mmoja wa kukopa ilivalau kabla hajaondoka Mama ahamie nyumba mpya ya bat. Na kwa kuwa kijijini hakuna umeme Mashauri hakuwa anapatikana kwenye simu yake kwa urahisi. Kwake kuwa karibu na Mama yake ambaye kwa sasa alionekana kama Bibi kabissa, ilikuwa ni faraja kubwa sana. Mashauri alitumia likizo yake ya mwezi mzima kuhakikisha anamsaidia Mama shughuli za shamba, lakini pia anasaidiana na fundi kujenga nyumba ya Mama, maana hakuwa na fedha ya kutosha kuajiri kibarua, kwa hiyo ye ye ndiye alikuwa kama kibarua wa fundi mpaka nyumba inakamilika. Hakika hii ilikuwa likizo yenye kazi sana kwa Mashauri.

Siku moja Manka akiwa likizo wakati anatoka Moshi Mjini kwa daladala kuelekea Kiboroloni kisha apandishe kwao Fukeni na bodaboda, daladala ilipofika kwenye Round About ya YMCA ghafla alipotazama nje alimuona mtu kama Mzava yule rafiki yake Mashauri waliyekutana nae Luguruni ambaye anasoma St Joseph. Mzava ye ye alikuwa kwa mguu anaelekea barabara ya KCMC, Manka hakuwa na uhakika sana kama ni ye ye ila akaamua kushuka kituo cha YMCA na kisha kwa kuwa alikuwa na namba

za Mzava akampigia. “Mtumishi nimekuona YMCA, ni Wewe??!!” Manka aliuliza. “Ndio ndio, nani mwenzangu?!!” aliuliza Mzava. “Mimi Manka rafiki yake Gwantwa tuliyekuja na Mashauri siku ile!!” Manka alitoa maelezo ya kutosha. “Oooh samahani Manka Mtumishi, nimebadili simu nisamehe sana, Wewe uko wapi?!” aliuliza Mzava kwa shauku. “Nimeshuka hapa YMCA!” Manka alijibu. “Nakuja hapo nisubiri tafadhalii!!” Mzava alisema kwa kusisisitiza. Japo alikuwa ameshika barabara ya kuelekea RAU, Mzava aligeuza kwa haraka na kumfuata Manka pale kituoni YMCA. Basi Manka na Mzava walikutana, wakatafuta mahali wakakaa na kuongea mengi sana na hii iliwapa nafasi ya kufahamiana vizuri. Tangu hapa waliamua kuitana “MTANI, MTANI” Si unajua tena Mzava ni Mpare na Manka ni Mchaga. Wachaga na Wapare ni Watani walioshibana sana.

# 24

## VURUMAI ZA UCHAGUZI!

**K**ikawaida Semister ya pili Chuoni huwa ni Semister yenye mambo mengi sana. Wakati huu Chuo kizima kilikuwa na shamrashamra za kuelekea Uchaguzi wa Serikali ya Wanafunzi yaani DARUSO. Uchaguzi huu ulikuwa ni wa aina

yake kwa sababu kuna kijana wa mwaka wa kwanza kitivo cha Sheria, ambaye inasemekana Baba yake ni kigogo Serikalini aliamua kugombea nafasi za juu kabisa za Uongozi wa DARUSO. Huyu sio mwingine bali ni Calvin John Sanga, ambaye ni Mtoto wa Brigedia Jenerali John Sanga ambaye ni Waziri wa Nishati na Madini. Kama kawaida Matawi ya vyama vyaya siasa ndani ya Chuo ndio haswa hufanya michakato ya chini kwa chini kuhakikisha kwamba anayeshinda kiti cha Urais wa DARUSO ni mtu wao. Hivyo Chama Tawala cha OCM kupitia Umoja wa Vijana wake tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nao walianza michakato ya chini kwa chini kuhakikisha wanaweka mtu sahihi ambaye atashinda kwa kishindo kama ilivyo kawaida yao. Na hofu yao kubwa ilikuwa ni mgombea ambaye Chama Kikuu cha Upinzani CHAUKA wangemsimamisha kugombea nafasi hiyo.

Calvin John Sanga mtoto wa Waziri aliwasumbua sana akili zao, hasa ukichukulia kwamba ni mtoto wa kigogo na tayari Mama yake alishamtenga fedha za kutosha kuhakikisha anashinda uchaguzi huu. Viongozi wa Tawi la OCM Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walimtaka sana Leon Magibo mwanafunzi wa mwaka wa tatu sheria ndiye asimama kuwania nafasi ya Urais wa DARUSO kupitia chama chao. Leoni Magibo alikuwa na ushawishi wa aina yake, na kwa uongozi unaoondoka alikuwa Spika wa Bunge. Japo Leon hakuwa ametoka familia tajiri wala yenye historia ya Uongozi wowote mkubwa, bado uwezo wa ushawishi wake ulikuwa mkubwa mno. Ndio hasa kupitia Bunge alisababisha viongozi wa DARUSO wakutwe na kesi kubwa ya Ubadhilifu wa fedha. Kwa hiyo Calvin John Sanga hakustahili hata kidogo kugombea nafasi hiyo kubwa unapomlinganisha na

Leoni Magibo. Na OCM waliogopa zaidi kutomsimamisha Leoni Magibo mara baada ya kusikia CHAUKA wana mpango wa kumsimamisha Waziri Mkuu aliyemaliza muda wake kugombea Urais wa DARUSO.

Wakati huu Queen alikuwa karibu mno na Calvin kuliko wakati wowote ule. Daima Calvin alikuwa akitembea na Queen na Hamidu, Hamidu aliyejazia haswa mwili wa mazoezi alionekana kama Bodigadi wake na Queen alionekana kama mpenzi na mshauri wake wa karibu. Na hawa wawili ndio walikuwa wanampa kichwa Calvin kwamba anastahili kuwania nafasi hiyo kubwa kabisa ya Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi. Calvin kwa kutumia fedha aliweza kuwanunua baadhi ya viongozi wa juu wa OCM tawi la Chuoni kwao, na hawa wakawa upande wake. Kama isingekuwa hekima za Katibu wa Itikadi na Uenezi Mkoa wa Dar es Salaam kuingilia kati, basi ni dhairi Chama kingegawanyika. Baada ya Vuta Nikuvute nyingi pamoja na Maagizo kutoka juu, ilibidi wakubaliane kwamba Leoni Magibo atasimama kugombea nafasi ya Urais wa DARUSO na Calivin John Sanga mtoto wa kigogo atapewa uteuzi wa Uwaziri Mkuu mara baada ya wao kushinda Uchaguzi huo.

Pilikapilika za Kampeni za Uchaguzi zilianza kwa fujo isiyo ya kawaida, OCM chinichini kupitia mgombea wao Leoni Magibo walinadi sera za moto sana huku wakikosoa vikali Uongozi unaoondoka madarakani ambao viongozi wote wa juu walitoka CHAUKA kwa ubadhilifu wa fedha, lakini pia kushindwa kusimamia maslahi ya wanafunzi ikiwemo mikopo na taaluma. Huku wakijinadi kuwa wao ndio wenye nguvu na watakaposhinda kila kitu kitaenda sawa. CHAUKA kupitia

Omary Rasuli mgombea wao wa Urais ambaye ndiye alikuwa Waziri Mkuu katika Serikali ya DARUSO inayomaliza muda wake aliendelea kusisitiza kwamba Bunge liliwafanyia fitina kubwa ili tu waonekane hawafai, na huku akisema mgombea wa OCM hawezi wala hana ubavu wa kuisimamia Serikali maana na wao ndio sehemu ya Serikali yenyewe.

Vuta Nikuvute hizi ziliendelea kwa muda wa wiki mbili, huku Calvin John Sanga akisimama kama Meneja wa Kampeni. Wanafunzi wajanja walifaidi fedha, nguo, pombe na vitu mbalimbali vilivyokuwa vinatolewa na vyama vilivyopo nyuma ya Wagombea. Mwisho wa siku Uchaguzi ulifika, na Leoni Magibo kushinda Uchaguzi ule kwa zaidi ya 70%, hii ilitokana na wanafunzi wengi kuwa na imani nae mara baada ya kuongoza Bunge kusimamia kidete kuibua ubadhilifu wa fedha ya uongozi unaoondoka madarakani. Wanafunzi wengi walifurahia sana ushindi wa Rais anayependa haki na maslahi ya Wanafunzi. Japokuwa walishangaa sana pale ambapo Rais mpya wa DARUSO Leoni Magibo alipomtangaza Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza Calvin John Sanga kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi yaani DARUSO. Wengi hawakujua ni kitu gani kilichotokea nyuma ya pazia, japo baadae walikuja kugundua kwamba Calvin John ni mtoto wa Brigedia Jenerali John Sanga ambaye ni Waziri wa Nishati na Madini.

Pamoja na kuteuliwa Rasmi kuwa Waziri Mkuu wa DARUSO, Calvin bado hakuwa na furaha kabisa maana alikuwa na uwanja mpana wa kumpata msichana yejote pale Chuoni kutoka nae kimapenzi isipokuwa Lulu.

# 25

## MISS UNIVERSITY!

“**L**ulu, tumeona tukutafute na tukushauri uwakilishe Kitivo cha Sheria katika shindano la Miss UD, tutakuwa nyuma yako na tuhakikishe unashinda taji hili!” alisema Annamary mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa sheria. “Tafadhali usikatae, unavyo vigezo vyote vya kushiriki na kushinda, kuanzia umbo, uzuri, urembo na akili” alikolezea binti mwingine aliyeshiriki mwaka uliopita na akashika nafasi ya pili. “Hii itakuongezea fursa na kujulikana, na baadae unaweza kushangaa unapata tenda za Matangazo na Project za Taasisi na Makampuni makubwa na Who knows baadae unaweza kuwa Miss Tanzania eti!!” alirudia kutoa maelezo ya kina Annamary anayeonekana kuyaelewa vizuri Mashindano hayo. “Yaani hata kama Dancing inakusumbua sie tutakufundisha maana tuna uzoefu wa kutosha!!” alisema binti mwingine. Wakati wote huu Lulu alikuwa ametulia tu akiwasikiliza kwa umakini sana, hata na hivyo walimfata Hosteli kwenye chumba chake wakati huo alikuwa akimuelekeza Irine baadhi ya mambo kuhusu Imani. Irine

aliamua kuachana kabisa na Queen Semister hii na kila mahali alionekana akiwa na Lulu.

“Dada zangu, Ahsanteni sana na mno. Mmenipa thamani kubwa sana na najiona mwenye bahati. Ila niwaambieni tu ukweli ili msiendelee kusumbuka sana, kwa namna ninavyoju Mashindano ya Umiss kuanzia vaa zao na mengine mengi yanayofanyika huko na kwa mujibu wa Maadili na Misingi ya Imani yangu SITAWEZA” aliwajibu Lulu kwa ujasiri na umakini mkubwa. “Yaani mnge newahi kabla ya BASH, kwa Lulu yule angeshiriki. Ila huyu ni Lulu mpya kabisa aliyetakaswa Fikra na Akili zake kwa Damu ya Yesu, huyu hawezi hata kwa bunduki kushiriki Mashindano hayo, Ahsante” aliwakazia Lulu kwa ujasiri. “Mmmmh!! Mbona unatuhubiria sasa mwenzetu!!!!” alihamaki Annmary “Kwamba wewe ndio Mtakatifu sana huna dhambiiiiii!!” akaongezea na kumalizia kwa kusonya. “Hoya, tuondokeni jamani tusije kuokoka bure hapa!!” akasema msichana mwingine. “Ndio tukome na Viherehere vyetu!!!” alisema Annmary huku wakiwa wanatoka nje. “Watu wengine bhana wanajidaigi wa Munguuu, yaani Am so disappointed!!!” Annmary aliendelea kulalamika na kujilaumu. Hata na hivyo wiki mbili baadae Queen alishiriki Mashindano hayo makubwa ya Umiss hapa Chuoni na alishinda kwa kishindo. Nyuma ya Ushindi wake alikuwepo Waziri Mkuu wa DARUSO Calvin John Sanga na haitoshi bado alipambana mpaka akahakikisha ametoka kimapenzi na Jaji Mkuu wa Mashindano hayo jambo lililomrahisishia sana kushinda. Mahusiano ya Queen na Irine yalivunjika mara baada ya Irine kuona Queen anaendelea

kuambatana na Hamidu na Calvin. Na akasikia pia kwamba Queen alishatoka pia kimapenzi na Hamidu hapa katikati.

“See Me at my office 14hrs!” sms toka kwa Dr Kimaro ilimfikia Lulu. “For what Dr?!! Sorry!!” Lulu alimjibu Dr Kimaro. “Office issues, don’t miss!!” alijibu Dr Kimaro. “Oky Dr!” alimalizia Lulu. Lulu alimpigia Mashauri simu kumjulisha juu ya ule wito wa Dr Kimaro, na Mashauri kwa kuwa anakumbuka kile ambacho Dr Kimaro alimuandikia Lulu wakati wa likizo, alimshauri Lulu atakapoenda ofisini leo ahakikishe anarekodi maongezi yao yote. Mida ya saa nane kasoro mchana Lulu alionekana akielekea ofisini kwa Dr Kimaro ili kujua ni nini hasa alichoitiwa na Mwalimu wake huyo.

“Oooh karibu Mrembo wa Kimasai!!” Dr Kimaro alimkaribisha. “Ahsante, Shikamoo Dr!” Lulu alijibu kwa kujihami. “Lulu, you are very beautiful girl I have ever meet in my life and career!!” alianza Dr Kimaro kwa maneno mengi wakati hata bado Lulu hajakaa. “I wanna make you the best girl ever in both class and life, tafadhali usichezee hii bahati!!” aliendelea Dr Kimaro. Lulu akiwa bado anashangaa shangaa tu hata bado hajakaa akasema kwa kuhamaki “How?!!” “You are matured enough, hope unanielewa hahahahaha, karibu ukae!!” alisema Dr Kimaro. “Ningeelewa nisingeuliza Dr!” Lulu alisema kwa upole sana. “Lulu nakupenda, na nakuhitaji sana, tafadhali usikatae ukafanya adui yako, then ukasoma kwa shida!!” alisema Dr Kimaro, awamu hii kwa Kiswahili akimaanisha zaidi. Kwa kuwa Lulu alikuwa anajua anachokifanya, aliendelea tu kuhoji maswali huku akijifanya kama anaingia uoga. “Please, Dr don’t do this to me!! Nisingependa nisome kwa shida jamani!” Lulu aliongea kwa

huruma akionyesha kuogopa sana. “You have a choice, being with me or live a hard life!!” alisema Dr Kimaro kwa kujiamini zaidi, alipoona Lulu anaogopa akaongeza mkwara zaidi “I have more than 12 course to teach from 1<sup>st</sup> year to 4<sup>th</sup> year, it is whether you with me or supplementaries and C” aliongea Dr Kimaro. “Imagine how 12 A’s will boost your G.P.A, or how 12 C’s will make you just an ordinary student ahahahaah” alimalizia Dr Kimaro kwa kicheko. Wakati huu Lulu alikaa kwa uoga zaidi huku akiminyaminyo vidole vyake vyake mikononi. “Dr you are my dad agemate, how can I sleep with you??!!” alisema Lulu huku anatetemeka midomo kwa hasira. “Unfortunate I’m not your dad, don’t complicate mrembo!!” aliongea Dr Kimaro kwa mbwembwe sana huku akisimama. Halafu akatoka mahali alipo akamfuata Lulu pale alipokaa, kisha akamsogelea karibu sana kama anataka kumnyanya kwenye kiti. Alipokuwa anainama akamkonyeza kiufundi sana kisha akamwambia kwa kumnong’oneza “the choice Is Yours, Good day!!!” Halafu akawa anarudi kwenye kiti chake mle ofisini akiwa anaangalia mikono yake akageuka akamwambia Lulu “Your degree is within the power of my hands, so I decide!!”

# 26

## JIMMY “The INVISIBLE”

**L**icha ya Calvin kuwa kiongozi wa juu pale Chuoni katika Serikali ya Wanafunzi yaani DARUSO, bado hiyo haikumfanya Lulu amkubali. Hii hali ilimuumiza sana na kumkondesha Calvin, na hiki kitu kilikuwa kikimuudhi sana Hamidu. Na kila walipokuwa wakijaribu kumfuatilia nyendo zake Lulu, waligundua mvulana pekee anayepata nafasi ya kuwa walau na muda kwa Lulu ni Mashauri. Mashauri ndiye yule kijana waliyemuona na Lulu ile siku wakitembea kuelekea Cafeteria, halafu Calvin na Hamidu wakawafata na gari na kuishia kumdhihaki na kumtukana Mashauri. Hivyo mpaka sasa waligundua kikwazo chao kikubwa kwa wao kumpata Lulu ni yule kijana yaani Mashuri.

“Ninajua cha kumfanya yule Mshamba!!” alisema Hamidu kwa dhiaka. “Unamaanisha nini??!!” aliuliza Calvin. “Niambie ikiwa nitakuambia cha kumfanya hautaleta uoga na huruma zako za kijinga!!” aliongea Hamidu akimtahadharisha Calvin. “Namuoneaje huruma mtu anayezuia furaha yangu?? Wewe sema tu tumnyooshe!!” alijibu Calvin kwa ujasiri sana. Hamidu alimueleza Calvin mkakati wa kumnyoosha Mashauri ambao utamfanya Lulu akubali, maana asipokubali itagharimu

uhai wa Mashauri. Na Hamidu alimtaka Calvin aandae fedha taslimu milioni 5 ili kazi hiyo ifanyike kwa haraka. Wakati huu ndio kwanza walikuwa wanaelekea kwenye Mitihani ya kumaliza Mwaka wa kwanza.

Jimmy “The INVISIBLE” alionekana kwenye maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwanza alionekana kwenye madarasa ya wanafunzi wa Engineering, na kisha Hosteli zao za ndani ya Campus, na baadae alionekana kuelekea CCT-Chapel. Muda wote alikuwa na begi lake lenye laptop ndani pamoja na dafatari moja la kaunta mkononi mwake. Ungekutana nae usingejua kwamba hakuwa mwanafunzi wa Chuo hiki maarufu Tanzania. Maana alivaa vizuri uhusika wa wanafunzi wengi wa kiume wa hapa Chuoni, mida flani alionekana akiwa anajisomea karibu na uwanja wa Basketball uliopo mbele ya madarasa ya Engineering. Maeneo alipokuwa anajisomea ilikuwa karibu kabisa na mahali ambapo Mashauri na Manka pia walikuwa wanajisomea. Kila baada ya muda flani Jimmy “The INVISIBLE” alikuwa anawaangalia Manka na Mashauri kwa jicho la kuibia, na kisha anaoanisha sura ya Mashauri na ile iliyokuwepo kwenye picha aliyonayo. Kwa kuwa hii ilikuwa siku ya Ijumaa, baadae Jimmy “The INVISIBLE” alionekana akiwa Fellowship CCT-Chapel kwenye kiti kimoja na Mashauri, alikuwa akiimba na kuomba kama moja ya wenyeji sana kanisani hapo. Ibada ilipoisha alimsalimia Mashauri na kisha akatoweka. Mashauri hakuwa na wasiwasi wowote japo aliona ile sura ni ngeni kidogo kwake, ila akajisemea Chuoni humu tupo wengi sana na sio rahisi kumfahamu kila mtu, lakini pia kikawaida karibu na Mitihani ya UE wanafunzi wengi sana uhudhuria Fellowship.

Kesho yake kwenye Ibada ya jioni yaani Jumamosi, Jimmy “The INVISIBLE” aliwahi mapema sana, wakati Mashauri anaingia alimkuta Jimmy amepiga magoti na amenyanya mikono juu akionekana kuutafakari Ukuu wa Mungu. Mpaka Ibada inaanza rasmi bado Jimmy “The INVISIBLE” alikuwa magotini akiendelea kuomba. Baadae alisimama na kujumuika na Wanafunzi wengine kwenye Ibada ya Baraka ya kusifu na kuabudu. Mara baada ya Ibada Jimmy alimfata Mashauri na kumuomba akitoka nje waonane ana jambo analohitaji ushauri wa Kiroho. Mashauri alikubaliana nae, walipotoka nje Mashauri akiwa anasalimiana na Lulu na Manka akamuona yule mtu pembeni akiendelea kuomba. “Jamani Dada zangu, kuna mpendwa pale alikuwa na jambo la kunishirikisha, na inaonekana ana mzigo mzito sana, tafadhali naomba nimuone!!” alisema Mashauri akiwaaga Lulu na Manka. “Unamfahamu vizuri, mbona sina amani jamani baada ya kumuona tu!!” alisema Lulu kwa tahadhari. “Ahahahahaha Lulu wewe Dadangu jamani, unapenda kampani sana, hapo unaogopa kushuka kula mwenyewe!!!” alisema Mashauri huku akiwa anaondoka. Mashauri alipofika kwa Jimmy, alimkuta bado anaonaekana kama anaendelea kuomba. Kisha Jimmy “The INVISIBLE” akamuonyesha Mashauri ishara amfate, halafu akaendelea kuwa kama anaomba huku akielekea nyuma ya Chapel. Mashauri akasema mwenyewe huyu jamaa atakuwa na jambo zito sana. Walipofika nyuma ya jengo Mashauri akashangaa kuona kama kuna gari kwa chini barabarani, akawa anataka kuzungumza akashangaa kazibwa punzi akaanguka akazimia.

Jimmy “The INVISIBLE” alikuwa tayari amemaliza kazi yake, Mtaalamu huyu toka kundi la 006 MAFIAN GANG lililo chini ya Chacha Marwa “CAPTAIN”, ndiye alipokea tenda hii ya kumteka na kumtesa Mashauri toka kwa Hamidu. Jimmy “The INVISIBLE” baada ya kujifanya mwanafunzi tena mpenda imani kwa siku mbili, alifanikiwa kuuteka ufahamu wa Mashauri na hivyo akamnyakua kirahisi sana bila kutumia nguvu. Kwa kuwa hili lilikuwa dili dogo tu la Milioni 5, Jimmy “The INVISIBLE” alishirikiana na deriva tu pamoja na jamaa mmoja bigwa wa kuteka na kutesa. Chacha Marwa “CAPTAIN” mkuu wa kikosi alimpa ruhusa Jimmy “The INVISIBLE” afanye hiyo dili aliyoita ye ye kama hela ya mboga kwake. Wakati Mashauri anashtuka, gari lililomteka aina ya Toyota Double Cabin ndio kwanza lilikuwa linaacha maeneo ya Tegeta kwa Ndevu kwa mwendo wa kasi sana kuelekea yalipo Makao Makuu ya kundi hatari la 006 MAFIAN GANG. Mashauri aliposhtuka alishangaa kuona yupo ndani ya gari linalokwenda kasi mno, na yuko nyuma ya siti ya dereva na jamaa mmoja aliyejifunika uso anaonekana macho tu. Mbele alikuwepo dereva pamoja na yule mpendwa aliyemuona Ibadani Ijumaa na Jumamosi jioni baada ya Ibada alimuomba amshirikishe jambo. Jimmy “The INVISIBLE” baada ya kuona Mashauri amezinduka mara baada ya kumbana pumzi kule nyuma ya Chapel, “Bwana Asifiwe Mtumishi, Tuendelee na maombi ahahahahaha” Jimmy “The INVISIBLE” alimsalimia Mashauri na kumcheka kwa dhiaka. Wakati Mashauri akifikiri ajibu au asijibu, ghafla ndani mwake akakumbuka ile **Kutoka 14:14** ya kwamba ***BWANA atawapigania nanyi mtanyamaza kimya***, akashusha pumzi akasema kwa sauti ya chini “BWANA NIPIGANIE”. Wakati yupo kwenye hayo mawazo, Jimmy “The INVISIBLE”

akamtania tena “Mtumishi kwa nini unagusa mali za wenyewe nguvu lakini??!!” Anyway, leo utaimba nyimbo zote za Zaburi ya 1 mpaka 150” Wakati huu Mashauri aliendelea kunyamaza kimya tu, kisha akakumbushwa tena ile **Zaburi ya 121:7** inayosema ***BWANA atakulinda na mabaya yote, Atakulinda nafsi yako.*** Jimmy “The INVISIBLE” alipoona Mashauri hamjibu kitu hii ilimtisha kidogo akasema “Ommy 006 mzime” Yule jamaa aliyekuwa na Mashauri huku nyuma akampiga Mashauri kichwani kitaalamu Mashauri akazimia tena. Gari lile liliendelea mpaka Mapinga kule yalipo makao yao ya 006 MAFIAN GANG. Mpaka anafikishwa Mashauri alikuwa bado hajazinduka, walichokifanya walimshusha na wakamfunga mikono na miguu kwenye mbuyu mmoja mkubwa sana ambao wao huutumia kwa utesaji wanaouita CALVARY. “Visa vya mapenzi vinachekeshaga kiukweli...!!” alisema Ommy yule mtaalamu wa Utesaji, halafu akaendelea “Imagine Mshikaji Mshamba Mshamba kama huyu bwana mdogo eti amewachukulia demu wale watoto wa mjini ahahahahaha!!” akamalizia kwa kicheko sana. Jimmy “The INVISIBLE” akacheka pia na kusema “Mapenzi Upofu!!!” “Oyooo Oyooo Oyooo!!!! Mshamba Mshamba mkononi mwa watabe!!” alisikika Hamidu akipiga ukulele wa furaha. “Kevo, That’s Step 1, then Step 2 Lulu mikononi mwako unajilia kirahisi mwenyewe!!” Hamidu aliendelea kujigamba na kumtia sifa Calvin. “Harifuu, Jamaa zako ni hatari kinoma!!!” alisifia Calvin. Wakati wanaendelea kuongea ikiwa ni saa saba za usiku tayari, mara simu ya Hamidu inaita “Dogo, tuma ile Advance au yote kabisa Mzigo wenu tunao hapa tayari!!” aliagiza Jimmy “The INVISIBLE”. “Oooh sawasawa, Naonelea kesho tuje nao wenyewe Cash kwa

usalama zaidi!!” alijibu Hamidu. “Basi sawa, Muwe Makini!!” alijibu Jimmy “The INVISIBLE”

Mashauri alipozinduka alijkuta yupo mwenyewe huku amefugwa mikono na miguu yake, na mwili wake umefungwa kwenye Mbuyu. Alipojitalidi kukumbuka ni nini kilichotokea, fikra zikamrejea na akaanza kujiangalia yeye kama yeye akagundua hana uwezo wa kujiokoa kabisa pale. Alipotazama huku na kule aligundua yuko katikati ya Msitu mkubwa sana, na pale alipo aliona hema moja kubwa la kifahari, na pasipo shaka alijua wale waliomteka ndio walikuwa ndani ya lile hema. Alipogeuza macho juu alifanikiwa kuona vibao viwili vilivyo gongewa kwenye ule Mbuyu, kimoja kilionekana kikuu kikuu yaani cha siku nyingi sana, na kingine kilikuwa kipyä kabisa. Kile kikuu kiliandikwa kwa maandishi makubwa mekundu “THE CALVARY” na kile kidogo kiliandikwa kwa maandishi madogo meusi “Operation MJM 006”. Alipojaribu kutafakari yale maneno alipata ufahamu kwamba ile CALVARY inamaanisha sehemu ya MATESO/KIFO, lakini hii ya Operation MJM 006 aligundua MJM ni majina yake matatu yaani Mashauri Jonathan Mkumbo. Kwa hakika aligundua kwamba yupo hatarini sana na hakuja ni nini afanye maana hata sababu ya kutekwa kwake bado hakuwa anaijua. Wakati anawaza hayo na hofu ikiongezeka ndani yake akakumbuka yale maneno ya **Zaburi 27:3 “Jeshi lijapoipanga kupigana nami, Moyo wangu hautaogopa. Vita vijapotokea, Hata hapo nitatumaini”** Baada ya Mashauri kukumbuka andiko hilo ndani yake ukaanza kuumbika ujasiri wa ajabu. Akaanza kunena kwa lugha taratibu taratibu kisha akaanza kukiri **Zaburi 46:1 “Mungu kwangu mimi ni kimbilio na nguvu, Msaada**

*utakaoonekana tele wakati wa mateso*” kisha akakiri tena **Zaburi 17:8** “*Unilinde kama mboni ya jicho, Unifiche chini ya uvuli wa mbawa zako,*”. Mashauri aliendelea kunena kwa lugha kwa muda mrefu zaidi, japo alikuwa akipigwa na upepo na baridi kali ya usiku ule mnene.

Wakati Mashauri amenyamaza kwa ukimya huku akisubiri kusikia kutoka kwa BWANA, mara ghafla Mungu akanza kusema nae kwa Maandiko halikadhalika. Akamwambia sawasawa na Neno langu la **Isaya 41:10** “*usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe, usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu*”. Mashauri alianza kububujika huku akitokwa na machozi mengi, wakati huo Mungu aliendelea kusema nae kupitia Maandiko akimhakikishia ya kwamba atakuwa pamoja nae, Mungu alimpeleka kwenye **Isaya 43:2** “*Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendako katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza*” wakati anashangaa huu mtembeo wa kiMungu akapelekwa tena kwenye **Isaya 54:17** “*Kila silaha itayofanyika juu yako haitafanikiwa.....*”. Mashauri alilia sana kwa furaha.

Kama saa 10 ya usiku Lulu aliyejekwa hapati usingizi kabisa aliona simu yake ikiita kwa namba mpya. Alitaka kusita kuipokea ila mwishoe akaipokea “Uhai wa Mashauri upo mikononi mwako, wewe unawenza kusababisha afe au aendelee kuishi. Ni vizuri usikilize maelekezo Binti!!” sauti ya kikatili ilionekana haina huruma hata kidogo ilimuagiza Lulu. Lulu huku akiwa anatetemeka akajibu kwa uoga “Nipo tayaarii nasii....

kiliza!!” Lulu alianza kuelewa ni kwanini simu ya Mashauri haikupatikana mara baada tu ya kuzunguka nyuma na Yule jamaa baada ya kutoka Ibadani. Sio Manka wala marafiki wa karibu wa Mashauri walijua Mashauri yuko wapi kila Lulu alipowauliza. Na kule kukosa usingizi usiku ule kilimrihidhishia hatari kwa Mashauri. “Ili huyu kijana awe hai, mwandikie Calvin sasa hivi sms kwamba umekubali na mwambie wakati wowote akitaka aje akuchukue, kinyume na hapo Mashauri atauawa. Una masaa manne tu na sio zaidi!!” Sauti ile iliagiza na kukata simu. Lulu alisikia ubaridi mwili mzima, hakuwahi kuwaza kwamba atakuja kuwa chanzo cha mateso na hata mauti kwa Mashauri. Alifikiri hata akienda kuripoti Polisi kuhusu kina Calvin, bado Polisi wasingeweza kumpata kwa haraka Mashauri akiwa hai. “Eeh YESU msaidie!!!” alitamka Lulu kwa sauti. Na alivyokumbuka namna Irine alimhadithia kuhusu ukatili aliofanyiwa na Hamidu, ndio alizidi kuchanganyikiwa. Kuna mda alijikuta chooni bila kujua alikwenda kufanya nini huko, ila wakati anaendelea kubabaika akakukumbua ile **Zaburi 42:5** “*Nafsi yangu, kwa nini kuinama, Na kufadhaika ndani yangu? Umtumaini Mungu;*” Lulu akajipigapiga kifuani akasema kwa sauti kuu ‘NAFSI YANGU USIINAME WALA USIOGOPE, UMTUMAINI MUNGU”

Lulu alipopata utulivu alimpigia simu Manka na Atupele wakutane Chapel asubuhi ile kwenye maombi ya Alfajiri, walipokubaliana kukutana Lulu akanyanyua simu yake akamwandikia Calvin sms “Please Let Him Live, Here I’m for you Calvin!!” kisha akajambia naenda vizuri. Walipokutana Chapel Lulu aliwahadithia kila kitu na kwa pamoja waliingga kwenye

maombi ya Nguvu kwa ajili ya Mashauri, kwa kuwa ilikuwa ni Jumapili walikubaliana wakutane tena kabla ya Ibada kwa ajili ya kuendelea kuomba. Lulu aliporudi Hosteli alishika simu yake na kukuta sms mbili, ya kwanza “Hakikisha leo jioni unaenda kulala kwa Calvin, ili kesho asubuhi tumuachie Mashauri awahi Mitiahani yake!!” hii ilitoka kwa namba nyingine ngeni tofauti na ile iliyompigia. Na sms ya pili ilitoka kwa Calvin ikiandikwa kwa kifupi sana “Prove to Me tonight!!” yaani nihakikishie usiku wa leo. Kwa haraka haraka Lulu alijiona mtegoni, na alijua hawa watu lao ni moja. Na alifahamu akicheza kidogo tu Mashauri anauwawa na haina shaka ye ye atakuwa sababu kubwa.

Saa 12 na nusu asubuhi Jimmy “The INVISIBLE” na Ommy yule Mtesaji walitoka kwenye hema lao kulala, walipozunguka nyuma kwenye Mbuyu wao “The CALVARY” walitaharuki kuona Mashauri bado yuko pale pale ila hana kamba mahali popote. Kwa haraka haraka walianza kujihami kwa kuangalia huku na kule ya kwamba ni nani kamfungua????” Mashauri alicheka kisha akakiri ukuu wa Mungu kama **Ayubu 42:5** inayosema “*Nilikuwa nimesikia habari zako, kwa kusikia kwa masikio; Bali sasa jicho langu linakuona!*” Jimmy na Ommy waliogopa sana hali ile, na waliogopa sio kwa sababu kamba zimefunguliwa ila kwa nini yule kijana hajaondoka pale licha ya kamba kufungulia. Jambo moja wasilolijua ni kwamba Mashauri alipitiwa na usingizi, na aliposhtuka alishangaa kuona yupo pale pale ila hana tena kamba. Wakati anajiuliza nani kamfungua ndipo Jimmy na Ommy walifika pale na kuanza kutaharuki, ndani yake alijua wazi NI BWANA. “Kaka zangu Wapendwa, Tafadhalii nielezeni kwanini mliniteka na kunileta

hana Calvary??!!” Mashauri aliuliza kwa upole na ustaarabu wa hali ya juu. “wewe dogo ni Mchawi, yaani bonge la Mwanga. Upo hapa kwa sababu ya kisa cha mapenzi, Calvin na Hamidu wametulipa kukuteka ili wampate Lulu!!” alisema Jimmy akiwa kama mita 10 kutoka pale alipo Mashauri. Mashauri alijisikia sana kujawa na Nguvu za Mungu ndani yake, tangu alipookoka hakuwahi kuhisi nguvu za Mungu kiasi hiki. Hata siku alipoombewa ujazo wa Nguvu za Roho Mtakatifu kule Mzumbe Sekondari na Mtumishi wa Mungu Brother Kingu, alihisi Nguvu za Mungu ila hii ya leo ilikuwa zaidi. “Naombeni mnifunge tena, ili wakija wanikute nimefungwa. Mungu wangu ni BWANA WA VITA, wala Mimi sina nguvu za kupambana na ninyi” Jimmy ambaye alishazipangia zile Milioni 5 za kina Hamidu bajeti alimuonyeshea Ommy ishara waende wakamfunge tena, Ommy huku bado anaogopa akamfanya Jimmy ishara wakamfunge wote. Hii ilimpa ujasiri wakamsogelea, kila walipomjaribu kumfunga mikono yao ilitetemeka kama mtu aliyeishi baridi kali sana. Baada ya muda walikata tamaa na wakaanza kumuomba Mashauri msamaha, Mashauri akawambia hivi “Mimi, nimechorwa kwenye vitanga vyta mikono ya Mungu, Mimi nalindwa kama mboni ya jicho la Mungu. Kaka zangu hii dunia itapita pamoja na tama zake, bali yeche afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele. Katikati yenu hakuna atakayeishi duniani milele, Tubuni na Mpokeeni Yesu!!” alimaliza Mashauri na kuanza kuondoka zake asijue vizuri anapoenda. Jimmy “The INVISIBLE” na Ommy hawakuamini macho yao juu ya kile kinachotokea, kila mmoja alidhani labda ni ndoto.

“Tumefika Mapinga, tunaelekea wapi??!!” Hamidu alimsms Jimmy. “Simameni hapo hapo niwape maelekezo baada ya dakika 5” Jimmy alimjibu Hamidu kitaalamu. “Yaani leo najilia Mtoto mzuri taratibu bila kelele mwanangu, yaani hapa naona masaa hayaendi na jioni haifiki!!” Calvin aliyeonekana ana furaha sana alijigamba kwa Hamidu, “You’re My Best friend, nisingekubali uendelee kuteseka kisa yule demu!!” Hamidu alijibu kwa majidai. “Wekeni hiyo fedha yote kwa 0752..... weka Milioni 3.5 na kwenye 0715..... wekeni 1.5M majina ni James Onyango na Ommary Mkulima” sms kutoka kwa Jimmy iliwataka waweke ile fedha kwa Mpesa na Tigopesa kwanza. Kwa kuwa walikuwa wanapokea sms toka kwa Lulu hawakuwa na wasiwasi wowote hivyo wakaziweka kwa Wakala, kisha Hamidu akasms Jimmy “DONE”. Jimmy akaandika sms “Mfateni nyuma huyo kijana mwenye baisedhi nyuma yenu!” na kweli walipoangalia nyuma wakamuona mtu mwenye baisedhi na wakaanza kumfata. Baada ya nusu saa walijikuta katikati ya msitu, na kisha Jimmy na Ommy wakatokea, “Huyu Mshamba yuko wapi, nina hamu nae kishenzi yaani!” Hamidu alimuuliza Jimmy kwa mkwara. “Acha wenge dogo, mmetupa kazi ya kushika mchawi, Mchawi katoweka!!” alisema Jimmy kwa hasira. “Acheni Ufala bhana, turudishieni hela zetu basi!!” alitukana Hamidu na kusema kwa jazba. “Dogo jiangalie sana, huo mwili unakupa kiburii eeh!!” alisema Ommy. “Nyie ni Wapumbavu sana, yule Mshamba anawatorokaje??!!” Hamidu aliendelea kubwatuka maneno makali na matusi. Mara Jimmy akamuonyesha Ommy ishara flani halafu akasema “006 MALIZA” Ommy akamrukia Hamidu kitaalamu akamvunja shingo, Hamidu akafa papo hapo. Calvin ye ye aliikuwa kimya wakati wote huu, alipoona Hamidu kafunjwa

shingo na kukata roho, alipiga magoti akaanza kuomba msamaha huku akijikojolea “Jamaaani ..... naombeni msiniue..... nitawapa hela nyingine ipo kwenye gari..... naombeni kaka zangu!!” Jimmy “The INVISIBLE” kuona vile akacheka sana “Ahahahahaha Ahahahahaha hizo fedha ziko kwa wapi??!!” “Zipo kwenye kabegi kadogo garini ni milioni 3 tu, msiniue tafadhali!!” Calvin alielezea huku akiendelea kuwasii sana wasimuue. Jimmy akampa Ishara Ommy akachukue huo mzigo mwingine wa hela, wakati Ommy anafata ule mzigo uliokuwa kwenye gari kama mita 20 hivi, Jimmy akamwambia Calvin “Sitakuua bwana mdogo, zingatia mambo matatu,Moja PASAHAU KABISA HAPA, Mbili FUNGA MDOMO, Tatu UTAONDOKA NA MZIGO WAKO UJUE PAKUPELEKA” alimeza fundo la mate na kisha akaongeza “Dogo, ACHANA na Yule jamaa na MWANAMKE wake, ushauri wa bure wawahili uwaombe msamaha!!” Baada ya hapo wakambebesha Calvin mwili wa Hamidu mpaka kwenye gari yake Rav4, na baada ya hapo wakaenda nae mpaka karibu na lami wakamuacha aende. Wakati Calvin anabeba mwili wa Hamidu walikuwa wanampiga picha za kutosha za ushahidi. Hakika hii ilikuwa siku ngumu sana kwa Calvin tangu amezaliwa, tamaa ya wanawake na ujuaji mwingi ulimponza. Alitamani ardhi ipasuke aingie, alitamani iwe ni ndoto tu ila kila akijaribu kuamka anakuata sio ndoto tena ni uhalsia.

Mashauri baada ya kuondoka pale Mapinga kwa 006 MAFING GANG alianza kutembea bila kujua anapoelekea, njiani aliendelea tu kunena kwa lugha huku akimshukuru Mungu kwa muujiza ule mkubwa katikati ya watu wabaya. Baada ya masaa kama mawili alikuta barabara ya lami, wakati anashangaa asijue

yuko wapi ikapita daladala imeandikwa MSATA – BAGAMOYO. Akilini mwake akajua katika ule muelekeo ni aidha anakwenda MSATA au BAGAMOYO. Mara akapata akili akajigusa mfukoni akagundua ana elfu mbili, bahati nzuri wale jamaa hawakumkagua mfukoni. Alipoona daladala nyingine akaisimamisha aaulizia wapi inaenda, akaambiwa Bagamoyo akapanda. Alipofika Bagamoyo Stendi akiwa amebakiwa na Elfu moja tu akapanda magari ya Bagamoyo – Mwenge, baada ya lisaa na nusu akawa tayari ameshuka Mlimani City na kuanza kutembea kwa mguu kuelekea Chuoni. Kwa hakika alikuwa amechoka sana, huku akiwa na njaa kali maana tangu Jumamosi Mchana hakuwa amekula kitu chochote. Anachokumbuka kuhusu simu yake ya mkononi ni kwamba aliacha kwenye chaji wakati anaenda kipindi cha dini tena akiwa kazima. Hivyo kutopatikana kwake sio kwa sababu alinyang'anywa simu wakati alipotekwa na Jimmy "The INVISIBLE" bali aliacha kwenye chaji. Basi alitembea haraka haraka kwa uchovu mwingi, kwa maana alikuwa amechafuka kila mtu alimshangaa alipoanza kuingia maeneo ya chuoni. Baada ya dakika 15 tayari aliingia chumbani kwake Hosteli, akawasha simu yake na kwenda kuoga haraka haraka. Kisha akachukua hela kwenye begi lake na kuwahi Cafeteria kujipatia chochote, kwa namna alivyokuwa na njaa akasahau tena simu Hosteli.

Lulu aliangalia simu yake ndio kwanza saa 11 na nusu, alikuwa anatetemeka mno asijue ni nini cha kufanya. Akaanza kufikiria labda amdanganye Calvin kwamba yuko kwenye siku zake na hivyo wafanye kesho yake, ila akaona ataambiwa aje hivyo hivyo. Aliwaza mambo mengi sana bila majibu. Alitamani kumuokoa Mashauri, lakini alitamani kuutunza usichana wake.

Baada ya kujiambia “NAFSI YANGU UMTUMAINI MUNGU” mara akapata wazo la kumpigia simu Mashauri. Alitaka kudharau hilo wazo, ila akasema ngoja nijaribu tu, ile kupiga simu ikaita ikaita haikupokelewa. Akapiga kama mara saba hivi bila mafanikio, mwisho akaamua kutuma ujumbe wa maandishi “MASHA, NINAJUA MUNGU UNAYEMWABUDU NA UNAYEMTUMIKIA AMEKUOKOA” baada kama ya dakika 10 hivi sms nikaingia kwa simu yake, “Mungu naomba tu asiwe Calvin!” Lulu akasema kwa sauti. Alipoangalia simu yake hakuamini macho yake kabisa alipoona ni sms kutoka kwa Mashauri inayosema “LULU DADANGU, MUNGU HAKULALA WALA HAKUSINZIA!! NIPO CHUONI” Lulu kwa lile wenge la furaha akapiga kelele kwa sauti AHSANTE YESUUUUU, UMEJIBU MAOMBI YETU, NITAKUSIFU MILELE” Akanyanya simu yake akampigia Manka “Hellew MUNGU AMEJIBU!” wakati Manka anauliza “IMEKUWAJE!!!” simu ilishakatwa. Akampigia tena Atupele “Mtumishi, MUNGU AMEJIBU!!” kabla Atupele hajauliza simu ilishakatwa. Kisha akampigia sasa Mashauri “UKO WAPI SASA HIVI NATAKA NIKUONE??!!”, “Naelekea Chapel Dadangu, Moyo wangu umejawa na Shukrani kwa Mungu!!” alijibu Mashauri. Kabla hajapanda kilima cha CCT – Chapel Mashauri akasikia mlion wa Bajaji Nyuma yake kuhamaki ni Lulu amefika. Lulu leo hakujali ni karibu na kanisa wala kuna nani na nani, alimkimbia Mashauri akamkumbatia kwa nguvu huku analia halafu akasema “Masha, nisamehe, wewe ni mtu mwema, Mimi nimekusababishia matatizo jamani!!” Kwa mara ya kwanza Mashauri anakutana na kumbatio la nguvu la Msichana tangu amezaliwa, haitoshi anang’ang’aniwa kwa muda mrefu ambao

hakutegemea kabisa. Hapa sasa Mashauri alianza kuelewa ni kwa nini alitaka auwawe kwa sababu ya huyu binti. “Imetosha Lulu, Ahsante. Mungu ni Mwema!!” alisema Mashauri huku mapigo ya moyo yanaenda kasi sana. Ile Lulu kumuachia hivi mara paap Atupele na Manka nao wakamvamia huku wakilia kwa furaha. Walipoingia Ibadani Mashauri alipata nafasi na wasaa wa kutoa Ushuhuda juu ya kile kilichotokea jana usiku mara baada ya Ibada. Alielezea pia namna ambavyo Mungu alimuokoa, ila alitumia hekima sana hakusema sababu ya kutekwa wala waliohusika kumteka. Mwisho akaomba kanisa lifungue **Zaburi 18:16,17** “*Alipeleka kutoka juu akamshika, Na kunitoa katika maji mengi. Akaniokoa na adui yangu mwenye nguvu, Na wale walionichukia. Maana walikuwa na nguvu kuliko mimi*”.

# 27

## KIROBA KUNDUCHI!!

Calvin aliendesha gari lenye mwili wa Hamidu mpaka kwake Sinza Mapambano, na kwa kuwa alijua wazi kwamba kesho yake alitakiwa kuwa kwenye mitihani ya UE alipiga akili akaona ni vema amalizane na lile jambo siku hii hii mapema. Alichofanya alichukua simu yake akampigia moja ya madereva wa Bajaji ambaye huwa anamuagiza mara kwa mara. “Hoya njoo kuna dili la maana hapa!! Njoo fasta!” aliongea Calvin. “Hamna noma natimba hapo dakika sifuri tu!!” alijibu yule dereva wa bajaji. Baada ya dakika tano dereva Bajaji alikuja kwa Calvin. “Mwanangu nina kazi ya dakika 20 nataka uifanye halafu nakulipa milioni moja chaap” alisema Calvin. “Acha masihhara bhana, mnajua nyie wasomi mnatuonaga sisi hatuna akili. Dakika 20 unanipaje milioni mimi hiyo hela napata miezi karibu sita aisee weeee!!” alijibu dereva Bajaji anayejulikana kama Mgosi kwa lafudhi ya kigosi. “Acha mawenge bhana, nina mzigo nataka nikupe ukautupe baharini nikupe milioni moja yako chaap!!” alieleza Calvin. “Oooh kwenda kutupa tu, hiyo mimi sijali hata kama ni mtu, nipo mijini kutafuta hela hapa, sijaja kuuza sura” Mgosi alikazia. “Hapo mwanangu shega!! Njoo na mifuko miwili ya salfeti baada ya nusu saa. Halafu nikikupa itabidi utoweke kidogo Jijini walau wiki hivi!” alisema Calvin. “Acha

uoga bwana mdogo, mimi natupa na naendelea kula vichwa vyangu” Mgosi alijibu kwa ujasiri. Baada ya nusu saa Mgosi akaja na mifuko, Calvin akaingiza mwili wa Hamidu kwenye ile mifuko. Mgosi akabeba asichokijua akaenda mpaka kunduchi maeneo ya baharini akatupa akageuza na bajaji yake. Kwa kuwa watu wengi wana tabia ya kutupa mizigo ya uchafu baharini hakuna ambaye kwa usiku huo aliona umuhimu wa kumfuatilia Mgosi juu ya alichokitupa, tena ukichukulia ni usiku wa saa nne. Uzito wa ule mzigo ulimpa wasiwasi Mgosi ila akakumbuka maneno yake ya hata kama huo mzigo ni mtu yeche atautupa tu mbele ya hela. Alipomaliza kuutupa alirudi kwa Calvin akapewa hela yake wakaachana. Usiku huu Calvin hakulala kabisa, kila wakati alikuwa kama anamuona Hamidu anamjia. Ilipofika saa saba akampigia rafiki yake wa chuoni na kumwambia “Mwanangu, nasoma mwenyewe hapa sielewi chochote halafu Hamidu nae sijui alipokwenda na hapatikani. Naomba nije tusome wote na nilale huko huko” “Hamidu mtu wa mademu yule, hachelewi kuwa amefichwa mahali na lishuga mum, Wewe njoo bhana Waziri Mkuu wangu!!” alijibu Charles moja ya marafiki zao Chuoni. Calvin akawasha gari akaendesha mpaka Chuoni, akakutana na Charles wakaanza kusoma tayari kwa ajili ya UE zinazoanza Jumatatu asubuhi. Kila mara Charles aligundua Calvin hayupo sawa kama kawaida yake, na kila alipomuuliza Calvin alisema “Duuuh Mwanangu simuelewi Hamidu kabisa, tangu jana simpati kwenye simu yake ujue!!”.

Mzee Mhina “Mbabe wa Mji” alikuwa amejipumzisha na mkewe sebuleni kwao majira kama ya saa nne asubuhi hivi mara ghafla wakaona BREAKING NEWS kwenye channel ya ITV.

“Mwanafunzi Hamidu Mhina mwaka wa kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam amekutwa ameuwawa na kutupwa pembezoni mwa Bahari kule kunduchi Dar es Salaam, Polisi wanaendelea na Uchunguzi”. Mama yake Hamidu Bi Husna akazimia palepale, Mzee Mhina alilia sana huku anasema “Mwana kuyatafuta, Mwana kuyapata!! Nilikuonya Mwanangu, Iliingilia sikio hili ikatokea lingine. Sina hata haja ya kuhangaiaka kufuatilia aliye kuua, maana hautarudi. Nenda tu!!” Asubuhi baada ya Mtihani wa kwanza TAHARUKI ilipamba Chuoni, watu walijawa na hofu sana. Calvin alilia kama mtoto mdogo huku akisema hajui ni nini kilitokea, Irine alizimia. Polisi walifika Chuoni na kumchukua Calvin kwa mahojiano kituo cha Kati, walipofika nae kituoni walishangaa kuona kuna gari ya serikali ya Waziri wa Nishati na Madini pamoja na gari lingine la BOT. Baadae waligundua kijana ni Mtoto wa kigogo hivyo baada ya lisaa walitakiwa kumuachia haraka ili akaendeleee na Mtihani wake wa mchana, na wasimsumbue mpaka atakapomaliza UE. Lakini pia kwa kuwa aliyeuwawa ni rafiki yake wa karibu mno, wazazi wake waliamua kumuwekea mlinzi wa kumlinda ili asije akadhurika. Mwili wa Hamidu ulizikwa makaburi ya Kinondoni asubuhi ya Jumanne mara baada ya vipimo na uchunguzi. Ilibainika kwamba Hamidu alivunjwa shingo na mtu mtaalamu wa mapigano, hii ilithihirika mara baada ya kukutwa mishipa iliyovunjwa ilivunjwa kwa ustadi wa hali ya juu.

“Lulu, tafadhali naomba UNYAMAZE KIMYA ili KUNILINDA, Nisamehe sana Dadangu. SITAKUSUMBUA TENA, Calvin” hii ni SMS aliyatuma Calvin kwa Lulu kuititia simu ya mtu mwingine. Na alifanya hivi baada ya askari mmoja

kumuambia awe makini sana kwenye mawasiliano yake kwa sasa.  
“Calvin, Pole sana. Sikuchukii na Mimi na Mshauri  
tumekusamehe. Hata na hivyo Mashauri anatamani MUONANE,  
analo jambo angependa akushirikishe!!!” UE Njema!!” alijibu  
Lulu kwa kirefu na kumtakia Heri katika Mitihani inayoendelea.

# 28

## **MBUDYA ISLAND!!**

**W**iki ya mwisho ya kumaliza Mitihani ya UE lilitoka tangazo muhimu sana kutoka kwa viongozi wapya wa UCSF CCT Chapel. Mualiko huo ulikuwa na kichwa cha GOSPEL SHARING FRIENDS PARTY – MBUDYA ISLAND, wanachama wote wa UCSF walitakiwa kuwaalika marafiki zao kwa ajili ya safari ya kwenda kisiwa cha Mbudya kupumzika mara baada ya UE, lakini pia kuwashirikisha juu ya Habari njema za Yesu. Kila mtu alipaswa kuchangia Elfu 20 na alipaswa kuja na rafiki yake mmoja, aidha kutoka ndani au nje ya Chuo ila kikubwa awe Mwanafunzi.

Jioni moja wakati wanatoka Ibadani Lulu, Manka, Mashauri na Atupele wakawa katika maongezi ambayo Lulu ndio aliyaanzisha. “Masha unaonaje ukimwalika Calvin ili upate fursa ya kuongea nae kwa kina kule kisiwani, Mimi nitamualika Irine na Queen nadhani nitalipa zaidi ila for good! Vipi nyie guys??!!” Lulu alimaliza kwa kuwaliza Manka na Atupele. Manka akasema “Masha, how do you see nikimualika Mzava you friend??” “Hilo ni la Utukufu Engineer, limepita!!” Mashauri akajibu. “Ahahahahaha Mimi sijui hata namwalika nani jamani??” Atupele alianza kwa kucheka na kisha akauliza “Yees, nina wazo kama

utalikubali lakini mtumishi Atu!” Manka alisema “Leta wazo Mchaga” Atupele alisema kwa utani. “Nina rafiki yangu anaitwa Gwantwa anasoma kule St Foseph Computer Science, hope ukimualika pia!!” alisema Manka. “Safi kabisa Manka, napenda akili yako. “Dada anapika huyo!!” Mashauri alidakia huku akikumbuka kile chakula alichopika Gwantwa walipoenda kumtembelea kule Luguruni wakiwa na Manka. “Ipo siku nitakupikia na mimi halafu uniambie kama hautanying’ata!!” Lulu akadakia baada ya kusikia huyo Dada kasifiwa mapishi na Mashauri. Mwisho wa mada wakakubaliana Mashauri amualike Calvin, Lulu atamualiaka Irene, Manka atamualika Mzava na Atupele atamualika Gwantwa asiyemfahamu kabisa.

Hatimaye Mitihani ya UE ikaisha Alhamisi, Ijumaa wa kuanza kuondoka wakaondoka, Idadi kubwa ya wana USCF ilikuwa kwenye pilikapilika za Maandalizi ya kuelekea kisiwa cha Mbudya kesho yake. Wanafunzi wa Mwaka wa mwisho ambao ni kama wameshamaliza maana hii ndio ilikuwa Semister yao ya mwisho, waliipania sana hii siku maana kwao ndio ilikuwa kama kusema kwaheri kwa wadogo zao ambao walishirikiana nao vizuri sana Fellowship. Usiku wa Ijumaa Gwantwa alikuja akalala Hosteli na Manka na Mzava alikuja akalala Hosteli na Mashauri. Jioni hiyo kwa mara ya kwanza Atupele alipomuona tu Gwantwa akasema “Kumbe ni Gwantwa huyu jamani” Kisha akaanza kuwakumbusha namna walivyokuwa wanakutana Loleza Girls na Iyunga Boys kwenye Matukio ya UKWATA ya Mkoa. “Unajua Manka kila ulipokuwa unaimba, nilikuwa najiuliza hii sauti niliisikia wapi, Aaah nyie Loleza Girls nyie, nimemuona mwenzako nimekumbuka vile mlikuwa mnatukimbiza kwenye

Uimbaji” Atupele alionekana kuwakumbuka Gwantwa na Manka vizuri. Basi hii siku waliongea mengi na kubadilishana mawazo, mwishowe walitawanyika tayari kwa kukutana kesho kwa GOSPEL SHARING FRIENDS PARTY.

Asubuhi ya Jumamosi vijana zaidi ya 200 walionekana kupendeza sana tayari kwa PICNIC ya Kisiwa cha Mbudya. Wale wa Mjini walivalia kijanja zaidi maana haya ndio mambo yao, wale wenzangu na mimi walijaribu jaribu japo na wao wasiachwe sana, ila wale wapendwa wabishi walivalia suruali zao makoti na tai huku wengine wakiwa na magauni ya vitenge. Kwa mara ya kwanza Mashauri alionekana kuvalaa suruali ya Cadet ambayo haikuwa pana kivile na juu akapiga tsheti yake moja ya maroon ya form six, chini akapiga rabba nyeupe. Lulu, Irene, Gwantwa na Manka walivaalia suruali zao pana za kike zisizowabana sana na blauzi za vitenge kama waliambizana vile, kwa hakika walipendeza sana. Basi safari ya kuelekea Kisiwa cha Mbudya ikaanza. Ilikuwa ni siku kubwa ya furaha sana, watu wengi walikuwa wanashangaa kumuona Waziri Mkuu wa serikali ya wanafunzi DARUSO Calvin alivyokuwa karibu sana na Mashauri. Aliyejua kilichotokea nyuma ya pazia kuhusu kutekwa kwa Mashauri na kuhusika kwa Calvin na hata kifo cha Hamidu, ni Lulu, Manka na Atupele tu. Na kwa pamoja walikubaliana kunyamaza kimya ili kujaribu kuyaokoa maisha ya Calvin.

Walipofika mahali pa kupanda Boti, walipagwa kupelekwa kwa makundi maana idadi yao ilikuwa kubwa na Boti ziliikuwa chache. Ndani ya masaa mawili, vijana wote zaidi ya 200 walikuwa wameshafika wote kisiwani Mbudya. Chaplain Mchungaji Leon Chizza alifungua Sherehe zile kwa Neno la

**Zaburi 24:6 “Hiki ndicho kizazi cha wamtafutao, Wakutafutao uso wako, Ee Mungu wa Yakobo”.** Alielezea umuhimu wa kuutafuta uso wa Mungu kwenye maisha ya Ujana kwa kina sana. Alipomaliza, michezo mbalimbali ilianza, vijana walishindana kukimbia, kukimbia na magunia, kuruka kamba, mpira wa Wavu, Mpira wa Pete, Mashindano ya Kula. Wakati wote huu Nyimbo mbalimbali za Injili za Kiswahili na Kiingereza za vijana zilikuwa zikipigwa, Wataalamu wa mitindo mbalimbali ya kucheza nao walikuwa wakifanya yao. Ilipofika saa saba za mchana vijana walijipatia bites mbalimbali za mapande ya kuku huku wakisindikizia na vinywaji baridi. Wakati huu Mashauri alikuwa akiomba kimoyomoyo akimsihi Mungu ampe maneno machache ya uzima yatakayobadili muelekeo wa maisha ya Calvin. Wakati wanakula Mashauri alijitenga mahali na Calvin na akamueleza juu ya namna hakukuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi kati yake na Lulu zaidi ya ukaribu na urafiki wa kawaida. Alitumia mifano ya kutosha kuhusu Mungu na Maisha, na akamueleza vile Mungu alimuokoa mikononi mwa Jimmy “The INVISIBLE” na Ommy wale watu waliowatuma yeye na Hamidu kumteka na kumtesa. Calvin aliguswa sana na maneno ya Mashauri, lakini pia alishangaa sana hekima na uwezo wa akili alionao Mashauri. Akilini mwake Calvin alijiambia kwamba “USIONE UKADHANI” sawa na ule msemo wa Wazungu usemao “Don’t judge a book by its cover!!” Pamoja na wao kumuona Mashauri kama MSHAMBA FLANI hivi, aligundua yule kijana amejaliwa sana na Mungu.

Baada ya muda watu wote walipokuwa wamemaliza kupata chakula cha mchana, ikaanza ratiba maalumu ya SING

UNTO THE LORD ingekuwa ni Mtaani basi ni KARAOKE, au sisi wazee wa vipindi vya dini basi ni VISHIRIKISHI. Hivyo watu mbalimbali aidha mtu binafsi au kikundi flani cha watu walijitokeza ili kumsifu na kumuabudu Mungu kupitia UIMBAJI. Manka na Mashauri hawakuacha kuitumia fursa hiyo ya kuujenga Ufalme, nao walijitokeza na kuimba ule wimbo ambao waliuimba ile siku pale karibu na uwanja wa Basketball wakati Atupele alipowaona wanaimba akawafuata. Na baadae Loleza Girls Gwantwa na Manka nao pia waliimba pamoja kukumbushia enzi zao wakiwa UKWATA pale Loleza High School. Kiukweli hii session ilivutia na kupendeza sana hasa ukichukulia kwamba vyombo ya muziki vilikuwa vikipigwa LIVE. Mwishoni Chaplain Mchungaji Lewis Chizza nae alikamilisha session hii kwa mtindo wa nyimbo yake ya kufokafoka inaitwa TWENDE ZETU KWA YESU. Hatimaye saa tisa alasiri kilianza kipindi cha mwisho cha Q&A (Maswali na Majibu) ambayo yalilenga mada ya KIJANA MKRISTO NA MAHUSIANO YA KIMAPENZI ambapo Mwl Mgisa Mtete ndiye hasa alikuwa kinara wa mada tajwa. Vijana hapa walijiachia kwelikweli, maswali yaliandikwa na kwa hivyo watu waliuliza bila uoga. Wakati wote huu vijana wote walitulia na kusikiliza kwa umakini Mada hii pendwa, Calvin kuna wakati alisikiliza na kuguswa hadi kutoa machozi. Moja ya kauli iliyomgusa sana ilikuwa ni “Hajalishi wewe ni Nani au Unamiliki nini, Hautafanikiwa kwenye Mahusiano na Mtu mpaka Umejenga Mahusiano thabiti na Mungu kwanza!!”

Mwishoni Mtumishi alitoa nafasi kwa vijana ambao wapo tayari kujenga Mahusiano kwa upya na Mungu wasogee mbele ili aombe pamoja nao. Kilichoshangaza macho ya wengi ni pale

Waziri Mkuu wa serikali ya Wanafunzi yaani DARUSO Calvin John Sanga ndiye alikuwa wa kwanza kukimbia mbele na kupiga magoti huku akilia sana. Pamoja na wengine wengi Irine nae alisogea mbele huku akilia kwa uchungu sana, Lulu na Mashauri walipoona mguso ule wa kiMungu kwa Calvin walisogeleana na kwa pamoja wakaanza kumshukuru Mungu kwa machozi. Cha ajabu kabisa Lulu hakuwa amewahi kunena kwa lugha kabisa, ila ile wameeanza kumshukuru Mungu pamoja na Mashauri kwa ajili ya Calvin, Nguvu za Mungu zikamshukia na akaanza kuomba kwa kunena kwa lugha palepale. Wakati huu watu wakiwa wamesogea pale mbele Manka alikuwa akiwaongoza watu kwa wimbo wa

**“Wanijua vema BWANA, Wanijua vema BWANA,  
Wanijua vema BWANA, Nipo mbeeele zakoo”**

Hakika ilikuwa ni mguso wa aina yake.

Hivi ndivyo GOSPEL SHARING FRIENDS PARTY ilivyomalizika hapa katika kisiwa cha Mbudya. Lakini pia hivi ndivyo mwaka wa kwanza wa masomo uliisha kwa Mashauri, Calvin, Lulu, Irine, Manka, Atupele na wengine, huku ukiwa umegubikwa na visa na mikasa pamoja na shuhuda na Ushindi usio wa kawaida.

# 29

## CHEERS!!

Pembezoni mwa barabara inayotoka Phillips kuelekea Round About ya Kijenge – Njiro, katika Hoteli ya Sabasaba moja kati ya Hoteli tulivu Arusha walionekana marafiki wakubwa wawili walioshibana, Dr Stephen Mollel na Engineer Joseph Lukumay. Marafiki hawa walioshikana walikuwa wakiongea mambo mbalimbali ya kazi zao, biashara na hatimaye familia. Wakati Dr Stephen Mollel yeeye alikuwa Daktari Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha yaani Mount Meru, pamoja na kumiliki miradi kadhaa ya Mashamba na Maabara zinazofanya vizuri sana Jijini hapo. Rafiki yake Engineer Joseph Lukumay yeeye alikuwa Mkurugenzi wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano yaani AICC, lakini pia alikuwa na Kampuni kubwa sana ya Ujenzi. Watu hawa walikuwa wanapatana na wanapendana sana. “Mollel, do you know my last-born Prince Lukumay is a little older than your daughter Lulu??!!... almost 3 years!!” aliongea Engineer Lukumay kwa umakini mkubwa. “Then, what do you mean??!!!” aliuliza Dr Mollel kwa mkato mno. “Ahahaahahaha Mollel you have my point already ahahahahaha!!” alijibu Engineer Lukumay huku akicheka sana.

Prince Lukumay Jr kama anavyoitwa na Baba yake Mzazi Engineer Joseph Lukumay ni mtoto wa mwisho katika familia yao. Yeye alibahatika kwenda China na kusomea Shahada ya Software Engineering, na baada ya kumaliza akaenda tena Malaysia kwa Masters Degree ya mambo ya IT SECURITY. Kiukweli akiwa na umri mdogo tu wa miaka 24 alipata bahati ya kuajiriwa na Bank ya Dunia kama Mtaalamu wa mambo ya Usalama wa kimiradhi na kimawasiliano. Na kituo chake cha kazi ilikuwa ni Nairobi nchini Kenya, ijapokuwa kila wikiendi alionekana Arusha kwa jinsi walivyokuwa wameshibana na Baba yake.

Sasa kwa kuwa wazee hawa wasomi na marafiki wa miaka nenda rudi walikuwa wamepatana sana, na kwa namna walivyokuwa wanawafahamu vijana wao vizuri walitamani wawe pamoja kimaisha. Yaani Prince Lukumay Jr na binti Lulu waoane na kuwa mke na mume, Dr Mollel na Engineer Lukumay waliamini hili lingefanya urafiki na ukaribu wao kudumu zaidi na zaidi. “I know my daughter very well; she won’t disappoint again!!” alisema Dr Mollel kwa kujiamini. “Why again then??!!” alihoji Engineer Lukumay. “It was my dream for her being a Doctor like me since her childhood, but unfortunate she went for Law!!” alisema Dr Mollel kisha akaongezea “In this one, at least she will make me happy!”. “My son is my best friend; He will take her for life!!” alisema Engineer Lukumay. Kisha kwa pamoja wakagonga cheers wakaendelea kupiga mvinyo kama kawaida yao.

# 30

## SUPPLEMENTARY CASE

Lulu hakuamini macho yake wakati anaangalia kwa Mtandao wa Chuo Matokeo yake ya Semister ya pili. Alikuwa amepata A na B+ kozi zote za Semister hiyo isipokuwa kwa kozi za Dr Kimaro, moja alikuwa na Sup na nyingine ilionyesha Incomplete. Wakati amepaniki tayari aliporudi juu kuangalia na Matokeo ya Semister ya kwanza alishangaa kukuta zile kozi mbili za Dr Kimaro alizokuwa amepata A zote amewekewa C. Alijua wazi hizi ni salamu za Dr Kimaro kwake juu ya kile alichomwambia kwamba Shahada yake ipo mikononi mwa Dr Kimaro. Na kwa kuwa Lulu alikataa kutoa ushirikiano kabisa wa kimapenzi kwa Dr Kimaro, Dr Kimaro alianza kumtumia salamu kupitia matokeo haya ya Semister ya pili. “I’m a Law student and I’ll stand for Justice” alijiambia Lulu na kujitia moyo kama vile hakuna kilichotokea.

Baada ya kumshirikisha Mashauri na marafiki zake wengine wa Fellowship, walikubaliana kushirikiana kwa maombi ya mfungo ili kumsihii Mungu awape hekima na wepesi katika hili. Wakati huu wote Lulu alijizuia sana kutowasiliana na Dr Kimaro maana aligundua angemuandikia maneno ya lawama ambayo yasingekuwa mazuri. Dr Kimaro yeye alikuwa ametulia tuli huku

anasikilizia juu ya nini kitatokea, aliamini Lulu hakuwa na chochote cha kumfanya. Kwa miaka yake yote ya Uhadhiri yeote anayejidai kuleta ugumu kutoa ushirikiano wa kimapenzi kwake kama anamtaka, basi hii ilikuwa fimbo ya mwisho ya kumpiga. Wengi walisurrender baada ya kuwapiga na fimbo hii ya matokeo, na wale waliojidai kuendelea kukaza waliishia kudisko. Kuna wachache waliojikakamua kukata rufaa ya matokeo, nao waliishia kushindwa vibaya na Daktari huyu gwiji wa Sheria. Kwa kifupi Dr Kimaro alikuwa kashindikana, na hatari mbaya kuhusu yeche kila Semister alikuwa na kozi zaidi ya moja anayofundisha kwa miaka yote mine ya Sheria.

Na kwa Lulu alitegemea mara tu baada ya Matokeo kuachiwa Lulu angemtafuta na kumlalamikia, alijambia akimtafuta tu akiwa kakubaliana na ushirikiano basi naenda kumtafunia huko huko Arusha. Dr Kimaro alishangaa wiki ya kwanza imepita, mara ya pili nayo ikapita Lulu hajamtafuta. Alivyoona hivyo akajua Lulu lazima alikuwa na wazo la kukata rufaa ya matokeo, na bado Dr Kimaro akasema hapo ndio nitamuumbua huyu binti mchana kweupe “Angekubali tu Yaishe” Mara baada ya Maombi pamoja na Mashauriano na Wapendwa, Mashauri na marafiki zake wa karibu, Lulu aliamua kukata rufaa ya matokeo pamoja na hilo kwenda kumshtaki Dr Kimaro kwa Dean of School of Law juu ya tabu yake ya kumtaka rushwa ya Ngono.

Dr Stephen Mollel alionekana akiwa na mawazo sana, lengo lake ni alikuwa anawaza ni kwa namna gani atamwambia binti yake wa pekee Lulu mwenye miaka 20 sasa juu ya ule mpango wake aliokubaliana na Engineer Lukumay. Wakati

anasuasua ni kwa jinsi gani atamwingia Lulu ili amuelezee na akubaliane na mpango wao huo wa kirafiki. Lulu akaja Mpaka pale Baba yake alipokuwa, “Dad, Sorry!” alisema Lulu, “Welcome My Queen, I’ have been thinking about you!!” alisema Dr Mollel. “Ooow that’s awesome, but WHY??” alifurahia Lulu na aliuliza sababu. “Hope you understand you are the one and only child in this precious family, just your future!!” alisema Dr Mollel kitaalamu sana kisha akapotezea “Tell me my Queen!!” Lulu akameza fundo la mate na kisha akasema “Dad, I have to go Dar es Salaam tomorrow. There is problem to fix in my results!” alisema Lulu bila kuonyesha kama tatizo lilikuwa kubwa sana. “Hope its not big problem honey!!” akasema Dr Mollel, “sure Dad, three days will be very enough!!” akasema Lulu.

Kwa kuwa ilikuwa Jumapili mchana, Dr Mollel akanyanya simu yake na kumpigia Wakala wa Ndege za FAST JET, na kufanya booking ya tiketi ya ndege kwa ajili ya Lulu kwenda na kurudi Dar es Salaam. Na Jumatatu asubuhi ya saa nne tayari Lulu alikuwa ofisini kwa Profesa Ruechungwa Dean of School of Law. Alielezea mchakato na kisa kizima juu yake na Dr Kimaro, lakini zaidi aliomba Kamati ya Rufaa kumuita na yeze atatoa ushahidi wote wa mashtaka yake juu ya Dr Kimaro. Hatimaye Prof Ruechungwa Mzee huyu wa hekima na anayependa sana wanafunzi na kusimamia haki zao, kiasi cha kuchukiwa na Wahadhiri wengine. Mzee huyu mbobevu wa sheria za kimataifa alionekana kumuelewa Lulu vizuri, na alipoangalia muonekano na uzuri wa Lulu aligundua lazima kuna asilimia kubwa ya ukweli juu ya mashtaka haya. Hata na hivyo haikuwa mara ya kwanza kwa wasichana kuleta mashtaka juu ya kutakwa

kingono na Dr Kimaro, japo walipotakiwa kutoa Ushahidi (Evidences) wote waliishia kujiumauma na kumfanya Dr Kimaro kushinda kirahisi. “My Daughter, are you sure you have clear evidences??!!” aliuliza Profesa Ruechngwa kwa upole sana. “Absolutely Yes Sir, I have them and more enough I have God!!” alijibu Lulu kwa ujasiri mkubwa sana. Siku ya Jumatano ndio ilipangwa Kamati ya Rufaa iliyosheheni Madocta na Maprofesa pamoja na Waziri wa Elimu wa serikali ya wanafunzi kukutana ili kutatua kesi mbalimbali, hivyo washtaki na washtakiwa wanaitwa ili kupewa nafasi ya kutoa maelezo.

Siku ilipowadia asubuhi na mapema Lulu alimpigia Mashauri simu na wakaomba pamoja. Walishangaa sana Mungu aliwaongoza kuzitunza zile sms za matisho za Dr Kimaro kwa Lulu wakati ule wa likizo ya Semister ya kwanza, lakini pia ile akili ambayo Mashauri alimshauri Lulu ya kumrekodi sauti Dr Kimaro alipomuita ofisini na kumtisha pia. Hatimaye Lulu akaondoka kuwahi Chuoni tayari kwa kesi.

Ilipofika wakati wa kesi yao, Lulu akaitwa kwanza atoe maelezo na atoe ushahidi mezani. Kisha Dr Kimaro pia akaitwa alipoulizwa anamfahamu Lulu akasema “Not sure, I guess so!” “Why not sure Dr??!!” alihoji Profesa Ruechungwa. “As you know I teach thousands of students, its hard to know everyone!!” alieleza Dr Kimaro. “Can we see her final Exams please??!!” aliuliza Profesa Ruechungwa, “Here they are!” alionyesha kwa mkono Dr Kimaro pale alipoiweka Mitihani ya Lulu. Kamati ikaichukua na baadhi yao wakaanza kuipitia huku kesi ikiwa inaendelea. Hatimaye Lulu aliruhusiwa aanze kutoa ushahidi wake, kwa heshima kubwa akamuomba Dr Kimaro ataje namba

zake za simu. Dr Kimaro akataja, Kisha Lulu akazipiga zikaita huku kioo cha simu yake kikionyesha jina Dr Kimaro, Lulu akaanza kuwaonyesha zile sms za matisho ambazo Dr Kimaro alimtumia wakati walipokwa wanawasiliana. Na baada ya hapo Kamati ilishangaa umakini wa huyu binti pale alipoweza kumrekodi sauti Dr Kimaro walipokuwa wanafanya maongezi ofisini kwake. Dr Kimaro hakuamini ujasiri wa yule binti na namna alivyoweza kumkamata kirahisi vile, na kumdhalilisha mbele ya kamati. “I am very sorry Dr Kimaro, but this is not fair. TENDA HAKI!!” alisema Lulu wakati anamalizia kuwasilisha ushahidi wake mbele ya Kamati. Alipomaliza tu Profesa Ruechungwa akainuka kutoka alipokaa, akamuomba Dr Kimaro ampe simu yake. Alipompa Profesa akamwambia Lulu ataje namba zake za simu, kisha akazipiga kwa kutumia simu ya Dr Kimaro La hasha likatokea jina la “Masai Mrembo 1<sup>st</sup> Yr!”. Profesa akanyanya simu na kuonyesha Kamati, kisha akaomba wale Wataalamu waliokuwa wanapitia mitihani waleti taarifa. “This girl is geneus, She diserve ‘A’ ” walihitimisha wale Wataalamu baada ya kupitia Mitihani ya Lulu. Kisha Mwenyekiti wa Kamati ile akatoa maamuzi ya Kamati ambayo moja, Yalimtaka Dr Kimaro kumuomba Lulu msamaha na kumbadilishia Matokeo yake haraka. Mbili, Dr Kimaro hakuruhusiwa tena kusahisha Mtihani wowote au Kazi yoyote ya Lulu mpaka anamaliza Chuo. Hivi ndivyo Lulu alipata Ushindi wa Ajabu mbele ya Mhadhiri mahiri Dr Kimaro.

# 31

## QUEEN MAUTINI!

**M**aisha ya mwaka wa pili ndani ya Chuo yaliendelea vizuri sana, Calvin na Irine waliendelea vizuri maisha ya kuukulia wokovu na kujengeka kiimani. Calvin aliwatumukia Wanafunzi wa chuo Kikuu cha Mlimani kama Waziri wao Mkuu kwa Uadilifu na Weledi mkubwa sana. Hii ilisababisha Chama cha OCM ambacho ndicho kilikuwa kinatawala kutopata shida ya mgombea Urais wao kwa awamu hii, Uchaguzi ulipofika Calvin John Sanga alipita kwa kura nydingi mno kuwa Rais wa DARUSO. Alimuomba sana Mashauri awe mmoja kati ya washauri watano wa Rais, Mashauri akagoma kabisa. Alipoona Calvin anamsisitiza sana akaamua aende kwa Baba Mlezi Chaplain Rev. Lewis Chizza ambaye alimsisitiza kukubaliana na wito huo mkuu. Hivyo Mashauri akawa moja kati ya Washauri wa Rais wa DARUSO Calvin John Sanga. Wakati wa uongozi wa Calvin kama Rais wa DARUSO ndio wakati uliacha alama pamoja na kuleta mapinduzi makubwa kwa DARUSO. Pamoja na Calvin kuwa Rais mdogo zaidi kuliko wote katika historia ya DARUSO, lakini mpaka leo ndio mwenye rekodi nzuri kuliko viongozi wote waliopita.

Na kwa kuwa Calvin alipata bahati ya kuwa Rais akiwa mwaka wa pili, bado alipata fursa ya kuchaguliwa tena alipokuwa mwaka wa Tatu kuwa Rais kwa awamu nyingine. Na katika awamu zote mbili za Uongozi wake kama Rais wa DARUSO Calvin aliendelea kumtumia Mashauri kama mshauri wake mkuu. Kila wakati Calvin akikumbuka aina ya Upendo alionyeshwa na Mashauri na Lulu baada ya kuwatendea Ubaya uliopelekea rafiki yake kipenzi Hamidu kuuwawa, huwa inampa kuamini kwa habari ya Upendo wa Mungu usiopimika.

Queen mara baada ya kushinda lile Taji la Miss Mlimani, alifahamiana na wakubwa na watu maarufu Jijini Dar es Salaam. Kupitia ulimbwende wake wa Miss Mlimani, akashiriki tena Miss Kinondoni na kushinda kabla ya kuingia Top Five ya Miss Tanzania. Kutokana na harakati zake hizo alijikuta anashindwa kubalance na Chuo, na hatimaye akaacha Chuo. Na kwa kuwa anapoziona hela huwa hajui kusema hapana, mwishowe alijikuta anaandamwa na magazeti ya Udaku na kuchafuliwa sana. Hata hivyo Queen alikuja kuugua ugonjwa usiofahamika japo wengi walisema ni UKIMWI, hiyo ikampelekea kusafirishwa na kwenda kuugulia kwao KASULU – KIGOMA. Baada ya miezi 6 taarifa zilisambaa kwamba Queen alifariki dunia.

# 32

## NAMBALA, TENGERU

**M**waka wa Tatu Mashauri alifanikiwa kupata nafasi ya kufanya Field Makao Makuu ya TANESCO Mkoani Arusha. Hii ilitokana na uwepo wa Mjomba wake Mr Makalla ambaye naye ni moja ya waajiriwa wa siku nyingi katika Shirika hilo. Hivyo baada ya kufunga Chuo Mashauri alienda Singida kwenda kumjulia hali Mama yake Bi Wankembeta aliyekuwa mgonjwa sana, baada ya hapo alipanda basi la Mtei na kuja mpaka Arusha. Mjomba wake Mr Makalla alimpokea akiwa na gari yake Toyota Pickup, na kisha safari ikaanza kuelekea maeneo ya Nambala – Usa River anapoishi Mjomba wake. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kabisa ya Mashauri kuja Jijini Arusha, hivyo alikuwa na mengi ya kujifunza. Gari ile aina ya Pickup ya Mjomba Makalla alielekea mpaka Mianzini na kisha kukunja kulia kufuata barabara kuu ya kuelekea Moshi, gari iliendelea na ilipofika maeneo ya Tengeru ikaingia mkono wa kulia kufuata barabara ya kuelekea Chuo cha Mifugo Tengeru. Baadae ikaingia ndani ya eneo la Chuo na kuendelea na barabara inayopita ndani ya Chuo hicho mpaka kuikuta lami kidogo ya kuelekea kilipojengwa sasa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela. Kisha Mjomba Makalla akaiacha barabara ya Mandela na kuifuata

barabara ya kuelekea maeneo ya Mbuguni, baada tu kama ya dakika 5 walifika nyumbani kwa Mjomba Makalla. Wakati wote huu Mashauri alikuwa akimsikiliza kwa makini Mr Makalla alipokuwa anajaribu kumuelezea kuhusu Arusha. Hata na hivyo Mjomba Makalla aliamua kuishi Nambala kwa sababu ya shughuli zake za Kilimo na Ufugaji. Hapa eneo la Nambala Mr Makalla alikuwa na eneo la hekari 15, ambapo alilima Mahindi, Mihogo na Maheragwe. Lakini pia alikuwa akifuga Ng'ombe wa maziwa, Mbuzi na Nguruwe wa kutosha. Mashauri wakati anakuja Arusha aliwasiliana na Lulu ambaye pamoja na kwamba alijua Mashauri angekuja field Arusha, alifurahia sana kupata walau wasaa wa kuwa na Mashauri pamoja likizo hii. Lulu moyoni mwake alikuwa na jambo zito sana na alidhamiria kwamba ni lazima atumie likizo hii kulitoa moyoni. Field hii kwa Mashauri ilikuwa nyepesi sana, maana kila asubuhi walitoka pamoja na uncle Makalla wakapitisha maziwa maeneo mawili matatu kwa gari yao, na kisha wakawasili kazini. Na kila jioni baada ya kazi walipitia vyombo vya maziwa na hela na kisha wakarudi nyumbani. Mashauri alifurahi sana na kujifunza ujasiriamali huu wa Mjomba wake wa kufikia Mr Makalla. Mr Makalla sio ndugu wa Mama yake na Mashauri, japokuwa ni jamaa ya Ukoo mmoja kwa mbali lakini pia wanatoka kijiji kimoja kule Singida. Ilikuwa ni Mungu tu likizo flani walikutana Singida wakafahamiana na kupeana namba za simu, ndio maana ikarahisisha yote haya.

# 33

## PENZI PENZINI!!

Lulu aliamka akiwa na uchovu mwinci sana, akiwa anajinyooshanyoosha kitandani mara ghafla SMS kutoka kwa Mashauri iliingia kwa simu yake “We have been Friends for three years, I think its very enough!!”. Baada ya Lulu kuona ule ujumbe alichanganyikiwa, akaanza kukumbuka SMS ya jana yake aliyomtumia Mashauri akimueleza analo jambo moyoni mwake na angelipenda Mashauri alitambue. Na alivyoona Mashauri ameamua kuvunja Urafiki wao kwa kumuvisi vibaya. Moja ya mambo yaliyomchanganya sana Lulu, ni tabia ya Mashauri kutokuonyesha kama ana hisia zozote za kiume. Na hiyo haitoshi, mibili Mashauri hajawahi hata siku moja kuongelea mambo ya Mahusuano, Uchumba au Ndoa. Daima Mashauri anaongelea Mungu, Huduma na Shule basi. Hii ilimuweka Lulu kwenye sintofahamu nyingi, “Miaka mitatu jamani hata dalili ya mbali tu kwamba ananipenda hamna, kila siku ni Dada Lulu Dada Lulu!!” Lulu alijiongelesha akilaumu ukimya wa Mashauri. Halafu Lulu akajambia tena “Ngoja ninyamaze kimya, nione ataandika nini tena!!” Alipokaa baada ya muda ikaingia SMS kutoka kwa Mashauri tena “Also we have been sister and brother in Christ for three years, to me that’s very enough!!”. Hii ilizidi

kimchanganya Lulu ila akaamua kunyamaza tena ili aone mwisho wa hizi jumbe. “Lulu, We have been through a lot together. Those moments determine our strength as ONE!!” SMS nyingine kutoka kwa Mashauri. Hapa sasa Lulu alianza kuhisi nywele kichwani na vinyweleo mwili mzima vinasimama, ama kwa hakika kuna kitu alikuwa anasubiria kitamkwe. Na kweli bila kuchelewa SMS toka kwa Mashauri ikaingia “Lulu, I’m in Love with you. I’m so sorry!!”. Baada ya Mashauri kuandika ile SMS ya mwisho akazima simu, asingependa kuona kwa haraka atakachojibiwa. Maisha yale yote hakuwahi kumwambia hivyo msichana yeoyote, kwa hakika aliogopa sana, hasa ukichukulia namna wanavyoheshimiana na Lulu. Huku Lulu hakuamini anachokiona, kuna muda alidhania pengine Mashauri kaibiwa simu nini ama kuna mtu anamuandikia ule ujumbe. Ila akakumbuka Mashauri yupo Nambala kwa Mjomba wake, maana ilikuwa wikipendi na kikawaida Jumamosi huwa haendi field kule TANESKO. Alizidi kushangaa namna Mashauri alivyomuandikia maneno matamu machache, na hasa ukichukulia kwamba yeye mwenyewe alishadhamiria kuyatoa ya moyoni japo kwa msichana huwa inakuwaga ngumu sana kwa tamaduni zetu. Lulu nae aliamua sasa kuweka madeko ya kisichana kidogo, kwanza akakaa masaa matatu hajajibu kitu bila kujua kwamba na huku Mashauri alikuwa amezima simu. Alivyoona Mashauri haandiki kitu tena, akajambia mimi ni mwanasheria bhana, ngoja nimchallenge kidogo. “Mashauri My Brother, Ahsante kwa SMS zako japo sijakuelewa exactly what do you mean aisee????!!” aliandika Lulu SMS kwa mkwara. Mashauri ile anawasha simu tu akakutana nacho, mapigo ya moyo yalimuenda mbio sana halafu akajambia “Nimeshalivuruga, hivi niliomba sawasawa kweli!!” baada ya

robo saa Mashauri akaamua kujibu “Lulu, Am so sorry once again, what I mean is I’d like you being my wife. That’s all!!” alipomaliza kuituma hii SMS Mashauri alijilaumu sana, “Duuu bora nisingetuma, nimeingiwa na nini jamani!!” Mwisho wa siku Lulu akasema wala isiwe tabu akaamua kuutendea haki moyo wake, akaandika maelezo marefu ya tangu anamfahamu Mashauri. Akaeleza namna alivyokuwa anatamani sana ule muujiza wa kuishi na Mashauri kama mume wake, na vile alivyopambana kutokumfungukia Mashauri kwa miaka yote mitatu ya chuoni. Kisha akasema at laest mwaka wake wa nne wa sheria utakuwa mwepesi chuoni. Akamalizia chini “From the very first day I was in love with you, I’m in love with you and I’ll always be in love with you Engineer Masha!!” Mashauri baada ya kusoma ule ujumbe hakuamini macho yake, alipiga magoti na kumshukuru Mungu. Hivyo ndivyo mapenzi ya wawili hawa yalianza.

# 34

## TOM BOY PENZINI!!

**J**umapili, mchana wa saa nane gari aina ya Rav4 ilisimama maeneo ya Tengeru na kisha Mashauri alionekana kupanda lile gari. Kumbe Lulu alikuwa anaendesha gari ya mama yake

Bi Suzan na mchana huu Lulu na Mashauri walikubaliana kwenda Moshi kumtembelea Manka nyumbani kwao. Wakiwa wawili garini waliongea mambo mengi kuhusu Maisha na familia, kiukweli walifurahia sana kule kuwa pamoja na hasa wakimuomba Mungu afanikishe safari yao hiyo ya Mahusiano waliyoianza.

Walipofika Moshi Mjini walinunua vitu viwili vitatu kama zawadi maana walikuwa wanafika nyumbani kabisa kwa kina Manka kule Fukeni. Baada ya manunuzi wakaanza safari ya kuelekea Kiboroloni, lakini walipofika YMCA walitakiwa kumchukua Mzava yule rafiki yake Mashauri anayesoma St Joseph. Na hapo sasa Mzava akaanza kumuelekeza, walipofika kwa Alphonsi kabla ya Kiboroloni Mzava akamuelekeza Lulu aingie kushoto. Hapo waanza kupanda kuelekea Mbokoni wakapanda mpaka Kiwalaa na hatimaye Saoni na mwishoni juu sana wakafika Fukeni nyumbani kwao Manka karibu sana na yalipo makazi ya Mangi Mlatie wa Mbokomu. Mashauri licha yeye na Lulu kushangaa mandhari ya mlimani kule Mbokomu, walishangaa mno imekuwaje Mzava mpare wa Same amewaelekeza njia yote mpaka kufika kwa kina Manka. Kwa kuwa Mashauri alijua Mzava hajazoeana na Lulu aliamua kukaaa kimya bila kuuliza ila akaliweka moyoni.

Walipofika ilikuwa furaha kubwa sana kwa familia, vijana hawa wanne walikaa nje na kuongea mengi huku wakila kiburu (Chakula cha kichaga) pamoja na maziwa mazito ya mgando. Waliongea mengi kuhusu shule, maisha na kuhusu Mungu. Walitupiana utani wa hapa na pale na wakacheka sana kwa furaha. Hatimaye Mashauri akawaomba awasilishe jambo, “Marafiki

zangu Mzava na Manka, watumishi wenzangu wa Mungu. Mimi na Lulu tumeonelea ni vema kuanza kwa urasmi safari ya Mahusianao ya Urafiki kuelekea Ndoa. Mtuombee tafadhali!!” alimaliza Mashauri wakati huo Lulu anaonaona aibu. “Mmmh masikio yangu yamekusikia au naota!” alisema Mzava kwa utani, kisha akaongezea “Kwa utulivu wako Brother unastahili huyu mrembo, Congrats!!” huku anampa mkono. “Yaani mimi nilijua tu, tangu ile siku pale Cafeteria mmeshikana mikono nikahisi kitu. You deserve 100%” alisema Manka. Unajua kikawaida Mzava ni mtu mwenye masihhara sana, sasa kwa yaleyale masihhara na yeche akasema “Ndugu zangu mimi nina jambo la kuwashirikisha. Najua mnashangaa nimepajuaje huku kote ila ukweli ni kwamba mimi na Manka tunaelekea kukubaliana kuanza safari ya Mahusiano kuelekea ndoa” halafi akakoho kidogo kisha akasema hivyo hivyo kimasihara “Oooh nimesahau mtuombee tafadhali!!” wote wakaangua kicheko sana huku Mashauri na Lulu wakidhania ni utani. “Guys ni kweli, we’re in early stages za Mahusiano, hope we will make it!!” Manka akaongea sasa akiwa serious. Kisha Mzava akasema “Kama hawaamini waache, ili kuwahakikishia nyie mtarudi na gari lenu kisha mimi nitashuka zangu baadae na toyo!!” Wote wakacheka sana kwa sauti, kwa hakika ilikuwa siku nzuri sana.

# 35

## BAHATI YA MTENDE!!

“Hello, Wewe ni Mashauri Jonathan Mkumbo?!!” ilisikika sauti nzito ikiuliza kwa simu. “Ndio, Mimi ndiye!!” alijibu Mashauri kistarabu sana. “Naongea kutoka CSI Electrical International Company hapa Dar es Salaam, najua hukuwahi kuomba kazi hapa ila kampuni imeridhishwa na matokeo yako na inakuomba kufanya nayo kazi tafadhalii!!” alitoa maelezo yule mtu wa upande wa pili. “Nashukuru sana, nawafahamu vizuri nipo tayari, nasubiri maelekezo!!” Mashauri alijibu huku anatetemeka hakuamini ule muujiza maana ni jana tu alitoka Dar es Salaam kuja Singida mara baada ya kumaliza Mitihani yake ya mwisho.

“Lulu, I go back to Dar. BWANA AMETENDA, Nimeitiwa kazi na Kampuni kubwa ya Umeme ambayo hata sikuomba!!’ alisema Mashauri baada ya kumpigia Lulu simu. Hivi ndivyo Mashauri alipata kazi hata kabla ya Matokeo yote kutoka. Alipanganya kufanya kazi Makao makuu ya Kampuni kwa Tanzania ambayo yapo Dar es Salaam hapo hapo.

Ilipofika siku ya Graduation, Mashauri alitangazwa kuwa mwanafunzi kinara wa Electrical Engineering na Engineering kwa ujumla, na Lulu pia akatangazwa kuwa mwanafunzi kinara wa Sheria. Calvin pia alipewa tuzo ya heshima ya Uongozi kutokana na namna aliongoza DARUSO kwa mfululizo katika mwaka mmoja wa Uwaziri Mkuu, na miaka miwili ya Urais. Hii ilikuwa siku kubwa sana kiukweli japo ilikuwa siku mbaya kwa Dr Mollel, maana hii ndio siku Lulu aliamua kumtambulisha Mashauri kwa wazazi wake huku akisindikizia na ushuhuda wa maisha yao ya Chuo. Na mwishoni akasema “This is a man of My Destiny!”. Dr Mollel alichukia sana kitendo cha mtoto wake wa pekee kumdisappoint kwa mara nyingine tena. Hakujua angetoa maelezo gani kwa rafiki yake Engineer Lukumay. Hata hivyo Engineer Lukumay alinyamaza kimya kutokuongelea ile ishu baada ya kugundua kuwa tayari kijana wake Prince Lukumay Jr alikuwa na mahusiano na Binti mmoja mtoto wa Waziri kule Kenya ambaye wanafanya nae kazi World Bank. Mwisho wa siku sio Dr Mollel wala rafiki yake Engineer Lukumay aliongelea tena suala la vijana wao kuoana.

Wakati Mashauri anafanya kazi CSI ofisi zao zilikuwa Mlimani City, Lulu yeye alikuwa anafanya kozi maalumu kule Law School ili kuwa Wakili. Vijana hawa walijitahidi kuishi

maisha ya ushuhuda na baaada ya Lulu kufaulu vizuri sana Law School. Mashauri na Lulu walifunga ndoa takatifu katika kanisa la KKKT Ilkiranyi kule Arusha, na kufanya sherehe kubwa sana katika Ukumbi wa LUSH GARDEN uliopo maeneo ya Sakina kama unaelekea Ngaramtoni. Usiku wa Harusi yao ulikuwa ni usiku mwanana wa kihistoria, kwa mara ya kwanza Mashauri anauona mwili wa Msichana ukiwa utupu ambaye ndiye mke wake, na Lulu anauona kwa mara ya kwanza mwili wa Mvulana ukiwa mtupu amba ni wa mume wake Mashauri. Asubuhi na mapema, wahudumu wa Hoteli waliolala usiku wa kwanza wa ndoa, walishangaa mno kukutana na mashuka yamejaa damu. Waliaambiana karibu Hoteli nzima, kiasi kwamba wakaamua wawasubiri wakitoka tu wawapongeze kwa kuwapigia makofi ya kutosha. Wakati Mashauri na Lulu wanatoka kwenda kupata Breakfast na kupunga upemo walishangaa kuona kila mhudumu anawapigia makofi, wao walidhani ni utaratibu wa kawaida kwa Honeymooners kwenye hii Hoteli. Mpaka baadae mmoja wa Wahudumu alipowaambia ile tafsiri ya kwamba ni kwa sababu waligundua wamejitunza ndio maana wakawapongeza. “Huwa tunapokea Honeymooners wengi hapa, lakini kwa miaka mingi hatujawahi kushuhudia jambo adimu kama hili!”

# 36

## **MSHAMBA ULAYA!!**

**K**wenye kiwanja cha ndege cha Julias Nyerere Dar es Salaam, alionekana DC Mteule Calvin John Sanga ambaye ndio kwanza aliteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha. Calvin alionekana akiwasindikiza Wapendanao wawili Uwanjani hapo, sio wengine bali ni Engineer Mashauri Jonathan Mkumbo na Mke wake kipenzi Advocate Lulu Mollel Mkumbo.

Kampuni ya CSI ilimteua Mashauri kwenda Oxford University Nchini Uingereza kusomea Masters of Electrical Engineering In Power Plant, lengo lao lilikuwa ni kumuandaa kuwa Mtaalamu wa mitambo mikubwa ya Umeme. Mashauri alipokubaliana na ile fursa walishirikiana na Dr Mollel na kwa bahati Lulu nae akapata ufadhili wa kwenda Oxford University pia kufanya Masters of Law In Human Rights. Na leo ndio haswa Advocate Calvin John Sanga Mkuu wa Wilaya ambaye hajaapishwa bado, alikuwa akiwasindikiza wawili hao Airport.

“Hey!!! MSHAMBA FLANI hivi ALL THE BEST Mshauri wangu na Mtumishi wa Mungu. Advocate You’re always THE BEST, mkatuwakilishe vyema huko. Mrudi na Masters ila

pia walau na Kitoto jamani!!’ alisema Calvin kwa utani wakati  
anawaaga!!!!

## **KIPANDE MUHIMU**

Najua umefurahia Riwaya hii, na pasipo shaka umejifunza mambo kadhaa ya kukusaidia.

Ikiwa umeguswa na Riwaya hii na ungelipenda kujenga na kuimarisha mahusiano yako na Mungu, tafadhalii Omba nami sala hii

“Bwana Yesu, Nimeona umuhimu wa kutembea na Wewe maishani mwangu. Ninakuhitaji mno kwenye kila nyanja, tena kwa kila nyakati na majira.

Mimi .....

ninakupokea Yesu uwe BWANA na MWOKOZI wa maisha yangu kuanzia leo. Ninatubu na kuungama kila dhambi na kila uovu kwa Damu ya Yesu.

Tembea na Mimi Roho Mtakatifu maishani mwangu mwote,  
Amen.”

**NIPE USHUHUDA HUU NA WASILIANA NAMI KWA**

**0752/0715 307008**

